ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa na Rais
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
43.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
44.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
45.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
47.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
48.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
49.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake

50.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa Jimbo la Kikwajuni

51.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk Jimbo la Kitope

52.Mhe. Marina Joel Thomas Kateuliwa na Rais

53.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Jimbo la Mkwajuni

54.Mhe. Mgeni Hassan Juma Nafasi za Wanawake

55.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma Jimbo la Bumbwini

56.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

57.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

58.Mhe. Mohammed Said Mohammed Jimbo la Mpendae

59.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

61. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

65.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

66.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

67.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

69.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

70.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

71.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

72.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

74.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

75.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe

76.Mhe. Shawana Bukheti Hassan Jimbo la Dole

77.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni

78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndugu Yahya Khamis Hamad	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Pili – Tarehe 11 Oktoba, 2012

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika (Ali Abdalla Ali) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa idhini yako naomba kuwasilisha mezani mswada wa sheria ya Usajili wa Taasisi za Biashara na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Naomba kuwasilisha.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Katiba na Utawala): Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa idhini yako naomba kuwasilisha hotuba ya maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Mswada wa Sheria ya Usajili wa Taasisi za Biashara na Mambo mengine yanayohusiana na hayo.

MASWALI NA MAJI BU

Nam. 20

Mapinduzi ya Kilimo

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuanzia bajeti yake ya 2011/2012 na hii ya 2012/2013 ina mpango wa kufanya Mapinduzi makubwa ya kilimo kwa kuongeza zao la mpunga kupitia mbegu yake ya Nerika. Na kwa kuwa Nyevule na Nzige ni adui mkubwa wa zao la mpunga, na kwa kuwa wadudu hawa wanashambuliwa sana na kunguru weusi ambao Wizara yako inaendelea kuwateketeza bila huruma.

Je, ni lini Serikali itawaleta kunguru vipaku (Kunguru wa Pemba) ili kuchukua nafasi ya kunguru weusi ili kuwadhibiti Nyevule na Nzige.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais – Alijibu:-

Mhe.Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi suali lake nambari 20, kabla ya kumjibu Mheshimiwa Swali lake namba 20 naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Kunguru weusi wamekuwa na athari mbali mbali za kijamii na kimazingira hapa Zanzibar ambazo ni pamoja na:-

1. Athari kwenye Kilimo na Ufugaji.

    i. Kuharibu na kushambulia viota vya ndege wengine na kula mayai na makinda ya ndege wa asili ya Zanzibar na hivyo kuathiri ustawi wa bio anuwai ya Zanzibar. Hali hiyo imechangia kupotea kwa ndege wa aina mbali mbali kama vile Zuwarde, Mnana, Tongwa, Chozi, Dete, Kijumba na mshare.

    ii. Kunguru weusi wana uwezo wa kueneza magonjwa mengi kama vile maradhi ya matumbo kutokana na tabia yao ya kutua na kula kwenye uchafu wa kila aina ya mizoga na hata kwenye majaa ya hospitali. Aidha kunguru hudondosha uchafu na hasa wa mizoga katika vianzio vya maji na kuyafanya yasiwe salama.

iii. Kunguru weusi ni wadokozi wa vyakula kila mahali watakapokiona majumbani na kwenye mahoteli au mama lishe. Kunguru husababisha usumbufu kwa watalii ikiwa ni pamoja na kuchafua maeneo ya mahoteli jambo ambalo linatishia ustawi wa utoaji wa huduma za kitalii hapa nchini.

iv. Kunguru anasababisha kuenea kwa miti tishio ambayo inaua miti ya asili ya Zanzibar.

v. Kunguru hutua kwenye minara ya simu na kuchukua baadhi ya vifaa muhimu vya minara hiyo. Mhe. Naibu Spika, katika miaka ya hivi karibuni Kampuni ya simu ya Zantel imepoteza zaidi ya shilingi milioni 30 baada ya kifaa kimoja cha mnara wa simu kuchukuliwa na Kunguru Weusi. Hali hiyo pia ilipelekea kukosekana kwa mawasiliano nchi nzima.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe.Saleh Nassor Juma swali lake namba 20 kama ifuatavyo:-

Kwa sasa Serikali haina mpango wowote wa kuwaleta kunguru vibaka kutoka Pemba. Hii ni kutokana na kuwa kunguru vibaka bado wapo Unguja ingawa kwa kiasi kidogo sana, ambapo huonekana katika baadhi ya maeneo ya pwani ya upande wa mashariki pamoja na eneo la Posta Kuu. Hivyo basi, idadi ya kunguru weusi ikiondolewa ni dhahiri kuwa jamii hii ya kunguru vibaka inaweza kuongezeka kwa vile nao ni miongoni mwa ndege ambao wanaothiriwa sana na kunguru weusi.

Ni imani ya Ofisi yetu kuwa baada ya kupungua kwa kiwango kikubwa cha Kunguru Weusi hapa Zanzibar kutapelekea kuongezeka kwa kasi kwa ndege asili mbali mbali ikiwa ni pamoja na kunguru vibaka katika maeneo mbali mbali ya Unguja.

Aidha kuongezeka kwa ndege wa asili hasa yange yange, jore fufu, kunguru vibaka na kadhalika ambao kwa njia moja ama nyengine mayai yao hivi sasa yanaathiriwa na kunguru weusi, kutasaidia sana kupunguza wadudu wa jamii ya nyevule na nzige na hivyo kusaidia katika kuimarisha zao la mpunga hapa Zanzibar.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana na lugha nzuri aliyotumia Mhe. Waziri katika kunijibu naomba niulize swali dogo sana la nyongeza. Kwa kuwa taaluma ya ikolojia inaonesha kwamba hawa kunguru weusi ni moja katika *species* ziliomo katika *given habitat* hapa Zanzibar, na kwa mujibu wa taaluma hii ya ikolojia inaonesha kwamba *within the equal system there is a balance of nature* yaani kuna *independent of food between living organisms.* Sasa unapoondosha *specy* moja *suddenly* kama inavyofanya serikali lazima kutaongezeka *spicies* nyengine ambao ni hawa nyevule na nzige haraka haraka kuja kutuharibia nerika ambayo tumeshaipanda. Je, kwa nini Mhe. Waziri akawa mgumu akatuletea kunguru vipaku kutoka Pemba haraka haraka ili ku-*replace* ile nafasi ya kunguru weusi ili taathira ya nzige pamoja na nyevule isipatikane katika mipunga yetu ambayo tayari tumeshaipanda hivi sasa. Moja.

Pili, Mhe. Naibu Spika, kwa nini serikali inakuwa kaidi katika kuchukua ushauri wetu sisi wataalamu, sisi tunawaambia kwamba katika kudhibiti uharibifu wa baadhi ya wanyama watumie *natural enemy* sio kutumia ma-*chemical* tu. Kwa mfano sasa hivi Pemba tumeshindwa mpaka sasa hivi wale wadudu wa maembe. Je, haoni kwamba tukiendelea kutumia madawa haya kudhibiti hao wadudu wengine na huku mabadiliko ya tabia nchi yanaongezeka sana kuongeza ma- *chemicals* si kujiongezea maradhi katika nchi hii jamani.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Ninakushukuru Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba kwa idhini yako kulipa taarifa kwa mara nyengine tena Baraza lako tukufu akiwemo Mheshimiwa ambaye kauliza swali hili la nyongeza, kwamba kunguru katika historia ya ikolojia ya visiwa hivi sio ndege asili katika ikolojia ya visiwa vyetu hivi. Niliwahi Mhe. Naibu Spika, kueleza historia jinsi gani kunguru hawa waliletwa katika visiwa hivi na hatimae hivi sasa wanatuletea madhara makubwa ndani ya jamii yetu. Kwa hivyo kunguru badala ya kuwa wao ni wageni katika ikolojia yetu wametuondoshea kama nilivyoeleza katika jibu langu mama, ndege ambao ni wa asili na ni wazuri katika ikolojia ya visiwa vyetu.

Lakini swali la pili, ni kwamba kwanza naomba nitoe taarifa tu kwamba hapa Zanzibar Mungu atunusuru hatujawahi kuwa na historia ya kuwa na wadudu wa nzige, tulionao katika visiwa vyetu ni viwavi jeshi. Na si mara

nyingi mashamba yetu ya mpunga kuathiriwa na wadudu hao ambao ni viwavi jeshi na nyevule kama ambao ametaja. Unaweza kukaa katika kipindi cha miaka 3 yaani ni *seasonal*, miaka miwili au mitatu wanatokea na wakitokea Wizara ya Kilimo ina utaratibu ambao yeye ameelezea kwamba haupendi, kuna dawa ambayo inatumika wakulima wanapewa kwa ajili ya kuwaondosha, na shughuli za kilimo cha uzalishaji wa mpunga zinaendelea vizuri sana.

Kwa kupima tu ni kwamba bora kuwaondosha kunguru hawa ambao taathira zake ni nyingi mno katika jamii ukilinganisha na faida ya kuwaondoa nyevule na viwavi jeshi katika mashamba ya mpunga.

Lakini la Pili Mhe. Naibu Spika, serikali hii ni sikivu na haikatai kusikiliza utaalamu wa wataalamu na ambao si wataalamu ndani ya visiwa vyetu katika shughuli zake za kila siku. Lakini tu utaalamu ambao unatolewa ni lazima tukae pamoja ukubaliwe pia na wataalamu wetu kwa lengo la kwamba uweze kuleta faida katika shughuli zetu za kijamii za kila siku katika visiwa vyetu. Utaalamu ambao mwenzetu huyu amewahi kutupa wa kutumia njia nyengine za kuwaua kunguru kwa kweli hauwezi kutumika hapa kwetu kwa kuweza kuwaondoa kunguru, kabla ya kufikia hatua hii ya kutumia sumu ambayo haina madhara makubwa kwa binaadamu. *Research* zilifanyika kwa upeo mkubwa kuangalia ni jinsi gani tunaweza kupata njia ya kuondolewa.

Ninaomba kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba serikali inayo wataalamu na haifanyi mambo haya kwa kubahatisha.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru sana na ninamshukuru Mhe. Waziri kwa kumjibu mtaalamu mwenziwe kwenye suala hili la kunguru. Sasa Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri alipokuwa anajibu swali la msingi alisema kwamba kunguru hawa wamekuwa na tabia ya kufanya uharibifu, na eneo moja ambalo Mhe. Waziri ameeleza ni minara ya simu ambao kunguru hao huchukua vifaa na kuharibu mawasiliano. Naomba kujua kunguru hao hutumia kifaa gani walichonacho ili kuharibu sehemu ya mnara wa simu ili wazanzibari wakakosa mawasiliano.

Pili, muda mrefu nimekuwa nikilalamika kwamba mnara wa mawasiliano wa tigo pale Mtambile, wananchi wa Mtambile na Vitongoji vyake hawapati mawasiliano. Na kwa kweli mnara ule umekuwa kunguru wakitua juu. Hebu atwambie ni sababu hiyo ndio tukapata usumbufu wa mawasiliano.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti kama nimelisikia vizuri kwa ruhusa yako naomba kujibu masuala ya nyongeza mawili ya Mhe. Hija kama ifuatavyo:

Kunguru kwa maumbile yake kuwa kutumia miguu yake na mdomo wake ndio uwezo wenyewe waliojaaliwa na Mwenyezi Mungu ya kuweza kufanya hayo maharibifu ambayo wameweza kuyafanya katika mnara wa Zantel.

Kuhusu suala lake la Pili la kukosekana mawasiliano ya tigo, kwa kweli Ofisi yangu haijaarifiwa juu ya uharibifu wowote ambao umefanywa katika minara ya tigo na kunguru hawa weusi. Ninamshauri tu kwamba awasiliane na Wizara inayohusika Wizara ya Miundombinu ili kujua tatizo hasa liko wapi.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, ninashukuru sana kupata nafasi kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Spika, katika kutoa majibu Mhe. Waziri amesema kuwa haiwezekani kuwaleta kunguru vibaka hapa kutoka Pemba kwa sababu mayai yao yanaathiriwa na hawa kunguru weusi wanaoangamizwa. Lakini kwa kuwa Pemba tayari hivi sasa kunguru weusi wameshafika, na hii ndio athari yao zaidi ya mambo mengine, ana mpango gani wa kuona na kunguru weusi walioko kule Pemba wameangamizwa ili kunusuru kunguru weupe wasitoweke katika jamii. Hilo ni swali la mwanzo.

Swali la pili Mhe. Waziri kasema kunguru weusi hawana asili ya hapa. Swali ni kuwa asili yao ni wapi, waliletwa na nani kwa shughuli gani ikiwa sasa hivi sisi tumeona kuwa wanatia hasara.

Na la mwisho Mheshimiwa kasema kuwa faida inayopatikana na kunguru hawa weusi ni ndogo kuliko hasara kubwa wanayoingiza katika nchi hii. Ni faida gani hiyo na kwa sababu ni faida Wizara ina mpango gani wa kui-*replace* baada ya kuwaondoa hawa kunguru wanaoleta hiyo faida.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mhe. Salim Abdalla Hamad Mwakilishi wa Jimbo la Mtambwe kama hivi ifuatavyo:

Kuna hadithi mbili katika historia ya jinsi gani kunguru wamekuja katika visiwa vyetu. Moja inasema waliletwa kunguru hawa kutokea Persia kwa ajili ya kuja kula mizoga ya maiti. Lakini nyengine inasema waliletwa kama zawadi kwa mfalme katika miaka ya nyuma vile vile.

Swali jengine aliuliza ni kwa jinsi gani Ofisi inajipanga pia katika kuona kwamba kunguru weusi walioko Pemba nao wanaangamizwa ili wasilete uharibifu na kuwaua pia kunguru vibaka. Naomba niliarifu Baraza lako na Waheshimiwa kwa ujumla kwamba zoezi hili ni endelevu litaendelea, tumeanza na hapa Unguja ambapo idadi ya Kunguru weusi ni kubwa sana lakini hatimae tutafanya utafiti na kuwashughulikia pia walioko katika sehemu ya pili ya visiwa vyetu yaani kisiwa cha Pemba.

Mhe. Naibu Spika, naomba Mheshimiwa arudie swali lake la tatu sikulisikia vizuri.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri alipokuwa akijibu hili swali alisema, faida inayopatikana na kunguru hawa weusi ni ndogo kuliko hasara wanayoiingiza katika nchi. Mimi swali langu lilikuwa hapa, Wizara kwa sababu wanaangamiza hawa kunguru weusi ina maana ni pamoja na faida inayopatikana. Kwa sababu ni faida ina mpango gani wa ku-*replace* viumbe wengine ili hii faida isiondoke.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kama nimelisikia swali lake vizuri, nina wasiwasi sana kwamba Ofisi yangu inajipanga namna gani ya kuziendeleza faida zinazopatikana baada ya kuwaua kunguru. Nimuhakikishie tu kwamba faida nyengine ni za kijamii na zinaonekana wazi, hivi sasa tumepokea barua nyingi zinazotupongeza kwa jinsi gani tumeweza kuondoa usumbufu wa kunguru ambao wanaouleta katika mahoteli mengi ya kitalii na walikuwa wakiharibu sifa ya utalii mzuri hapa kisiwani kwetu.

Ni imani yangu kwamba sifa hizi wenyewe zitaendelea kujiendeleza na kuendelea kadri ambavyo kunguru weusi wanaondoka katika visiwa vyetu.

Nam. 22

Kuhamasisha Vijana Kusomea Udaktari wa Magonjwa ya Akili

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:-

Kwa kuwa kadri ya siku zinavyokwenda kunaonekana kuwepo na ongezeko kubwa la vijana kujiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya, matokeo yake ni kupata matatizo ya Afya ya Akili, na kwa kuwa inaonekana kuwa madaktari wengi wanakataa kusomea Udaktari bingwa wa magonjwa ya akili "*Psychiatrist*" na hivyo kusababisha upungufu mkubwa wa wataalamu hao.

Je, Serikali imechukua juhudi gani kuwahamasisha vijana kusomea fani hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi suali lake nambari 22 kama ifuatavyo:-

Ni ukweli usiofichika katika nchi yetu kuwa kuna upungufu wa madaktari bingwa wa fani mbali mbali wanaohitajika wakiwemo madaktari wa magonjwa ya akili *"Psychiatrist ".*

Jitihada zinachukuliwa na Serikali kuondosha upungufu wa madaktari hao.

Kwa wale wanaochagua fani hizo adimu na zenye upungufu kama *Psychiatry* hupewa kipaumbele cha Wizara na hupatiwa udhamini wa mafunzo.

Lakini kama hiyo haitoshi, Wizara kwa makusudi imeweka kipengele cha uuguzi wa maradhi ya akili katika mafunzo ya wauguzi wa Chuo cha Afya Mbweni. Wauguzi wanaume badala ya kipengele cha ukunga wao husomea uuguzi wa maradhi ya akili, lakini hiyo haimfungi muuguzi mwanamke anapoamua kusomea fani hiyo, yeye anaweza kuchagua kipengele anachokitaka aidha ukunga au uuguzi wa maradhi ya akili.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri wa Afya, daktari Mhe. Sira naomba kuuliza swali moja dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa vijana wengi mara nyingi huwa wanapata khofu na wasiwasi mkubwa pale wanapotoa huduma kwa wagonjwa wa sampuli hii ya kichaa. Na kwa kuwa ongezeko la wagonjwa wa kichaa linaendelea kupanda siku hadi siku kutokana na vijana wetu kujiingiza katika haya madawa ya kulevya. Je, Wizara ina mpango gani au serikali ina mpango gani wa kuweza kutoa motisha kwa hawa vijana wetu ambao wanakwenda kusomea udaktari ili motisha huo uweze kuwashawishi, kwa mfano mishahara mizuri pamoja na posho la ziada kwa wanaofanya *Psychiatry*. Ni lini serikali itatoa motisha ya posho pamoja na mafao mengine ya ziada ukiachilia na fani nyengine ili wavutiwe na hii fani ya *Psychiatry* badala ya kuiachia tu kukosa watu kama ilivyo sasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, masomo ambayo yapo katika utaratibu huu sio ya *Psychiatry* tu yapo mengi. Mengi yamo katika fani adimu ikiwemo hilo la *Psychiatry*. Lakini madaktari tulionao hapa hata katika hizo fani za kawaida zinazotakiwa kila siku pia nako kuna upungufu.

Linapokuja suala la mafao na maposho sisi huwa tunafuata taratibu zinazowekwa na serikali. Daktari anapaswa kupewa posho, anapaswa kupewa mshahara kwa mujibu taratibu zilizopo. Fani ya *Psychiatry*, na fani ya uuguzi mwengine au udaktari mwengine wowote tukiuangalia una uzito unaolingana kutegemeana na ile fani yenyewe. Tusifikiri kwamba daktari anayepasua kwake ni rahisi, hakuna kazi yenye *stress* kama ya daktari wa upasuaji. Lakini usifikiri kazi ya daktari anayezalisha na kupasua wajawazito ni kazi nyepesi, nayo pia inampa *stress*. Kwa hivyo madaktari wetu kwa fani zote tatizo hilo ni lao na ni zito kwao.

Lakini daktari anayetaka kwenda kuchukua *Psychiatry*, kwa sisi kama Wizara kumpa kipaumbele na tukamsomesha hata kabla ya wakati wake na tukamlipia ninafikiri hiyo ni motisha tosha kwa daktari yule. Lakini hata hivyo juu ya yote hayo bado daktari kama hataki atabaki kuwa hataki. Tusifikiri tatizo hilo lipo Zanzibar tu, ulimwengu mzima. Kama jana ulisikiliza vyombo vya habari, jana ilikuwa ni siku ya watu wenye maradhi ya akili duniani. Huko ulimwenguni huko basi kuna daktari mmoja tu kila wagonjwa laki mbili, seuze hapa Zanzibar. Kwa hivyo hilo ninafikiri ni tatizo la dunia, kwa hivyo tujitahidi kwa hawa wanaokwenda tuhakikishe wakirudi tunawaweka. Na wapo waliokwenda na *inshaallah* wakirudi watakuwa wamepewa kipaumbele kwa kuwa serikali iliwapendelea kuwapeleka ikawaacha wenzao labda watakaa.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri yenye kutia khofu naomba kuuliza swali dogo sana la nyongeza. Mhe. Waziri kwa sababu umekiri kuwa kuna upungufu mkubwa sana wa madaktari wa *Psychiatry*, je ni ma-*specialist* wa *Psychiatry* waliopo hivi sasa na wangapi wame-*retire*.

Lakini la pili na kama wapo walio-*retire* hatua gani zimechukuliwa na serikali za kuwarudisha kimkataba.
Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, daktari tuliyenaye sasa hivi wa maradhi ya akili tunaye kutoka Cuba yuko pale, na kuna madaktari ambao wanakuja kwa kujitolea, wanakuja na kuondoka sasa hivi tunaye mwengine mmoja. Kwa hivyo tuna madaktari wawili wa jumla pale lakini hakuna mzalendo. Daktari aliyestaafu mwenyewe kwa hiari yake na hana haja ya kurudi ni Dr. Wakil lakini bado anakuja, anakuja clinic siku anazotaka lakini hatutoweza kumrudisha kwa sababu yeye mwenyewe hataki kufanya kazi serikalini.

Nam. 43

Uwekaji wa Taa katika Mitaa

(Mhe. Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hili ameliondoa)

Nam. 29

Juhudi za Ununuzi wa Meli mpya

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:-

Kwa kuwa hivi karibuni tumeshuhudia meli ya Skagit ile ya Kampuni ya Seagull ikizama katika mkondo wa Kibaazi siku kadhaa, na kwa kuwa bado usafiri wa baharini baina ya Unguja na Pemba ni wa kubahatisha mno usiokuwa na uhakika kupitia vyombo vya watu binafsi.

(a) Je, ule mpango wa Serikali kununua meli ya uhakika itakayofanya kazi baina ya Unguja na Pemba bado upo.

(b) Na kama upo, Je, umefikia hatua gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi suali lake namba 29 lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mpango wa Serikali wa kanunua meli ya uhakika itakayofanya kazi baina ya Unguja na Pemba bado upo na unaendelezwa. Serikali imeshafanya maamuzi ya upatikanaji wa fedha na sehemu ya kujengwa meli hiyo.

(b) Meli hiyo tunatarajia itajengwa nchini Korea ya Kusini na Kampuni ya Dual Company Ltd ya Korea ya Kusini ndio itakayo tengeneza meli hiyo

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa fedha za kununulia meli hiyo tayari zimekatwa katika mafungu mbali mbali ya wizara zetu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kwa kuwa ahadi hii ipo na fedha zimeshaanza kukatwa ambapo yametoa usumbufu mkubwa kwa watumishi wa serikali pamoja na walipa kodi wa nchi hii. Je, Mhe. Naibu Waziri anaweza kunieleza ni lini sasa meli itafika na ni kiasi gani kimepatikana.

Kwa sababu kampuni za watu binafsi zinaendelea kuleta meli sisi tunaendelea kusema maneno, ni lini tutaleta meli kwa matendo baada ya kuchapachapa maneno tu.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, utaratibu wa uundaji wa meli hii ni kwamba serikali cha kwanza walichofanya ni kutafuta fedha, baada ya kupatikana kwa fedha serikali imefanya mawasiliano na makampuni mbali mbali na hatimaye kufikia maamuzi kwa kampuni ya Dual ya Korea ya Kusini kuweza kujenga meli hiyo. Lakini katika utaratibu wa kujenga meli hii, serikali inashirikiana na Kampuni ya *International Lio Classification* kwa ajili ya kuipitia na kuihakiki michoro na matumaini ya serikali ni kwamba katika miézi 18 meli hii itakuwa imejengwa na tayari kwa ajili ya kutumika.

Matumaini yetu kwamba meli hii iwe kubwa itakayokuwa na mnasaba na muonekano kama ilivyo meli yetu ya MV. Maendeleo. Kwa hivyo, nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba meli hii katika kipindi hicho cha miezi 18 itakuwa tayari imeshapatiwa ufumbuzi kuundwa kwake.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri yenye kutia moyo wa uhakika naomba nimuulize kuwa hivi karibuni tulishuhudia meli kubwa ya mfanyabiashara mmoja ikiwa imewasili katika bandari ya Zanzíbar. Ni lini meli ile itafanya kazi katika visiwa vyetu kwa maslahi ya wananchi wetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba Kampuni ya Azam Marine ni miongoni mwa kampuni tanzu wamekuja na meli mpya, lakini maumbile ya meli ile ni meli ambayo inatumika katika mfumo wa *row-on row-off* , kwa maana ya kwamba ni meli ambayo inahitaji kufunguka milango kwa ajili ya kushusha mizigo, Magari na vitu vyenginevyo. Kama itakuwa umefanya bahati ya kupita bandarini hivi

sasa kuna marekebisho makubwa sana eneo la *ram* kwa ajili ya kuweza meli ile kuwa *accommodate* na kuweza kutoa huduma kwa wananchi wetu. Matarajio yetu kwamba taratibu husika na miundombinu itakapokamilika meli hiyo itaanza kutoa huduma kwa wananchi wetu.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, baada ya kupata ajali ya *MV. Skagit* vyombo vinavyofanya safari zake Unguja na Pemba vilizuiliwa safari za usiku na baada ya muda mfupi vyombo vimeruhusiwa kufanya safari hizo za usiku. Kulikuwa na maana gani kuzuwia na baadae kuviruhusu.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, madhumuni ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzíbar ni kuimarisha huduma kwa wananchi wake pale tu serikali itapojenga hofu au kuwa na mashaka ya wananchi wake, serikali itaendelea kuchukua hatua za kuimarisha usalama huo. Katika utaratibu huo ndio uliopelekea serikali kusimamisha safari za usiku kwa kujipa muda wa kuzichunguza, kuhakiki na kujiridhisha na baada ya kuona kwamba kuna mapungufu serikali ilizuia safari zile. Lakini baada ya kuona kwamba mapungufu yale yamefanyiwa kazi serikali imeruhusu, lakini azma ya serikali ni kutaka kuona kwamba eneo hili la safari za usiku linaondoka moja kwa moja, tumechelewa kufikia maamuzi hayo moja kwa moja kwa kutambua kwamba yawezekana tukiondoa hivi sasa kwa kutambua kwamba bado huduma ya usafiri haijaimarika vizuri tutasababisha matatizo na usumbufu wa wananchi wetu.

Matarajio yetu ni kwamba, wamiliki na washirika wetu wa shughuli za usafiri baharini vyombo vyao vitapoanza kufanya safari ikiwemo hii meli mpya ambayo tumeizungumza muda mchache uliopita basi utaratibu wa safari za usiku madhumuni ya serikali ni kufungia moja kwa moja na usiwepo.

Nam. 2

Kubinafsishwa kwa Huduma ya Maji

Mhe. Jaku Hashim Ayoub (Kny. Mhe. Saleh Nassor Juma) – Aliuliza:-

Mamlaka ya Maji Zanzibar (*ZAWA*) wameanzisha utaratibu wa wananchi kuchangia huduma ya maji kwa matumizi ya kila siku na tayari wameanza kufunga mita katika baadhi ya maeneo. Ingawa wananchi wanachangia katika kupata huduma hii muhimu bado maji hayapatikani vilivyo katika miji na vijiji kadhaa vya nchi yetu.

Je, ni lini serikali itabinafsisha huduma hii ili kuondosha usumbufu kwa wananchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:-

Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 2 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba Mamlaka ya Maji imeanzisha utaratibu wa kuwafungia mita wananchi ili kuwafanya wananchi hao kulipa kwa mujibu wa matumizi wanayotumia na kuiwezesha *ZAWA* kujiendesha kiufundi.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la ubinafsishaji wa huduma ya maji safi na salama naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kwamba, Serikali bado haijaona kama kuna haja ya kufanya hivyo, kwani wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji bado haijashindwa kuwasambazia wananchi huduma ya maji safi na salama.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu ambayo hayaridhishi yanavunja moyo wananchi wa visiwa hivi siwezi kusema ni ya uongo, lakini mimi nitalithibitishia Baraza hivi sasa kwa muda huu. Kila kiumbe hai kinahitaji maji ni muhimu lakini Mamlaka ya Maji haijawa tayari kuwahudumia watu wa Zanzibar. Mmoja wa miongoni mwa wadau wa mamlaka hii ni mimi, nalithibitishia Baraza tena kwa mara ya pili. Maji yanatoka katika sehemu lakini vitendea kazi hawana zikiwemo gari zenye mkonga wa *crane*, nilisema suala hili kipindi kilichopita katika bajeti nikaambiwa na Mhe. Waziri ipo Nungwi. Nilimwambia kama imenunuliwa jana jioni itakuwa kweli lakini gari haipo.

Katika miongoni mwa watu wanaokosa maji ikiwemo Bwejuu, Pete, Muungoni na Kitogani. Mhe. Naibu Waziri hivi juzi tu mimi binafsi nimetoa shilingi 120,000 kukodi gari ya *crane* kupeleke huduma hiyo kutoa *pump* kisimani, baada ya kutolewa *pump* hiyo imeharibika leo wiki ya pili wananchi wanakosa maji na nimefuatilia nikaambiwa serikali imeshindwa kutoa shilingi 250,000. Leo naomba Mhe. Naibu Spika, aje mhusika anikabidhi shilingi 250,000 hapa ili wananchi wa Muungoni na Kitogani wapate huduma hiyo. Naomba Mhe. Naibu Spika, swali hilo nipate maelezo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, niko tayari kuisaidia Mamlaka ya Maji shilingi 250,000 ikanunue hicho kifaa kilichoharibika cha watu wa Muungoni na Kitogani kukosa maji. Naomba nizikabidhi aje mhusika mbele yako Mhe. Naibu Spika, nimkabidhi leo.

Mhe. Naibu Spika: Hilo ndio swali lako? Wajumbe utulivu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Swali langu Mhe. Naibu Waziri atakuwa tayari kupokea msaada huu kutoka kwangu kwa ajili ya wananchi wangu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, lengo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuhakikisha kuwapatia huduma ya maji safi na salama wananchi wake wa Zanzibar. Nataka nimthibitishie Mhe. Mwakilishi kwamba suala la *crane* ndani ya Mamlaka ya Maji….

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Naibu Waziri swali limeulizwa uko tayari kupokea msaada wa shilingi 250,000 kwa Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, labda niendelee kumjibu maswali kwanza.

Mhe. Naibu Spika: Hilo ndilo swali alilokuuliza pesa anazo je uko tayari kupokea msaada?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Naibu Spika, niko tayari kupokea msaada wake kwa mashirikiano ya kujenga taifa letu.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe tusikilizane na Mhe. Naibu Waziri ukishakujibu maswali uje kuchukua mchango huu.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Naibu Spika, nashukuru kunipa nafasi ili nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa serikali hivi sasa kwa kushirikiana na wafadhili inaendelea na mpango mkubwa wa kuchimba visima katika sehemu mbali mbali katika miji yetu Unguja na Pemba. Na kwa kuwa kutokana na athari ya kimazingira inasadikiwa na inaonekana kwamba kiwango cha maji ardhini kimepungua, hali inayopelekea wakati mwengine kuchimba visima vilivyokuwa havina maji ya kutosha.

Swali, Ili kuepusha tatizo hilo kujitokeza katika mradi huu mkubwa ambao umechukua sehemu ya fedha zake ni mikopo ambayo wananchi watalazimika kulipa, naomba niiulize wizara kupitia Mamlaka kwamba wizara au serikali imeendesha tafiti ngapi kubaini kiwango cha maji kilichopo katika sehemu hizo zilizokusudiwa kuchimbwa visima.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, serikali imefanya tafiti nyingi tu za kuchunguza tatizo la maji Zanzibar, ingawa siwezi nikamtajia idadi maalum kwa sasa hivi lakini nimthibitishie kwamba serikali imejitahidi kufanya uchunguzi na inaendelea kufanya uchunguzi na kuhakikisha kulipatia ufumbuzi tatizo hili ili wananchi waondokane na kadhia hii iliyowakabili.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nami kuweza kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri swali la nyongeza. Pamoja na majibu yake mazuri kwanza niipongeze Mamlaka ya Maji kwa jitihada zao za kufikisha maji vijijini na sio mjini. Je, Mhe. Naibu Waziri sehemu zilizobaki kuanzia Mkadini, Kazole Mwembe Amari ni lini utaweza kuwafikishia maji wananchi hao ili wanufaike kama hao ambao umeshawafikishia maji hivi sasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, lengo la wizara yangu kama nilivyoeleza kwamba ni kuwasambazia wananchi wake wote huduma ya maji safi na salama. Kwa hivyo, vile vijiji vyote ambavyo havijanufaika na huduma hiyo basi wizara yangu inawaangalia na itajitahidi kuwapelekea huduma hiyo ya maji safi na salama.

Nam. 25

Soka la Wanawake Zanzibar

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:-

Soka la Kinamama limechukuwa nafasi pamoja na tunzo kubwa katika medani ya Kimataifa. Kwa kuwa hadi leo hii Zanzibar haionekani kujishughulisha na mchezo huu kwa akinamama.

(a) Je, ni sababu gani inayoipelekea wizara kutokutilia nguvu mchezo huu kwa akinamama.

(b) Je, hii ni sera ya nchi au ni katika kuenzi mila na silka za Kizanzibari.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 25 lenye vifungu a na b kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, wizara yangu kwa kweli inatilia nguvu Soka la Kinamama, kwa sababu soka hili lipo na linaendelezwa kupitia Chama cha Soka Zanzibar (*ZFA*). Kwa hivyo, vipo vilabu mbali mbali ambavyo viliwahi kusaidiwa na Baraza la Taifa la Michezo na wizara. Katika kuendeleza hili haionekani kuwa linavunja mila na silka za Kizanzbari kupitia soka la akinamama.

Napenda kumhakikishia Mheshimiwa kuwa wizara inatilia mkazo soka la kinamama ili ling'are ndani na nje ya Zanzibar. Hata hivyo, tatizo kubwa liliopo sasa ni ushiriki mdogo wa jamii katika kuwapata hao kinamama. Wizara inatoa wito kwa jamii kushiriki katika soka la kinamama ili kujenga afya na kuiletea sifa nchi yetu.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana aliyonijibu Mhe. Naibu Waziri ndugu yangu pale naomba nimuulize swali dogo sana la nyongeza. Kwa kuwa ulimwengu mzima sasa hivi una *advocate gender balance* na kwa kuwa soka la kinamama katika viwanja vya kawaida halionekani. Je, Mhe. Naibu Waziri pamoja na kusema kuwa mmelipa umuhimu hilo soka la kinamama wanacheza katika viwanja vya ndani au hivi vya kawaida. Hilo la kwanza.

La pili, kwa sababu akinamama siku zote wanadai haki sawa pamoja na wanaume huoni akinamama kuwa hawaonekani katika mchezo kama huu huoni kuwa kinamama hamjafika kiwango cha kutaka *gender balance* katika nchi hii kwa sababu nyinyi mnashindwa kucheza *foot ball*.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, kama nilivyojibu katika swali mama kwanza unatakiwa ushiriki kwa waheshimiwa wote kuhamasisha kwenye majimbo yao ili wanawake na wao wawe na kipaumbele zaidi kwenye soka hili. Lakini nataka nimhakikishie Mhe. Mwakilishi nikiwa ni Naibu Waziri mwanamke aangalie kwenye Baraza hili la Wawakilishi juzi tu tulikwenda Arusha kwa kweli ilikuwa mimi ndiye msimamizi mkuu kwenye soka hili la wanawake na namhakikishia soka hili litaendelea na kwa kushirikiana na wao Waheshimiwa Wawakilishi kwenye majimbo yao ili tuweze kuendelea na sisi wanawake tuwe tunaingia kwenye soka hili hata kwenye shughuli zote zinazotakiwa kwenye serikali na hata kuingia katika shughuli za soka za nje na sisi pia tuweze kuingia Mhe. Mwakilishi.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kwanza na mimi nichukue fursa hii ya kumpongeza Mhe. Hussein Ibrahim Makungu maarufu Bhaa kwa kuweza kushinda ushindi wa kishindo katika Jimbo la Bububu katika uchaguzi uliopita.

Mhe. Naibu Spika, mpira huu wa *foot ball* wa wanawake hapa Zanzíbar bado haujakuwa makini, ningependa kumuuliza Mhe. Naibu Waziri ni vilabu vingapi vya timu za wanawake viliopo Zanzíbar.

Pili, timu ya *Zanzíbar Queen* imeshiriki mashindano gani katika Afrika na katika *East Africa* katika mashindano ya wanawake.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mwakilishi kwa kweli vilabu vya wanawake nitamletea kwa maandishi na yeye akiwa Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Rahaleo alikuwa ni Katibu wa *ZFA* Zanzíbar naomba mashirikiano yako ya pamoja ili tuweze kuviendeleza vilabu hivi vya wanawake.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante Mhe. Naibu Spika, napenda kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moa la nyongeza. Kwa kuwa hivi sasa katika wilaya zetu Unguja na Pemba wameshaanzisha timu hizo za mchezo wa *footbal* kwa kinamama. Je, Mhe. Naibu Waziri wizara yako ina mpango gani wa kuziendeleza timu hizo. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, kwa kweli kipindi kilichopita nilijibu swali kama hili na nikaeleza kuwa tuwe na mashirikiano ya pamoja ili kuziendeleza hizi timu zetu za wanawake za *netball* na *footbal*.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Afya ya Jamii na Mazingira ya Mwaka 2012

(Kusomwa mara ya pili)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe naomba nitoe taarifa kwamba kwanza kuna tangazo limeletwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu, anaarifu kamati yake kwamba saa tano wakutane kwenye ukumbi wa juu kuna masuala muhimu.
Waheshimiwa Wajumbe naomba sasa hivi nimpe nafasi Mwanasheria Mkuu na baadae nimwite Naibu Waziri wa Afya na baadae amalizie mwenyewe Mhe. Waziri kufanya majumuisho. Kwa hivyo naomba Waheshimiwa msitoke ili msikilize zile hoja zinapojibiwa. Mtu yeyote ambaye atakuja kuuliza hoja ishajibiwa alikuwa hayupo hatutoisikiliza hoja yake. Tunawashauri mbaki msikilize ili tuweze kwenda vizuri katika majadiliano yetu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Naibu Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu naomba nikushukuru na wewe binafsi kwa kunipa fursa hii ya kuchangia katika hoja ya mswada huu na mimi kutoa maoni yangu au mchango wangu katika kufanikisha hoja hii ambayo iko mbele yetu.

La Pili, naomba na mimi nichukue fursa hii kumpongeza kwa dhati Mhe. Hussein Ibrahim Makungu kwa kuchaguliwa kuwa Mwakilishi wa Jimbo la Bububu na tunamkaribisha sana.

Mhe. Naibu Spika, zimetolewa hoja nyingi kuhusiana na suala la mswada huu, mimi naomba nichangie katika maeneo machache ili kusaidia na mimi kutoa maoni yangu kuhusiana na ninavyouona mswada huu.

Suala la kwanza nashukuru kwamba Waheshimiwa Wajumbe takriban wote wameafiki kwamba kuwa na sheria hii ni muhimu sana. Mhe. Naibu Spika, naomba niwakumbushe wenzangu kidogo historia ndogo au fupi ya sheria ya afya ya jamii kwa upande wa Zanzíbar. Na pengine historia hii ndio itatusaidia kujua kwamba kwa kweli leo tunapitisha mswada ambao ni muhimu sana kwa afya zetu, kwa maisha yetu, kwa ustawi wetu na vizazi vinavyokuja.

Mhe. Naibu Spika, kwanza sheria ya afya ya jamii kwa Zanzíbar ni miongoni mwa sheria ambazo zilitungwa mapema sana na sheria ya Mwanzo Nam. 4 ya mwaka 1909 ni miongoni mwa sheria za mwanzo kabisa kutungwa Zanzíbar, fikiria vatu 1909 walitunga sheria ya *public health* kwa kuona kwamba inahitajika na kuna mambo kadhaa ambayo yalizungumzwa katika sheria ile. Sababu kubwa nadhani tukisoma historia yetu utaona kwamba kuna

bwana mmoja anaitwa Major PS, yeye kaandika Mhe. Naibu Spika, kitabu hiki hapa kinachoitwa *Zanzíbar Island Metropolicies of East Africa*. Hiki kitabu kakiandika mwaka 1909, katika hiki kitabu kwanza anaeleza jinsi ya mji wa Zanzíbar ulivyokuwa na moja katika alilokuwa analieleza ni hali ya uchafu uliokuwepo na mpaka ikaja *cholera* kubwa ya mwaka 1869 ikaishitua sana Zanzíbar, mana *cholera* ile watu elfu kumi na tano walifariki.

Sasa ukitizama mwaka huo watu elfu kumi na tano walikuwa ni kiasi gani kwa Zanzíbar. Kwa sababu ukitizama sensa iliyofanywa mwaka 1910 *population* yote ya Zanzíbar ilikuwa watu 197,000; watu 117,000 hapa Unguja na watu 80,000 Pemba. Kati ya hao watu 36,000 ndio waliokuwa wakiishi katika Mji wa Zanzíbar. Sasa hiyo ilikuwa mwaka 1910 sasa jaalia mwaka 1869 ambapo watu 15,000 walifariki dunia, lakini yeye anatema huyu mchango mkubwa ilikuwa ni kutokana na hali ya usafi (*sanitation*) iliyokuwepo na utunzaji wenyewe wa usafi katika mji wa Zanzíbar na ndio moja katika juhudi zilizofanywa kwa sababu huyu bwana baadae alikuja kuwa ni katika *British Resident* wa mwanzo wa Zanzíbar.

Sasa moja ililolifanya serikali ikatunga sheria mapema ni kwa sababu ya kudhibiti usafi katika nchi na ukiangalia utakuta sheria hii imekuwa ikirekebishwa mara nyingi mpaka mwaka 1931 ndio ikatungwa sheria ambayo ni comprehensive, yaani ina masharti takriban yote hayo tunayoyaona leo katika mswada basi asilimia 90 yamechukuliwa kutokana na sheria iliyotungwa mwaka 1931, sheria hiyo ya public health decree sura ya 73 ya mwaka 1931.

Kwa hivyo tunaposema kwamba sheria hii au mswada hatujawa tayari, leo mwaka 2012 lakini watu mwaka 1909 walikuwa tayari. Watu mwaka 1931 walikuwa tayari. Sasa tukizungumza Zanzibar ya leo hatujawa tayari kwa sheria hii, mimi ninadhani tujiulize hilo tena vizuri pengine hili suala tumejiuliza vibaya.

Mhe. Naibu Spika, si kwamba sielewi sababu za Waheshimiwa Wajumbe wengine kusema kwamba pengine sheria hii hatujakuwa tayari. Ninadhani sababu yao kubwa ni suala la usimamizi wa sheria kwa sababu hii sheria tumekuwa nayo ni nzuri sana. Lakini kuacha kuisimamia ndio tumefika hapa tulipo.

Mhe. Naibu Spika, naomba niwakumbushe wenzangu, Wazungu wana msemo wanasema, “failure just like success is a process”. Yaani kama vile mafanikio yalivyokuwa ni mchakato ndio ukafika mafanikio na kufeli nako pia ni mchakato. Unaweza kujiona wewe unafanya na unaelekea kumbe yale unayoyafanya unaelekea kwenye kufeli.

Sasa na sisi tumefanya mengi, tumeacha mengi mpaka tukafika hapa tulipo, sasa ule mchakato wetu umetufikisha tumefika pahala kila mtu sote tunakubali tumefeli katika usimamizi wa hii sheria, lakini hili si la kulaumiwa leo wala wa jana wala au wala wa juzi. Huu ni mchakato tumeuanza siku nyingi sana.

Maana Zanzibar tumefika pahala hivi sasa kufuata sheria unaonekana mshamba, muoga au sio mtu wa mjini. Lakini usimamizi wa sheria Mhe. Naibu Spika, wanasema ni kama triangle. Usimamizi wa sheria unahitaji sheria yenyewe, kipembe kimoja iwepo wananchi na upande mwengine ni serikali.

Sasa mimi ninasema serikali kwa upande wake ina sehemu yake ina jukumu lake equally kama ambavyo wana jukumu wananchi katika kusimamia sheria za nchi. Mifano ipo.

Mhe. Naibu Spika, kuonesha kwamba wananchi wana mchango mkubwa sana katika kusimamia sheria hiyo ndio mifano tunayoisoma katika historia yetu Zanzibar. Maana hili suala linaloitwa la nuisance yaani maudhi. Leo tunapiga kelele kila mtu kelele zimezidi lakini mtu anategemea kwamba serikali ndio iende ikamzuie mtu asifanye maudhi. Serikali ndio inayotegemewa kunguru kafa itoke iende ikamchukue ikamzike, mzoga wa kunguru na sio wa ng’ombe au wa punda aah! wa kunguru. Kunguru amekufa mbele ya nyumba yake anategemea serikali ndio itoke iende ikachukue mzoga ule ikazike wa kunguru.

Lakini kwenye historia yetu Mhe. Naibu Spika, mwaka 1886, wenzetu wa jamii ya Paris walitaka kujenga kitu wanaita mnara wa ukimya. Yaani ‘‘tower of silence’’ hapa zamani pakiitwa kwa Muumiani, pale karibu ya Madema.

Sasa pale walitaka kujenga mnara kwa ajili ya kutimiza ule utaratibu wao kwamba maiti yao wanawaweka pahala wanakauka kwa jua, baadae ndio inakuwa mazishi yenyewe. Lakini waliokwenda Mahakamani kupinga suala lile na wala sio serikali iliyowakataza, waliokwenda Mahakamani ni watu binafsi. Tena mmoja aliyekwenda Mahakamani

ni mwanamke Binti Masoud akiitwa na wakapeleka hoja zao kwamba hii itakuwa ni madhara kwa watu, itakuwa ni usumbufu na maudhi. Mahakama ikakubaliana nao ikatoa amri mnara ule usijengwe.

Mhe. Naibu Spika, ukisoma katika kumbukumbu za sheria kwenye *law report* utakuta kesi nyingi watu wamekwenda Mahakamani kupinga pale Hurumzi kuna bwana kakodi chumba kwa ajili alikuwa daktari, lakini chini wamekodishwa wenzake wahunzi. Akenda Mahakamani akasema hawa wanazofanya kelele hizi zinaudhi na majirani wale wakamuunga mkono. Mahakama ikatoa amri kwamba tafuteni pahala pengine bwana mufanye kazi yenu ya uhunzi, lakini hapa munaudhi watu.

Sasa huko ndiko tunakotoka na sheria ya *public health* kwa kawaida yake Mhe. Naibu Spika, inasimamia zaidi na serikali za mitaa na serikali za mitaa ni za wananchi ndio sehemu kubwa kwa kweli. Sehemu kubwa ya kazi za serikali za mitaa ni kusimamia sheria ya afya ya jamii.

Sasa serikali ya mitaa yenyewe wananchi tumekuwa dhaifu, serikali za mitaa zimekuwa dhaifu na ndio maana hii ni *genetic*. Maana serikali inazaliwa na wazee wake ni wananchi na hizi serikali zao za mitaa, sasa zenyewe kama dhaifu maana yake huo ugonjwa unaendelea mpaka juu.

Lakini jengine katika usimamizi wa sheria tumekuwa na tabia ya kuchukua tabia zetu tukazitia katika usimamizi wa sheria bila ya kutizama kwamba hapa ninasimamia jambo la umma. Kwa hivyo ndio maana mtu aliyekuwa jamaa yake basi huyo hana kosa, ikiwa ndugu yake huyo hana kosa, swahib wake hana kosa. Unaweza ukenda pahala wewe kwa sababu hujulikani ukazuiwa kumbe wewe ndio mwenye haki ya jambo lile. Lakini mtu akapita jamaa yake akamwambia basi pita twende, fanya na ndio maana tumefika pahala kuna vurugu hii.

Lakini na hilo unakuta vitu vyengine tunaviharibu kwa sababu hiyo. Mnazimmoja ni mfano mzuri Mhe. Naibu Spika, kama tunasoma historia ya Zanzibar katika pahala ambapo tungepaenzi kupita kiasi ni Mnazimmoja. Maana huyu bwana kaandika mwaka huo alioandika, anasema Mnazimmoja ndio miongoni mwa pahala pazuri viwanja vya mapumziko katika Afrika kwenye mwaka huo alioandika.

Sasa leo tunapaona tu kuwa ni pahala pa kawaida na tunasema sasa tunataka kupatumia kwa vitu vyengine, lakini pale ndio maana pakatungiwa mpaka sheria tupahifadhi Mnazimmoja. Lakini na jengine ni mihali.

Zanzibari yetu ni ndogo, mihali imekuwa mingi. Sasa kwa muhali huwezi kusimamia sheria. Mifano ipo kwamba sheria inahitaji utekelezaji. Jengine Mhe. Naibu Spika, wakati wa Sultan Barghashi alikuwa na mkewe akiitwa Bi. Moza Binti Hemed, akikaa mjini kule Forodhani.

Moja katika mapenzi yake ilikuwa ni kufuga ng'ombe, kwa hivyo ile nyumba ilikuwa na sehemu chini yeye alikuwa anapenda kufugia ng'ombe. Lakini kuna bwana mmoja yeye ndiye msimamizi wa *public health*, siku zile wakimwita *medical officer of health*. Basi siku zote ilikuwa ugomwi na bibi yule kwamba bwana hapa sitaki pafugwe ng'ombe na mke wa Sultan na huyu *medical officer of health*, lakini ugomvi mkubwa walikuwa wakigombana na Bi. Moza ni kufuga ng'ombe.

Leo nani utaweza kufanya hata kwa swahib zetu tu, sikwambii kwa wengine. Sasa ndio mimi nasema kwamba haya ni mambo ambayo mimi nashukuru kuwa sisi viongozi tumeyaona na nadhani kwa pamoja tusaidiane katika kuyaimarisha mambo haya. Hii sheria ni moja katika ile *triangle* ya usimamizi wa sheria, kwamba uwe na sheria lakini uwe na wananchi wenyewe, uwe na serikali yenyewe zote hizi ziwe madhubuti ndio utaweza kuwa na usimamizi wa sheria ulio mzuri.

Sasa mimi nadhani hii sheria ninaamini kwamba sote tunaiunga mkono na tunaposema hatujakuwa tayari naamini maana yake tafsiri niliyoitafsiri mimi ni kwamba tuimarishe usimamizi wa sheria, ili hii sheria iwe na nguvu. Sasa nadhani hili ni jukumu letu tusaidiane ili tuweze kuimarisha huu usimamizi wenyewe wa sheria.

Lakini jengine Mhe. Naibu Spika, eneo la nne ambalo nilitaka kulichangia kidogo ambalo limezungumzwa ni suala la matangazo ya pombe. Mhe. Naibu Spika, mimi niungane na waliosema kwamba kile kifungu cha 112 nadhani kimefanywa kwa makosa, na mimi naunga mkono kwamba kirekebishwe, nadhani Mhe. Waziri atakapokuja ataleta mapendekezo ya marekebisho. (*Makofi*).

Hili si jambo la ajabu kwa sababu *WHO* yenyewe ina muongozo wa udhibiti wa matangazo ya pombe. *EU* ina sera maalum ya udhibiti wa matangazo ya pombe. Lakini kuna nchi kama Sweden zimepiga marufuku kabisa matangazo ya pombe. Yaani kila nchi ina *restriction* zake, Malyasia wana *restriction* zao kwamba huwezi kutangaza pombe lakini zipo nchi ambazo nazo zimepiga marufuku matangazo ya pombe. Sasa mimi nadhani na sisi tukiendeleza sera yetu, msimamo wetu, maadili yetu kwamba tangazo jambo jengine lakini si pombe. Kwa hivyo hilo mimi naliafiki na kwa kweli nashukuru waliokuwa na macho makali hilo wakaliona na niwapongeze sana kwa kweli. (*Makofi*).

Hili la pombe sisi tuna historia. Tukisema watu wanapenda, wamo wenzetu wanaopenda kweli kweli huu uraibu wa pombe wamo wanaopenda tena kwa miaka mingi sio jambo ambalo limeanza juzi na jana. Pengine ndio maana katika sheria za mwanzo zilizotungwa nchi hii ni sheria ya kudhibiti pombe kali mwaka 1907, halafu ndio ikaja hii pombe ya kizungu.

Hapa tulikuwa maarufu tokea miaka hiyo lakini tukitumia nini, tembo na ndio maana likadhibitiwa tokea miaka hiyo ya 1907. Hata enzi walizokuja Wazungu wakati wa ukoloni lilidhibitiwa mpaka uwe na kibali kulewa, lakini tukubali historia yetu mwaka 1964 katika sheria za mwanzo zilizorekebishwa ni sheria ya pombe kuruhusu kila mtu anayetaka alewe, kila mtu ni uhuru wake. Sasa ni moja katika matunda yetu ya uhuru, huo uhuru jinsi tulivyouona.

Sasa hii ni kuonesha kwamba na sisi kama tunajificha au tunafanya nini lakini ni katika uraibu watu wanaufanya, lakini kwa maadili yetu kilichokuwa hakitakiwi ni hiyo fawahisha ndio ninavyofafanua, kama wewe unakunywa kunywa, ukianguka uangukie mwako, sasa lakini usiwatangazie wengine ukawatafuta na wengine, hili hata na wenzetu nchi nyengine wanalikataa. Kwa hivyo na mimi ninakubaliana nalo.

Lakini suala la sigara Mhe. Naibu Spika, hatujawahi kuwa na sheria wala sera ya kupiga marufuku uingizwaji wa sigara. Bila shaka ina madhara lakini hata maana serikali ilikuwa na kiwanda rasmi wala kiwanda kile sio serikali ilikifunga kama cha Mahonda kisizalishe sigara, kilishindwa kibiashara tu. Kwa hivyo kilichobakia ni ule udhibiti kama ambavyo sheria hii inakusudia kufafanua na kuweka vizuri katika sheria.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho nizungumzie kwa uchache au kwa ufupi suala linaloelezwa kwamba labda mgongano wa sheria hii na sheria nyengine pengine kuna moja hapa ni la tafsiri tu lile alilolieleza Mhe. Jussa kwamba kwa sheria hii ina maana tuna halalisha biashara ya ukahaba, ninadhani ndio hicho wakati mwengine tafsiri ukiikosea au hata *pronunciation* ukiikosea unaweza ukabadilisha maana.

Lakini kilichokatazwa pale sio biashara, yaani isipokuwa biashara ile *business* umeitafsiri kwamba ni biashara, lakini maana yake ni shughuli, yaani shughuli yoyote ya umalaya na vile vitu ambavyo vimeelezwa pale, lakini haikukusudiwa kuwa ni biashara kwa maana ya kwamba sasa basi uende tu ukate leseni au ufanye bila ya leseni.

Hilo ni muhimu kwa sababu, lile ukiliweka katika sheria ya *public health* kama ni *nuisance*, maana ya *nuisance*, maana yake ni kitu kinachowaudhi watu, na kwa maana hiyo hutosubiri lazima serikali ije ichukue hatua, wewe mwenyewe mwananchi unaweza ukenda kasema jamani hili kama hiyo mifano niliyoitoa kwamba watu wenyewe wamekwenda Mahakamani wakasema *this is public nuisance*, hawa watu hatuwataki hapa waondoke.

Sasa faida yake ni hiyo na ni vizuri iwemo kwenye sheria na ndio maana ikawekwa kwamba vitendo vile vyote, maana sasa kweli imekuwa ni maudhi. Maana zamani pengine ilikuwa ikijulikana pahala hapa na hapa, lakini sasa unaweza ukamkodisha nyumba mtu *innocent*, kumbe mtu kakusudia kufanya biashra hii, kila siku inatanuka, wenzetu sasa wanasema nao ni sekta isiyo rasmi, si ndivyo wanavyoita *sex industries* kwamba wao ni sekta *almost* takriban rasmi kuna nchi wanachukua kodi.

Sasa sisi hatuelekei huko na ndio maana tukatanua sheria yetu kwa kusema aah! hii tuifanye sasa ni *nuisance* na ikiwa ni *nuisance* maana yake serikali itadhibiti lakini na wananchi wenyewe wanaweza wakabidhi. Lakini jengine ni lile lililosemwa la migongano baina ya sheria hii na sheria ya *Municipal*, la kwanza utakuta sheria ya *Municipal* inazungumzia vitu viwili tofauti. Sheria hii inazungumzia kwa mfano kwenye ku-*set standard* na kuzisimamia zile *standard*. Sheria ya *Municipal* kazi yake ni kutekeleza.

Kama nilivyosema kwamba sheria hii watekelezaji wakubwa ni *local government*. Lakini na pia katika hilo na kwa hivyo ukitazama tokeo hiyo zamani sheria hii kwa mfano *public health decree*, hii ya mwaka 1931, ukitazama na

zile sheria nyengine zote utakuta muna mambo ambayo yanaowana lakini hii sheria kazi yake ni kuweka vigezo na kuhakikisha kwamba vigezo hivyo vinatimizwa na zile mamlaka ambazo zinahusika ambazo ni serikali za mitaa.

Kwa hivyo ukiisoma sheria hii na ukisoma sheria ya *Council* au *Township*, utakuta muna vifungu vingi vinaowana, lakini kwa sababu hii ni sheria kama ni *control law* na wale wengine ni watekelezaji, huyu ndio msimamizi mkuu.

Lakini jengine kuhusiana na hili ni lile lililozungumzwa kwamba sheria tena tunamkabidhi Mkurugenzi Mkuu wa Tiba. Mimi ninadhani ni rai nzuri kwa sababu *public hea*lth kwa kweli ni *eigth percent* ya health. Ukiiweza *public health* kuisimamia vizuri, maana yake unawahakikishia wananchi wako afya kwa asilimia 80, kwa sababu hapa unalitatua tatizo *at source*, kama ni maradhi ya kuambukiza una nini hapa, kama ni maradhi yanayotokana na matumizi ya chakula unayadhibiti hapa, yaani hapa unadhibiti unafanya kinga *at source*, kwa hivyo ninadhani ni suala zuri lakini ukiisoma sheria yetu ya *public service* ina utaratibu maalum wa kuanzisha ile idara.

Kwa hivyo ninadhani kwa hivi sasa ni vyema tukapitisha kama ilivyo, lakini tukatizama hapo baadae kwamba jee kuna haja ya kuwa na *department* ya *public health* ili ule mchakato ulioelezwa kwenye sheria ya *public health* ukafuatwa na ukafanyiwa utafiti ikaonekana, lakini mimi ninasema kama niseme wazi kwamba ninaiona kama ni rai nzuri kwa kweli, kwa sababu hii ina kazi nyingi na inahitaji usimamizi wa karibu na ikisimamiwa vizuri hii basi afya ya wananchi itakuwa imeimarika sana.

Kwa hivyo kwa ujumla mimi ninadhani sote tupongeze juhudi hizi kwamba kwa kweli leo hapa tutakuwa tumepitisha sheria moja muhimu sana katika afya zetu na ustawi wetu na maendeleo yetu. Lakini yale maangalizo yaliyotolewa kwamba yanahitaji usimamizi wa karibu mimi nayaunga mkono sana na vizuri tukajipanga wote tunaohusika katika hili ili tukaweza kuisimamia vizuri tuweze kupata manufaa ya sheria hii ambayo leo naamini tutaipitisha.

Baaada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, ninaunga mkono hoja nakushukuru sana. (Makofi).

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, naomba nikushukuru kunipatia nafasi hii baada ya wale wote ambao wamejitahidi kuifahamu sheria hii na wameichangia kwa nguvu zao zote na wakaonesha wasi wasi wao kwa yale ambayo wameone kwamba yanawatia wasi wasi. Lakini nimshukuru Mwanasheria Mkuu naye kajitahidi kwa kiasi fulani kujaribu kutoa ufafanuzi.

Wawakilishi wetu wametoa malalamiko mengi tu na walikuwa wana haki ya kufanya hivyo, kwa sababu mambo yalikuwa hayaendi vile yanavyotakiwa kuwepo ingawa sheria ilikuwepo. Kama alivyosema Mwanasheria Mkuu inaonekana kwamba usimamizi na wengine wengi wameona kwamba hilo ndilo tatizo.

Kama ni hivyo inabidi sasa suala la usimamizi liwepo na ili suala la usimamizi liwepo lazima kuwe na baadhi ya marekebisho na ndio maana sheria hii ikawepo. Yale yote wali yalalamikia, ina maana kwamba sheria hii ikipita karibu yote yataweza kufuatiliwa kwa sababu kuna sheria ambayo inashughulikia hili.

Lakini sheria hii ukitizama zipo mbili. Kuna sheria hii ambayo tutaipitisha leo na kuna sheria nyengine tutaanza kuishughulikia siku ya Alkhamis ambayo ni ya maafisa wa afya. Maafisa wa afya nao walikuwa hawana sheria ambayo ilikuwa inawa-*bind* au inawalazimisha kusimamia hilo.

Kwa hivyo kama sheria hii itapita vizuri na maafisa wa afya ikapita, kwa hivyo sisi kama viongozi wa kusimamia hapo tutakuwa tuna nguvu ya kulifanya hilo. Kwa hivyo naomba kuwatoa wasi wasi Wajumbe kwamba tuipitishe sheria, yale ambayo walikuwa hawakufahamu ninafikiri wameanza kufahamishwa na ninaimani Waziri atayatolea yale yaliyobakia, lakini kuipitisha sheria hii kuna umuhimu wake na huu ndio wakati hasa wa kufanya hivyo na kesho kutwa tukija kuipitisha hii tutegemee kuwa kutakuwa na mabadiliko kwa sababu kutakuwa kuna usimamizi unaoeleweka.

Kwa hivyo nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi sote kwa pamoja tuiunge mkono sheria hii ya leo ili tuweze kuhakikisha kwamba nchi yetu inakuwa salama, miji yetu inakuwa safi kila mmoja anatimiza wajibu wake.

Ni matumaini yangu kwamba maelezo ya Waziri yatawaridhisha na hatimaye mutaiunga mkono sheria hii.

Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, ninaunga mkono hoja. (*Makofi*).

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya pili kuja kutoa baadhi ya maelezo ya mjadala uliokuwa ukifanyika tangu jana. Naomba nianze kwa kushukuru kiti chako Mhe. Naibu Spika, kwamba umenisaidia sana kwa kuwaongoza Wajumbe watoe maelezo ya kina, na nakumbuka jana kuna mahali mpaka ukataka kumwambia rafiki yangu Mhe. Hamza na akafanya majumuisho nikafikiri labda yeye ni Waziri wa Afya; ahsante sana Mhe. Hamza na nikasema kumbe wamo lakini hawasemwi tu. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, naomba pia kushukuru Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Wanawake na Watoto, kwa kweli wamefanya kazi kubwa, walikaa na wataalamu wetu pamoja na Naibu Waziri wangu, nadhani siku mbili au tatu kuchambua masuala ya msingi yaliomo humu, na sheria yenyewe ni kubwa kidogo *infact* nilipomsikia Bi. Ashura hapa anafanya uchambuzi nikasema eeh! kumbe na yeye kawa mtaalamu kwa sababu ninaambiwa ndiye aliyekuwa akiuliza maswali mengi. Ninakushukuru sana Bi. Ashura.

Mhe. Naibu Spika, nimshukuru sana Mwanasheria Mkuu, unajua tumekuwa na hii tabia ya kukushukuru na kupongeza kama vile ni utamaduni lakini mara nyengine unashukuru kwa dhati yako hasa, kuona kwamba kama haya hayakupata mtaalamu wa aina yake maelezo yangu yasingetimia.

Nilitaka kumtaja mwisho Mwenyekiti wa Kamati Bi. Amina, ninamshukuru alikuja akatoa maelezo mafupi lakini ya fasaha na akaeleza kwamba walilazimika baadhi ya vifungu kuvifuta ili sheria iendelee kuwa njema na baadhi ya vifungu kuviongeza ili ipate maana iliyokusudiwa.

Mhe. Naibu Spika, ni vizuri nikawataja wale ambao wamechangia mswada huu ili kuonesha kwamba tunaithamini michango yao, nao ni:

1. Mhe. Amina Iddi Mabrouk Mwenyekiti wa kamati ya Ustawi wa jamii pamoja na Wajumbe wake.
2. Mhe. Hassan Hamad Omar
3. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
4. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
5. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
6. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak
7. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
8. Mhe. Fatma Mbarouk Said
9. Mhe. Mohamed Haji Khalid
10. Mhe. Ashura Sharif Ali
11. Mhe. Hija Hassa Hija
12. Mhe. Suleiman Hemed Khamis
13. Mhe. Saleh Nassor Juma
14. Mhe. Omar Ali Shehe
15. Mhe. Hamza Hassan Juma
16. Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi
17. Mhe. Mwanasheria Mkuu

18. Pia nimepata mchango wa maandishi kwa Mhe. Ussi Jecha Simai

Mhe. Naibu Spika, wote kwa pamoja nawashukuru na kwa kweli tunathamini michango yao.

Mhe. Naibu Spika, baadhi ya ufafanuzi ambao nilitaka kuutoa basi ameueleza kwa kina Mhe. Mwanasheria Mkuu. Kwa hivyo, mimi nitapitia juu juu tu ili tusichukue muda mrefu kurudia yaliyopita. Mwanzo mjadala ulivyoanza ilionekana kama huu mswada ni mgumu na haukufahamika, ikawa na tafsiri nyingi tu kama alivyosema Mhe. Mwanasheria Mkuu, mpaka ikafika hadi kuonekana labda wakati bado hatujawa tayari. Kumbe ilikuwa ni yale maelezo. Sisi Wizara ya Afya tulikuwa tunajua kwamba ilipofutwa ile sheria ya *caption* 73, kuna mambo mengi yalikuwa hayajaandikwa kwenye sheria nyengine zozote, na kwa hivyo ikapita muda kama kulikuwa na *vacuum*. Sasa sheria hii imetuchukua muda sana kutengenezwa, imebidi tuchukue yale ya zamani yaliyokuwa yanaelezwa na tuione hali ya mabadiliko ya jamii na mwenendo wa kimataifa. Kuna baadhi ya mambo yalikuwa wakati ule hayapo sasa yameingia kwenye afya ya jamii.

Kwa mfano maradhi ya ndege yalikuwa sio suala linalozungumzwa, kuna mambo haya ya ebola yalikuwa hayapo na maradhi mengine mapya mengi tu. Juzi nilikuwa nimetoka safari, nikasoma makala kuna maradhi fulani yametokea yamewapata watu wawili tu, mmoja wa Uingereza na mmoja wa Qatar, wanashtukia anakufa tu wala hawajui sababu, nikasema *Yarabbi Salaama*.

Juzi walikuja madaktari kutoka India ambao wamekuja kuwapima jamaa zetu wa hapa, wakaniambia wameona kitu ambacho sio cha kawaida hapa Zanzibar, ambacho inabidi kifanyiwe uchunguzi. Wamewakuta watoto watatu walipokuwa wanawapima miili yao Pemba kati ya watu waliowachunguza kule Pemba. Kwa kawaida moyo Mhe. Naibu Spika, ule mnofu wake au ile mashine yenyewe kwa *automatic* tangu ilipopigwa *switch* na Mwenyezi Mungu tumboni kwa mama mpaka unakufa, *automatic* inabonyea ile na ikibonyea ndio damu inaingia na kutoka ndio mashine ya kukupa uhai. Wao wamewakuta watoto watatu zile *muscles* za ule moyo ni kachu. Anasema kwa kawaida wagonjwa kiasi 10,000 mpaka 20,000 au 100,000 unampata mmoja. Wao wamewachunguza watu wasiofika 200 Pemba wamewapata watatu, wakapata mshtuko. Akasema katika jamii ya watu 1,200,000 wanawapata watatu hiyo ni asilimia kubwa sana ambayo haihitaji kudharauliwa.

Kwa hivyo, nilichotaka kusema hapa ni kwamba kuna mambo mengi yamebadilika tangu sisi wadogo na wazee wetu waliopita katika suala la ustawi wa jamii ambayo yameibuka, inabidi sasa sheria yetu iyaone hayo umuhimu wake. Kwa hivyo, baada ya maelezo ya Mhe. Mwanasheria, nashukuru Wajumbe watakuwa sasa wameelewa haja na umuhimu wa sheria hii.

Suala la pili lililozungumzwa kwa hamasa na karibu wachangiaji wote ni kuhusu hali ya usafi na mazingira ya jamii ilivyo hivi sasa, kwa hamasa kabisa kwamba samaki wanauzwa chini, makaro machafu na mambo mengi. Mimi pia naelewa hivyo hivyo Mhe. Naibu Spika. Mimi kwa sababu ni Waziri nikienda, wale wanaonitania na vidole wananioteza. Babu unaona mambo yako haya. Ni kweli hali ni mbaya kiasi cha kwamba hatuhitaji kuiacha ilivyo.

Vile vile lilikuja suala la uwajibikaji alilieleza Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa undani sana. Uwajibikaji sheria zipo hatuwajibiki, makosa ni yetu sote. Kasema Mhe. Mwanasheria Mkuu kuna suala la muhali. Hivyo Babu Juma basi nimtie adabu, ndio nimsimamishe. Sasa sheria ni msumeno, Mhe. Hamza Hassan Juma katuambia kuhusu Rwanda, nilikwenda na mimi nimeona usafi wao. Kama hufanyi unapata adabu. Naomba nitoe mfano mwengine Waziri wa Afya wa Rwanda ni mwanamke, lakini ni mwanamke ambaye ni Mwanajeshi, kila mara tunakutana naye katika mikutano yetu ya Mawaziri wa Afya. Eeh bwana ni *mama wa chuma*.

Mhe. Naibu Spika, naomba nitoe mfano wake mmoja katika kulitekekeza hili. Kule kwao afya wanachangia, yaani hizi *insurance policy* na wamegawa *level* kama nne au tano, sina haja ya kuendelea huko. Nikamuuliza sasa wale wasiokuwa na uwezo vipi. Akaniambia wasiokuwa na uwezo ni 24 kwa 100 hao serikali inawalipia. Halafu tena kuna mtu anaweza kulipa kwa mfano shilingi 3,000. Sasa nikamuuliza kama hakulipa kwa mwaka. Akasema hatumtibu. Narudia kama hukulipa hutibiwi, kufa hiyari yako. Sasa nikapiga loo! Huyu mama. Akaniambia lakini kama hatukufanya hivyo, hakuna wajibu wa kuona kwamba na wao wanawajibika.

Mhe. Naibu Spika, kulikuwa na kesi moja jamaa wameiba pesa katika shughuli hizo za *insurance*. Akaambiwa mama yule wakati wa saa tano za usiku, wakati huo huo akapiga simu akamwita Kamishna wa Polisi, kama hapa kwetu ni Bwana Mussa, akamuambia tukutane Wizara ya Afya. Akawaita wale wanaohusika, akamwita na Mkurugenzi wa Fedha wa pale palipoibiwa, akamwambia hatutoki hapa mpaka asubuhi kama sijapata pesa zilizoibiwa, walichanganyikiwa wale jamaa, akasema Kamishna wa Polisi huyu hapa ni lazima munipe *cheque* ya pesa zilizoibiwa kwa sababu mumeiba nyinyi. Wale bwana wakaandika *cheque* kutoka vifungu vingine wakamkabidhi yule mama *cheque* yake, kisha akawaambia haya sasa kalaleni.

Sasa hapa ndio nataka kuonesha ile *seriousness* ya wenzetu katika kuhakikisha kwamba kile kinachostahiki kusimamiwa kinasimamiwa. Kwa hivyo, wale mawaziri wote tukikutana tunamsalimia yule bibi, tunamuambia; *an iron lady.* Muhali ndio uliotufikisha hapa. Sasa swali tubaki hivi hivi, hapana. Ndio maana tukaona tuje na hii sheria tujaze mapengo na tuanze kubadilika.

Juzi tulikuwa na semina na Mhe. Rais pale siku tano na kauli mbiu ni hiyo '*viongozi tubadilike*'. Mimi siku hizi kila nikiandika barua popote pale chini ndio *slogan* yangu. Kama CCM wanasema Kidumu Chama cha Mapinduzi, CUF wanasema Haki Sawa kwa Wote, basi *GNU* Viongozi Tubadilike. Ni lazima tubadilike, vinginevyo kila siku

tutakuja kulaumiana. Waheshimiwa Wajumbe tunaomba mtusaidie kwa upande wenu kama Baraza mnaosimamia mambo ya serikali.

Waheshimiwa Wajumbe, kulikuwa na mjadala juu ya sheria kugongana Mhe. Mwanasheria Mkuu ameeleza na rafiki yangu Mhe. Jaku Hashim Ayoub alikuja na maelezo mengi na kunukuu vifungu. Tumekwenda kuzitizama hizo sheria, sina haja ya kuchukua muda. Sheria zote hizo ambazo alisema labda tunazirudia, zote zinatekeleza sheria ya *public health,* na inasema hasa hii ni katika kutekeleza sheria ya *public health.* Kwa hivyo, Wizara ya Afya ni kusimamia Mabaraza ya Miji na ya mitaa ni kutekeleza.

Mhe. Naibu Spika, sina hakika kama nitajibu masuala yote moja moja, kwa sababu mengi yalikuwa yanafanana. Kulikuwa na hilo suala la kutangaza pombe, ambalo ndio lililojitokeza sana na Mhe. Mwanasheria Mkuu amenisaidia kwa mashirikiano, amesema kwamba kifungu (p) kile itabidi kifutwe na ameshauri kisomeke hivi. Nomba nikisome ili kiingie kwenye *hansard*.

Kifungu cha 112 mbadala ambacho Mhe. Ismail Jussa Ladhu na Mhe. Jaku Hashim Ayoub na wengineo walikisema kwamba kifutwe na walikuja na hamasa sana. Hilo tumelikubali na tumeshauriwa kisomeke hivi.

Kifungu 112(1)

"Itakuwa ni marufuku kutangaza au kushajihisha biashara ya pombe".

Hicho kitakuwa ni kifungu cha 112(1).

Kifungu cha 112(2)

> "Kwa madhumuni ya kifungu hiki kutangaza inajumuisha kutumia njia ya vipeperushi, vijarida, magazeti, redio, televisheni au njia nyengine za kutoa habari kwa vifaa vya *electronic*, ufadhili wa hafla, michezo, au shughuli yoyote, matangazo ya hadhara na njia nyengine yoyote ambayo inafikisha ujumbe kwa watu ndani ya Zanzibar".

Namshukuru Mhe. Mwanasheria Mkuu, kwa hivyo kifungu kile kimekwenda. Kifungu chengine ambacho kilikuwa nacho Mhe. Ismail Jussa na Mhe. Jaku Hashim ilikuwa ni lile suala la biashara ya ukahaba. Mhe. Mwanasheria Mkuu kakitolea maelezo ya kutosha. Sisi tulitaka tuseme jambo moja kama wizara, kwamba na sisi vile vile tunakerwa kuwaona ndugu zetu kina mama wanauza miili yao. Ni kitu cha aibu hasa kwa jamii ya Wazanzibari.

Mhe. Naibu Spika, mara nyingi mimi huwa nasema huko kwenye majukwaa, kwamba hakuna kitu ambacho kinaniudhi kwamba wale dada zetu ambao wanafanya shughuli hii bila kutaka au pengine kwa starehe huitwa changudoa, lakini ndio wanaitwa changudoa. Sio kitu cha kufurahisha. Kwa taarifa yenu mimi nakaa hapo alipopasema Mhe. Mwanasheria Mkuu pale pa Maparis, upande wa urejua nyuma ya *immigration* pale ndipo penye kibanda changu. Wakati wa usiku nikipita na watoto wangu tena wanawake wanawari, wachumba wa kuolewa wanawaona pale wanawake wengine wamesimama wanawangoja watu wenye magari wawachukue. Gari yangu ikipita pale Mwenyezi Mungu nisamehe wanaona labda ndio hiyo, inakera, inaudhi na inasikitisha.

Mhe. Naibu Spika, suala hili ukilitizama lina pande mbili. Lina upande wa wao kudhalilika na lina upande kwamba jamii yetu ya Kizanzibari hailikubali kinyume na maadili ya jamii yetu, lakini muda wote huu ndugu zangu hakukuwa na sheria ya kwenda ukamkamata na kumwambia bwana usifanye biashara hiyo au usifanye shughuli hiyo, inaudhi ukimshika yule ukamwambia polisi mkamate, atakuambia nimshitaki kwa kifungu gani. Dhamira ya kukiingiza kifungu hiki katika kundi la shughuli ya maudhi, na bahati nzuri shughuli hii ya maudhi hukumu yake Waheshimiwa Wajumbe ni kwamba sio kwamba unangojea ukamtafute polisi, amekuudhi mtaani kwako mnashirikiana mnawaita watu hukumu ni hapo hapo, hailali au ikangoja nini ni kwamba inaudhi, bila shaka yanayoudhi sio hili tu kuna mengine. Lakini hiki ni kitendo tunachohitaji kukiondoa katika jamii, lakini hatuwezi kukiondoa kwa kuogopa kusema ukweli wa kitendo chenyewe.

Kwa hivyo, lile neno biashara pale ya umalaya sio kwamba tunakusudia kuhalalisha kwenye sheria, hapana. Sasa ndio lipo na tunataka tulifute, sasa ni lazima tulipe jina, tulipe jina gani basi tunaweza kutafuta jina lolote. Mhe. Mwanasheria Mkuu anasema tuliite shughuli mbaya, shughuli ya kuudhi. Hiyo ndio ilikuwa dhamira yetu.

Vile vile naomba nikumbushe kwamba pamoja na kuwa hapa neno hili limetokeza wazi zaidi, tayari maneno haya yamekuwa yanatumiwa kwenye mambo ya ukimwi. Mhe. Fatma pale ni shahidi wangu tunapotaka kusema kwamba nchi hii ukimwi ni hatari na tunahitaji kuupiga vita, tunajiuliza, uko kwa kiasi gani sasa. Tunasema uko chini ya asilimia moja, lakini makundi yanayoathiri sana ukimwi ni matatu, kila mara tunayataja. Tunasema tunawaita *sex workers*, sasa hapa ni kwa Kizungu tu, yaani ni wakina mama wanaouza miili yao, tunasema wanaume wanaojamiiana wenyewe kwa wenyewe ni matusi sio neno zuri, lakini tunalisema na kundi la tatu ni wale wanaodungana sindano. Kwa hivyo, maneno yasiyofurahisha na ni ya kuudhi bado yamo kwenye midomo yetu na jamii, kwa sababu yale matendo yenyewe ni mabovu, kwa hivyo matendo ni mabaya ni lazima yaondoke na katika kuondoka ni lazima yawemo kwenye sheria. Mhe. Naibu Spika, hilo nilitaka nichukue muda kidogo kulieleza pamoja na maelezo ya Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Kwa hivyo, baada ya mambo haya mawili makubwa juu ya ulevi na juu ya shughuli za kina mama, mambo mengine mengi yalikuwa ni mambo aidha ya kueleza hali ilivyo au ushauri. Sasa katika mambo yaliyoshauriwa. Mhe. Ismail Jussa alisema kuna neno pale mwanzo kwenye sheria tafsiri limeandikwa raia, na badala yake tuandike ukaazi. Hayo nadhani ni mambo ya kurekebisha na tumelikubali neno hili.

Mhe. Naibu Spika, kuna ushauri umetolewa na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, bahati mbaya hayupo hapa, alisema kaenda Marekani kule akala kuku kwa mrija kidogo na vyoo vinavyotembea barabarani na jinsi zile taka zinavyotumiwa. Tunampongeza kwa hilo, lakini alipokuwa anasisitiza kwamba kampuni hii iitwe, tunachomshauri ni kwamba sio shughuli ya Wizara ya Afya, isipokuwa kuna Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ambayo ndio inayoshughulikia mambo haya, na tungeomba kwamba nyaraka au ushauri huu angeupeleka huko kama ni suala linalofaa, ukituita sisi watu wa afya tutafurahi kwa sababu litasaidia katika kufanya usafi.

Mhe. Mwinyihaji Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alinisaidia katika kutoa maelezo hapa akasema kwamba hivi sasa wanashajihisha (*PPP),* yaani *Public Private and Partnership* na kwamba hayo wanayakaribisha na wako tayari. Kwa hivyo, Mhe. Makame Mshimba angekwenda huko atakuwa ametusaidia sana katika kufanya shughuli hiyo ifanikiwe.

Mhe. Naibu Spika, kuna ushauri mwengine mzuri tu uliotolewa na Mhe. Omar Ali Shehe. Kwanza nampongeza, alinisaidia na katika watu walioifahamu hii sheria mmoja alikuwa ni yeye, maana alikuwa anajua hasa nani anayestahiki katika kuwepo mule katika Baraza la Ushauri, na akasema kuna baadhi ya idara nyengine tumezisahau mmoja akasema kwamba ni Idara ya Maji (ZAWA) na kuna watu wengine. Akasema kwamba hivi sasa wanaoteuliwa mara nyingi wanakuwa ni maofisa wadogo ni vizuri wakawa wale waliomo mule, kwa sababu ya hili suala na uzito wake wangekuwa Wakurugenzi ili ule uwajibikaji wa baada ya maagizo ya *council* uwe unafuata mjumbe ambaye keshokutwa anaweza akaulizwa kwenye kamati. Hilo tumelichukua na tunakushukuru na Mhe. Mwanasheria Mkuu pia ame-*acknowledge* kwamba kwa sasa mtu atakayesimamia sheria hii ni Mkurugenzi Mkuu wa Afya, yaani *Director General*. Lakini kwa kweli kazi hii ile Idara ya Kinga ya Wizara ya Afya ilikuwa ni moja katika majukumu yake kusimamia afya ya jamii, lakini imebidi apewe Mkurugenzi Mkuu ili pale anapotoa amri chini iwe anawapa watu walio chini kidogo ya idara yake.

Vile vile Mhe. Omar Ali Shehe akasema kwamba kumekuwa na tabia ya kupitisha kanuni nyingi tu, mawaziri wanapitisha kanuni mara nyengine kanuni zinakuwa kubwa kuliko sheria, akatoa ushauri kwamba basi labda Kamati ya Sheria na Katiba ishirikishwe. Nadhani ni ushauri mzuri, lakini hilo watu wa Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wanaweza kuliona na Idara ya Mwanasheria Mkuu waliendeleze.

Mhe. Naibu Spika, kulikuwa na suala, naomba nikaribie kumaliza, kwa sababu mengine yalikuwa yanarudiwa. Kulikuwa na suala katika kifungu cha 68 ambacho Mhe. Omar Ali Shehe nacho alikisema kwamba kingefanyiwa marekebisho, kwa sababu mtu yeyote kwa kujua atakodi nyumba maradhi haya. Yeye amesema kwamba inawezekana ikawa ni ubaguzi kwamba mtu ana maradhi fulani akawa kakodi nyumba mkimuhamisha mtakuwa na ubaguzi. Nadhani hakutuelewa, hatusemi sisi kwamba mtu mwenye ukimwi umfukuze kwenye nyumba yako aliyokodi. Lakini una taarifa kwamba humo kwenye nyumba hii kuna watu wawili wameshapelekwa hospitali kwa kuharisha au kipindupindu, halafu useme hapana, humo usiende, utakuwa unabagua. Au kuna haya maradhi mapya ya sasa ya kamasi za ndege. Kuna maradhi haya ya ebola.

Mhe. Naibu Spika, juzi kulikuwa na mshtuko hapo Dar es Salaam, alipatikana mtu mmoja sijui kama alikuwa katoka Uganda au wapi, ikawa balaa. Sisi watu wa afya hapa tukaanza kusema eeh! Mwenyezi Mungu asije akapanda boti akajia huku. Sasa haya yatakapokuwa yanatokea Mhe. Omar Ali Shehe basi tutakuwa tunatangaza kwamba kuna maradhi kadhaa na kadhaa, hivyo kama kuna mtu yeyote anayejua au mahali popote ambapo kuna hatari hiyo tuelezwe na bila shaka kwa kawaida huwa tunapiga karantini, hatuchukui mambo tu juu ya kichwa chetu. Hilo lilihitaji ufafanuzi wa kutosha.

Mengine Mhe. Naibu Spika, nadhani tunapopitisha ule mswada kama nitakuwa sikuyaeleza na Mjumbe atakuwa anaona kuna haja tulitolee ufafanuzi basi tutalitolea ufafanuzi. Lakini mengi ya yale ambayo nilitegemea niyaeleze basi tayari yalikuwa yameshafanyiwa uchambuzi na Mhe. Mwanasheria Mkuu, ninamshukuru sana kwa hayo.

Vile vile kulikuwa na suala la kwamba maradhi kutoka nje tutayadhibiti vipi pale gatini, tunahitaji kujiimarisha, lakini hivi sasa kazi hizo zinafanywa. Kuna idara zetu pale zinashughulikia hiyo. Kuna tofauti tu kati ya sheria zinazoshughulikia mambo ya meli imefika vipi, ina vifaa vyote, inastahiki kusafiri kule ni kushughulikia, lakini mambo yote yanayohusu afya na chakula basi yako chini ya Wizara ya Afya na bado shughuli hizo tunaendelea nazo. Kwa hivyo, suala la kumjua nani ana maradhi hayo, kuna suala sasa hili la vitambulisho, vitambulisho vinaweza kuwa ni moja katika kitu kitakachoweza kutusaidia. Itabidi mfumo wetu wa kuingiza watu katika hizi *official port* ubadilike, iwe labda angalau mtu akipita amwambie tunaomba *passport* yako, tumeondoa *passport* mara nyengine hii vururu nayo ina athari. Lakini nadhani hili ni suala la kulitekeleza huko baadae.

Hilo ni suala la msingi katika kudhibiti. Lakini udhibiti hautokei kwenye uwanja wa ndege tu na gatini, unatokea mwahali mwengine ambamo sisi hatumo kwa kawaida, wengine wanakwenda kuvua wanarudi na tumeshawahi kupata maradhi, mtu anapata kipindupindu Tanga anakuja zake, unasikia kipindupindu kimefumuka, huko itakuwa ni halmashauri za miji na mabaraza ya miji yawe yanatusaidia. Pale Mkokotoni kule kwa jamaa zangu sasa imekuwa ni karibu nusu *port,* watu wanakwenda wakirudi mule itabidi tuongeze udhibiti wa kupitia shughuli za mikoa na wilaya.
Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak alikuwa na wasiwasi kwamba je, shughuli hizi zikipita sasa wale kina mama wanaoweka kuni kwenye majumba yao watakuwa hawafanyi. Hatufanyi hivyo. Kama umeweka kuni na tumegundua kwamba hapo pana sababu ya maradhi, hapana, hatuwezi kukusamehe. Lakini kama umeweka kuni ili zisirowe kwa mvua kwa sababu ya masika, hayo sisi hayatuhusu. Lakini kama una makumbi unataka kuchomea vyungu vyako, lakini pana madudu ambayo yanasababisha kuendeleza maradhi, itabidi tushike. Kwa hivyo, tusiwe na wasi wasi ya kuathiri shughuli za jamii ati kwa sababu sheria imesema tutawachukulia hatua.

Mhe. Naibu Spika, nadhani nimeeleza mengi na mengi ya msingi. Yale ambayo nitakuwa nimeyasahau nitawaomba Wajumbe waniwie radhi na pale patakapotakiwa ufafanuzi, nitatoa ufafanuzi huo wa kutosha. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe, ahsante.

Mhe. Naibu Spika: Utoe hoja, yaani utamke kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Waheshimiwa Wawakilishi, naomba kutoa hoja na ninaomba muikubali hoja yangu.

Mhe. Naibu Spika: Sasa niwaulize Wajumbe wote kwa ujumla. Wale walioafiki hoja ya Mhe. Waziri wa Afya wanyooshe mikono. Waliokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Kutunga Sheria, ili kuupitia mswada kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Mswada wa Sheria ya Afya ya Jamii na Mazingira 2012

Sehemu ya Kwanza

Utangulizi

Kifungu 1 – Jina fupi na kuanza kutumika
Kifungu 2 – Matumizi ya sheria pamoja na marekebisho yake
Kifungu 3

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu nasimama mara ya kwanza, basi kwanza naomba nimshukuru sana Mhe. Waziri pamoja na Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa ufafanuzi wao mzuri wa hoja mbali mbali.

Mimi nilikuwa na mambo mawili ambayo niliyachangia. Moja naomba niseme kwamba nitalisimamia katika kifungu cha 42 kwa sababu nadhani tunayo njia nyengine ya kulirekebisha lile la tafsiri au athari ya yale maneno kuingizwa katika tafsiri ya neno biashara inayoudhi kwamba kuna maneno ya ukahaba na umalaya.

Lakini ninachotaka kusema hapa katika mchango wangu jana hapa Mhe. Mwenyekiti, nilipendekeza mbali ya mambo mengine ambayo nashukuru serikali imeyakubali kwamba katika tafsiri ya udhia na kwenye tafsiri ya maneno ya biashara inayoudhi nilipendekeza kwamba pia tujumuishe hizi biashara za muziki unaopigwa katika maeneo ya wazi, kwa sababu nilisema ina athari pia hata kiafya, kwa sababu muziki ukiwa mkali na kila siku ukipigwa katika sikio unaweza kuleta athari katika afya pamoja na kuleta usumbufu.

Sasa nilipendekeza na hili Mhe. Waziri alichukue na rekodi za *hansard* zikae sawa Mhe. Mwenyekiti naomba kupendekeza kwamba kwenye tafsiri ya udhia katika *paragraph* ya mwisho kabisa baada ya (f) kuna maneno yanayosema kwamba “na unaweza pia kuhusika na pahala, maji au ardhi iliyofunikwa na maji, mnyama akiwa hai au mfu, taka, vumbi, moshi, mvuke baada ya neno hili liongezwe neno kelele, yaani mvuke, kelele au kitu chengine chochote chenye kutoka”. Hilo napendekeza likae hapo.

Vile vile katika biashara inayoudhi tuongeze pia biashara ya kupiga muziki.Kwa hivyo, napendekeza maneno haya mawili yaingie hapo Mhe. Mwenyekiti kama nilivyopendekeza jana, kwa sababu sikuyasikia katika majumuisho ya Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, sina pingamizi na marekebisho hayo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na naomba tuendelee. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba nitoe tahadhari kidogo, maana yake Mhe. Ismail Jussa Ladhu alisema kwamba biashara ya muziki, nafikiri alitaka liongezwe hilo neno, sasa kama lengo ni muziki basi ile biashara itolewe, kwa sababu kama mimi nyumbani kwangu sifanyi biashara na nimeweka yale madubwana wakati wowote ule huwezi kunikamata. Kwa hivyo, naomba irekebishwe na iwe ni muziki tu ambao ni wa hali ya juu kabisa. *(Makofi)*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, mimi sina pingamizi na yote ikiwa yeye mwenyewe Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria amebobea zaidi katika fani hii kuliko mimi na hilo naliheshimu, ikiwa yeye ataniridhisha kwa sababu hapa tafsiri ya juu ni ya udhia, sasa katika udhia tutaongeza kelele na muziki ikawa ni jumla ya udhia nadhani itakuwa imekaa vizuri.

Lakini cha pili kinazungumzia biashara inayoudhi ndio maana nikatamka kwamba hapa tuongeze biashara kwa sababu hapa pametajwa kwa mfano biashara za kuchoma mkaa, kuchoma chokaa, ukamuaji mafuta na katika Kiingereza imetumika *offensive trade* ndio neno lililotumika. Kwa hivyo, nadhani atusaidie zaidi kwamba akiona tukitia muziki inatosheleza kwa tafsiri hiyo au mpaka tui-*qualify* basi mimi nitakuwa sina matatizo.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee na halafu tutaweka inavyohusika.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nirudie kwenye tafsiri ya maneno ya maradhi yenye kuambukiza nikihusisha na kifungu cha 68, kwamba mtu yeyote kwa kujua atakodi nyumba au sehemu ya nyumba ambayo mtu mwenye vijidudu vya maradhi ya kuambukiza ameishi au mtu yeyote aliyeumwa na maradhi ya kuambukiza kitu kama hicho.

Sasa tatizo langu liko kwenye tafsiri na Mhe. Waziri alituambia kwamba katika hali hii ni yale maradhi ambayo yatatangazwa na Mhe. Waziri kwa kila wakati au wakati yatakapotokea. Sasa nahisi kwamba iwapo tutatia tafsiri hii katika sheria, basi nadhani itakuwa inaathiri moja kwa moja katika kifungu hichi.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema jana kwamba dunia nzima pamoja na sisi tunakubaliana kwamba tuondoshe unyanyapaa kwa wenzetu hawa ambao wanapata janga hili la maradhi ya Virusi vya UKIMWI. Kwa hivyo, tafsiri hii moja kwa moja inawagusa wao, kitu ambacho tunajua sote kwamba maradhi haya ya UKIMWI ni maradhi ya kuambukiza lakini kwa njia maalum na kuna mafundisho yanayotuambia kwamba unaweza kugusana na mtu mwenye virusi, unaweza kula sahani moja na mtu mwenye virusi.

Kwa kweli mimi nadhani tafsiri hii kuwekwa ndani ya sheria itakuwa haiendani na ile dhamira ya Mhe. Waziri aliyotuzungumzia. Kwa hiyo, napendekeza kwamba maradhi yenye kuambukiza ielezewe tu ni yale maradhi ambayo yatatangazwa na Mhe. Waziri katika wakati unaohusika. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikifanya majumuisho nilisema kwamba mara nyingi maradhi haya tuliyoyakusudia kifungu hichi kila mara atakuwa Mhe. Waziri anayatangaza, sasa tukeshakulitangaza tena huwezi kuja kutuambia kwamba tusikuhamishe au tusikupige karantini pale.

Vile vile maradhi ya UKIMWI yana kundi lake peke yake ni tofauti na hili, kwa sababu maradhi ya UKIMWI yanapatikana kama ni maradhi, si ya moja kwa moja kama yale ya *cholera* au *yellow fever*, yaani ni maradhi ambayo ukiyangojea kesho tu watu wanateketea.

Sasa huwezi kusema kwamba huyu bwana utambagua kama utamdhibiti hapa kwa sababu ya kulinda haki za binadamu wakati watu wafe, tumesema kwamba tutakuwa tunayatangaza na tukishalitangaza hilo tatizo. Kwa hivyo, hatubishani na Mhe. Mwakilishi kwamba tutakuwa tunatangaza na ndio dhamira iliyokusudiwa.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, ni sawa. Lakini kitu ambacho kinanipa tatizo kwamba tayari tafsiri imeshaeleza moja kwa moja ni aina hii na hii. Sasa kama hivyo ndivyo basi ningeliomba kwenye hii tafsiri tusiende moja kwa moja kuainisha, kwa sababu maradhi yenye kuambukiza maana yake ni maradhi yanayosababishwa na vimelea kama vile *bacteria*, virusi, kupe au kuvu, maradhi ambayo yanayoweza kuambukiza na tafsiri tayari imeshaelekeza moja kwa moja.

Kwa hivyo, mimi khofu yangu ni kwamba iwapo tafsiri katika sheria imeshaelekeza maana yake hata tangazo lake halitokuwa na nguvu isipokuwa sheria ndio itakayokuwa na nguvu zaidi katika tafsiri yake.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nimeifahamu vizuri hoja ya Mhe. Omar Ali Shehe, lakini ukisoma na hicho kifungu cha 68 ambacho amekihusisha na hiyo tafsiri. Madhumuni ya kifungu cha 68 ni kuchukua hatua za tahadhari kuhakikisha kwamba kama kuna kitu ambacho kinahitajika katika hiyo nyumba kufanyiwa usafi kabla ya kuingia mtu mwengine basi zichukuliwe hizo hatua kabla mtu mwengine hajaingia kwenye hiyo nyumba, na wala hii haizungumzii unyanyapaa.

Sasa nadhani kama ni mgonjwa wa UKIMWI kinachozungumzwa kwenye kifungu cha 68 sio kwamba mtu ahamishwe, isipokuwa kinasema kabla ya kuingia mtu mwengine ni lazima zichukuliwe hatua za kuhakikisha kama kuna kitu ambacho kinawezekana nacho ku-*return* vile vimelea vya maradhi, basi kitu hicho kisafishwe.

Mhe. Mwenyekiti, nafikiri kwa *nature* ya maradhi ya namna hii ya mripuko mengine, inaweza kutokea na wala hamjui ni maradhi gani na hata lile jina halijulikani, maana yake hata Mhe. Waziri akitangaza atalitangaza kwa jina gani gonjwa au alipe jina tu yeye mwenyewe. Kwa mfano, inaweza kutokea na kujua kwamba hili linaambukiza lakini huu ni ugonjwa gani, sasa itakuwa shida hata Mhe. Waziri kusema kwamba huo ugonjwa wa ajabu, yaani *administration* yake inakuwa ngumu.

Lakini la pili kutangaza kwa maana ya sheria ni kwamba ichapishwe kwenye gazeti, sasa *by the time* inachapishwa kwenye gazeti watu wengi wanaweza kuwa tayari wameshapotea na Mwenyezi Mungu atuepushie mbali sana, umeingia ugonjwa wa *ebola*, ambao *within* 24 *hours* unaweza kupoteza watu wengi sana, sasa mpaka Mhe. Waziri aje atangaze iende *Press* kama mashine zinafanya kazi na umeme upo itoke.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani hii kwa *nature* ya jambo tunalolishughulikia katika sheria hii, kwa sababu hii tunayoishughulikia ni sheria ya kushughulikia maafa, yaani dharura, mambo ambayo yametokea katika hali ya dharura. Kwa hivyo, mimi namuomba Mhe. Omar Ali Shehe kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti aridhike kwamba hii hapa hakuna unyanyapaa wa aina yoyote, isipokuwa kifungu cha 68 kinazungumzia kuchukua hatua za tahadhari. Kwa maana hiyo, naona hivi ilivyo inatosheleza kabisa.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee. *(Makofi)*

Kifungu 3 – Ufafanuzi pamoja na marekebisho

Sehemu ya Pili
Utawala

Kifungu 4 – Jukumu la Mkurugenzi
Kifungu 5 – Uteuzi na uwezo wa Maafisa wa Afya wa Kanda na Wilaya
Kifungu 6 – Uteuzi na uwezo wa wakaguzi

Sehemu ya Tatu
Usafi na Makaazi

Kifungu 7 – Miongozo bora ya usafi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 8 – Uwezo wa kuweka viwango vya usimamizi takataka
Kifungu 9 – Uwezo wa kuweka viwango vya usimamizi usafi kwa maeneo tofauti pamoja na marekebisho yake
Kifungu 10 – Wajibu wa kusimamia njia za utekelezaji wa usimamizi takataka pamoja na marekebisho yake
Kifungu 11 – Wajibu wa kutosababisha madhara kwa jamii
Kifungu 12 – Usimamizi wa uangamizaji takataka kuwa chini ya uangalizi wa Mtaalamu wa Afya
Kifungu 13 – Kuweka na kushughulikia maeneo ya kutupa taka pamoja na marekebisho yake
Kifungu 14 – Kukataza kuchanganya taka hatari na taka zisizokuwa hatari pamoja na marekebisho yake
Kifungu 15 – Kifungu cha 15 pamoja na marekebisho yake
Kifungu 16 – Usimamizi maji taka pamoja marebisho yake
Kifungu 17 – Usafi wa maeneo pamoja na marekebisho yake
Kifungu 18 – Wajibu wa usimamizi wa taka ngumu pamoja na marekebisho yake
Kifunfu 19 – Utendaji na ubaguaji wa taka ngumu pamoja na marekebisho yake
Kifungu 20 – Uhifadhi na utunzaji wa majaa pamoja na marekebisho yake
Kifungu 21 – Usimamizi wa taka zenye maambukizi
Kifungu 22 – Kifungu cha 22 pamoja na marekebisho yake
Kifungu 23 – Usimamizi wa taka za kitabibu
Kifungu 24 – Usimamizi wa taka za mifugo na kemikali za Kilimo
Kifungu 25 – Usimamizi wa taka za gesi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 26 – Waziri kuweka kumbukumbu za ramani za mitaro ya umma
Kifungu 27 – Mitaro ya umma ya maji machafu pamoja na marekebisho yake

Kifungu 28	–	Mitaro binafsi ya maji machafu kuunganishwa na mtaro wa umma
Kifungu 29	–	Chanzo cha maji na uchafuaji maji
Kifungu 30	–	Jengo au mahala kukidhi matakwa ya afya ya jamii
Kifungu 31	–	Sababu ya kutoidhinisha ramani
Kifungu 32	–	Masharti ya bomba la maji machafu katika jengo na utanuzi wa ramani
Kifungu 33	–	Uwepo wa vyoo katika jengo au mahala pamoja na marekebisho yake
Kifungu 34	–	Ukiukwaji wa Kanuni za Ujenzi
Kifungu 35	–	Uwezo wa Mamlaka ya Upangaji kutoa notisi kuhusiana na jengo liliopo
Kifungu 36	–	Jengo hatari na chakavu pamoja na marekebisho yake
Kifungu 37	–	Ombi la kuondoshwa au kubadilishwa notisi
Kifungu 38	–	Ubomoaji na usafishaji wa mtaa wa ovyo na kuujenga tena pamoja na marekebisho yake
Kifungu 39	–	Uwezo wa Waziri kutunga kanuni pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Nne
Usumbufu

Kifungu cha 40	–	Kifungu cha 40 pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 41	–	Kuzuia usumbufu na kuweka usafi
Kifungu cha 42		

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa mara nyengine tena, jana wakati nipokuwa nikitoa mchango nilizungumzia pamoja na mambo mengine matatizo yangu yale ambayo niliyokuwa nimeyagusa mwanzo kabisa wakati tulipokuwa tukipitisha kifungu cha 3 kuhusu tafsiri ya maneno juu ya kuweza kutokezea kufahamika vibaya kwa kuingia katika tafsiri ya biashara inayoudhi maneno ukahaba au umalaya.

Sasa nilisema nimeachia pale lakini nilisema kuna njia nyengine ya kuirekebisha kwa kutumia kifungu cha 42(1), ambacho hichi kwa ujumla wake kina tafsiri kwa urefu sana maana au mambo yanayochukuliwa kwamba ni udhia au usumbufu.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti nimepata nafasi ya kushauriana na Mhe. Mwanasheria Mkuu hapo na nilikuwa napendekeza kwamba ili isije ikaleta tafsiri ile ambayo tuliyoizungumza jana, basi serikali ikubali moja wapo katika mapendekezo haya mawili na lolote mimi litaniridhi kwa ajili ya kuchukua ile *concern* yetu.

Nakubali kimsingi Mhe. Waziri katika majibu yake tayari alishakubaliana na ile *feeling* yetu ambayo tunayo, lakini namna ya kuli-*accommodate* Mhe. Mwenyekiti, basi napendekeza ama katika kifungu cha 42(1) (g) kwenye ile iliyoandikwa biashara yoyote inayoudhi au biashara yoyote inayoendeshwa, na hapa inaelezwa kwamba inayoweza kuleta athari au hatari kwa jamii au afya ya mazingira, sasa hapa tunaweza kuongezea pia au inayoleta usumbufu au maudhi kwa mtu au jamii. Kwa hivyo, ili nifahamike niisome kwa Kiingereza 42(1)(g) Mhe. Mwenyekiti naomba kunukuu.

Kifungu cha 42(1) (g) kinaeleza hivi:-

> "*Any offensive trade or business so carried on as to be injuries or dangerous to public and environmental health*. Kwa hivyo, nasema ingeweza kuongezwa *or disturbing and nuisance to individual or community*". Hilo ni pendekezo moja Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, au mwisho kabisa katika hicho kifungu cha 42 tungeweza kuongeza maneno kabla ya ile (t) ya mwisho kwa sababu kwenye (t) pameandikwa kitu chochote ambacho ni au kinaweza kuwa ni hatari kwa maisha au

kinaathiri kwa afya na tungeweza kuongeza hii (t) ikawa (u) na kuongeza (t) mpya pale kwa ajili ya kuongeza hiyo ukahaba na umalaya.

Sasa nilikuwa nasema tunaweza kufanya hivyo au kwa Kiingereza nakusudia tungeweza kuiweka pale mwisho kabla ya (t) ya sasa na kuna (t) mpya inayosema *sex working or child prostitution* na halafu ile (t) ikawa ni (u). Kwa hivyo, yoyote katika hayo mawili Mhe. Mwenyekiti ikiwa serikali itayapokea, nadhani Mhe. Mwanasheria Mkuu anaweza kutusaidia, basi nafikiri inaweza kuwa imekidhi ile haja ambayo tuliizungumza jana. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja hiyo na ahsante sana.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwa *observation* yake na alivyokiona hicho kifungu, na kweli baada ya kukiangalia tunahisi tukikirekebisha kitakuwa na faida zaidi katika usimamizi wa hii sheria. *(Makofi)*

Kutokana na sababu hiyo nadhani lile pendekezo lake la pili la kuongeza (t) na halafu (t) ya sasa ikawa (u) ni bora zaidi kwa sababu liko wazi zaidi kuliko lile la mwanzo, nadhani hili la pili lingefaa zaidi kulikubali.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na kwa sababu yeye mwenyewe ndiye aliyenisaidia fikra namna gani ya kukiweka vizuri, basi siku zote vichwa vingi ni tofauti na kimoja, basi nakubaliana na pendekezo hilo alilolikubali.

Kwa hivyo, naomba tuendelee Mhe. Mwenyekiti nikisema tu kwamba kama alivyosema mwenyewe Mhe. Mwanasheria Mkuu katika maelezo yake ya awali kwenye mchango wake, kwamba kwa kusema hivyo haina maana kwamba hatutambui kama vitendo hivi kuwa vinafanyika, lakini kwa sababu sheria yetu inazungumzia afya ya jamii na mambo yanayoudhi jamii ni mambo yale ya kufanyika hadharani, lakini huko binafsi hatuwezi kumzuia mtu asifanye mambo haya.
Mhe. Mwenyekiti, ninachosema na tunachokikusudia hapa ni kukinga, ili jamii isiathirike katika maadili yake. Kwa maana hiyo, nashukuru Mhe. Mwenyekiti serikali kwa mara nyengine kuonesha kwamba inasikia mawazo yetu na wameyakubali na naomba tuendelee. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu 42	–	Mambo yanayoainishwa kuwa ni usumbufu pamoja na marekebisho yake
Kifungu 43	–	Kutoa taarifa ya usumbufu
Kifungu 44	–	Mhusika wa usumbufu
Kifungu 45	–	Kuondosha usumbufu pamoja na marekebisho yake
Kifungu 46	–	Amri ya usumbufu
Kifungu 47	–	Aina tofatui za amri ya usumbufu
Kifungu 48	–	Kutotekeleza amri ya usumbufu pamoja na marekebisho yake
Kifungu 49	–	Usumbufu uliopo katika nyumba inayomilikiwa na watu wawili au zaidi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 50	–	Rufaa dhidi ya amri ya usumbufu pamoja na marekebisho yake
Kifungu 51	–	Mazingira ya kutoa amri ya usumbufu kwa Mkurugenzi
Kifungu 52	–	Kuvunja jengo lisilofaa pamoja na marekebisho yake
Kifungu 53	–	Uwezo wa kuuza
Kifungu 54	–	Uwezo wa kuingia pamoja na marekebisho yake
Kifungu 55	–	Gharama za utekelezaji pamoja na marekebisho yake
Kifungu 56	–	Uwezo wa mtu binafsi kufungua kesi ya usumbufu pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Tano
Kukinga na Kuzuia Maradhi ya Kuambukiza

Kifungu 57 – Uwezo wa Waziri kutangaza maradhi ya kuambukiza pamoja na marekebisho yake
Kifungu 58 – Taarifa ya maradhi ya kuambukiza pamoja na marekebisho yake
Kifungu 59 – Ukaguzi wa jengo pamoja na marekebisho yake
Kifungu 60 – Usafishwaji na uuaji wa vidudu vya maradhi
Kifungu 61 – Njia za kuzuia maambukizi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 62 – Masharti ya njia za kuua vijidudu
Kifungu 63 – Mtu mwenye maradhi ya kuambukiza apelekwe kituo cha afya cha karibu pamoja na marekebisho yake
Kifungu 64 – Kukataa au kudharau kutekeleza amri pamoja na marekebisho yake
Kifungu 65 – Ruhusa ya kutembelea mgonjwa mwenye maradhi ya kuambukiza
Kifungu 66 – Waziri kuweka viwango vya kutupwa taka za maambukizi
Kifungu 67 – Kutupa kusikofaa taka za maambukizi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 68 – Adhabu kwa kukodisha nyumba mtu mwenye maambukizi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 69 – Kosa la kutoa maelezo ya uongo
Kifungu 70 – Kosa la kusambaza kwa makusudi maradhi ya kuambukiza pamoja na marekebisho yake
Kifungu 71 – Nguo zenye maambukizi zisipelekwe kwenye maeneo ya umma kwa kufuliwa pamoja na marekebisho yake
Kifungu 72 - Kukataza kumchukua mtu mwenye maradhi ya kuambukiza katika vyombo vya usafiri wa umma pamoja na marekebisho yake
Kifungu 73 - Pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 74 - Kosa la kuondosha maiti.
Kifungu 75 - Kuzikwa au kuchoma maiti.
Kifungu 76 - Uwezo wa kumkamata mtu mwenye maradhi ya kuambukiza.
Kifungu 77 - Kukataza eneo la maambukizi.
Kifungu 78 - Pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 79 - Udhibiti wa watu waliomo katika chombo chochote aliyekumbana na uambukizo pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 80 - Kuingiza maradhi Zanzibar pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 81 - Uchunguzi wa afya pamoja na marekebisho yake.

Sehemu ya Sita

Maraadhi ya Kutolewa Taarifa Kimataifa na Chanjo

Kifungu 82 _ Uwezo wa kutangaza orodha ya maradhi ya kutolewa taarifa.
Kifungu 83 _ ukaguzi na uchunguzi wa vyombo na wasafiri.
Kifungu 84 chanjo za watu wanaoingia Zanzibar.
Kifungu 85 chanjo ya dharura.
Kifungu 86 chanjo zidi ya maradhi ya watoto pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 87 cheti kutolewa kwa ukamilishaji chanjo.
Kifungu 88 gharama za chanjo.
Kifungu 89 uwezo wa Mkurugenzi kutembelea skuli.
Kifungu 90 gharama za chanjo kwa watoto.
Kifungu 91 uwezo wa kutunga kanuni za kuzuia maradhi ya kutolewa taarifa.

Sehemu ya Saba

Kukinga na Kuzuia Wadudu na Mapanya Waenezao Maradhi

Kifungu 92 mahala kuwekwa bila ya wadudu waharibifu na panya pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 93 katazo la taka katika makaazi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 94 kupuliza dawa kuzuia maradhi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 95 makaro kuhifadhiwa pamoja na marekebisho yake.

Sehemu ya Nane

Maeneo ya Kuzikiwa

Kifungu 96 katazo la kuanzisha maeneo ya kuzikia bila ya kibali pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 97 kuanzisha maeneo ya kuzikia.
Kifungu 98 kutumia chemba za familia za kuzikia pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 99 mamlaka inaweza kutengua sehemu ya kutumika kwa kuzikia pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 100 ufungaji wa eneo la kuzikia pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 101 marufuku ya kufukua bila ya kibali pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 102 uwezo wa mamlaka wa kufukua.
Kifungu 103 uwekaji wa maiti katika makaazi.
Kifungu 104 kibali cha mazishi.
Kifungu 105 ruhusa kwa ajili ya kuchoma maiti.
Kifungu 106 kanuni pamoja na marekebisho yake.

Sehemu ya Tisa

Udhibiti wa Bidhaa za Tumbaku na Ulevi

Kifungu 107 udhibiti wa uingizaji, uuzaji na usambazaji pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 108 udhibiti wa utangazaji.
Kifungu 109 uvutaji sigara hadharani.
Kifungu 110 uwekaji alama maeneo ya kutovuta sigara.
Kifungu 111 katazo la kilevi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 112 tangazo la kutangaza kilevi

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, uungwana ni pamoja na kutokuwa na shukurani panapostahiki, nimesimama tu kwa niaba ya wenzangu ambao tulisimamia kifungu hiki kumpongeza na kumshukuru Mhe. Waziri wa Afya na Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa niaba ya serikali kama ametoa hapa kauli kwa niaba ya serikali kukubali mapendekezo yetu na kukirekebisha sasa badala ya kuzuia kutangaza tu, lakini kupiga marufuku kabisa aina zote za matangazo ya ulevi katika Zanzibar. *(Makofi)*

Naipongeza serikali na nashukuru kwa kuwa sikivu ahsante sana Mhe. Mwenyekiti tuendelee.

Kifungu 112 tangazo la kukataza kilevi pamoja na marekebisho yake.

Sehemu ya Kumi

Huduma za Afya za Bandari

Kifungu 113 kuanzishwa kwa ofisi ya afya bandarini pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 114 uwezo wa maafisa wa afya wa bandari pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 115 uwezo wa maafisa wa afya wa bandari pamoja na marekebisho yake.

Sehemu ya Kumi na Moja

Vifungu vya Jumla

Kifungu 116 mmiliki wa eneo hahitajiki kutolewa maelezo ya ziada pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 117 kutofuata utaratibu na makosa katika nyaraka hayaondoshi uhalali wa nyaraka.
Kifungu 118 kuwasilishwa kwa notisi na kadhalika pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 119 kushindwa kufuata notisi na adhabu ya jumla pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 120 urejeshaji wa gharama.
Kifungu 121 fidia
Kifungu 122 shauri halitafungwa kwa sababu ya kifo pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 123 adhabu kwa kuweka vizuizi.
Kifungu 124 mahkama inaweza ikatoa hati ya kuingia pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 125 adhabu za jumla.
Kifungu 126 ushirikiano na polisi.
Kifungu 127 adhabu bila ya kushtakiwa.
Kifungu 128 Baraza la ushauri la afya ya jamii na mazingira pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 129

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi ili kupata ufafanuzi juu ya kifungu hiki. Kwanza nimshukuru Mhe. Waziri kwa kukubali ule ushauri au maelezo niliyompa kwamba suala hili la afya ya jamii ni suala mtambuka kwamba linahusisha taasisi nyingi na nilizitaja moja baada ya nyengine na Mhe. Waziri ka-*acknowledge* kama ni kweli hilo. Sasa kama hivyo ndivyo, niliuliza jana ni namna gani Baraza hili la Ushauri litahusiana moja kwa moja au sheria hii itahusisha moja kwa moja kati ya zile taasisi ambazo nilizitaja. Sasa kwa kuwa katika kifungu cha 129 kinaeleza kuwa Baraza la Ushauri kiujumla litakuwa na wajibu wa kumshauri waziri juu ya mambo yote ningelipendekeza, kwa sababu kwa vyovyote lazima kuwe na mashauriano na mahusiano ya karibu baina ya Baraza hili na zile taasisi. Bahati nzuri humu katika sheria hii zilitajwa chache tu lakini ziko nyingi kama nilivyotaja.

Kwa hivyo, ningelipendekeza hapa kuwe na kifungu ambacho kitaweza kulifanya Baraza hili lijenge mahusiano ya moja kwa moja na taasisi zile ambazo zinahusiana na mambo ya jamii, kulikoni waziri kuwa zitamshauri au litashirikiana na waziri, lakini Baraza hili kwa sababu ndilo litakalokuwa na jukumu hasa la kiutendaji na kumshauri waziri lakini sasa vile vile liwe na jukumu la kuzishauri au kuzisikiliza au kuwa na mahusiano ya kikazi na zile taasisi.

Mhe. Waziri kakubali kwamba wajumbe watakaoingia katika Baraza hili waingie kwa vyeo vyao hilo ni jambo zuri, lakini tunasema sio hawa tu, ziko taasisi nyingi ambazo zitahitaji zipate mashirikiano na Baraza hili. Nashukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, kidogo nina tatizo, kifungu kinasema Baraza la Ushauri kiujumla litakuwa na wajibu wa kumshauri waziri. Sasa likishakuwa Baraza la Ushauri unapoliachia mtendaji wake au katibu wake awe anahusiana moja kwa moja itakuwa sasa ni Baraza la utendaji sio la ushauri, wanashauri wakishashauri wakishakutana huko wanamwambia waziri katika hali hii tunaona iwe hivi, sasa waziri ndio ana mahusiano na hizo taasisi. Ukitaka kuweka uhusiano na Baraza la Ushauri moja kwa moja na taasisi hiyo inakuwa tena ni *commission* au ni *executive board.* Nilivyoiona hivyo sina hakika kama ni sahihi lakini na Mwanasheria Mkuu atatusaidia.

Baraza likishakuwa la ushauri kuna mtu anashauriwa sasa huyo mtu akishashauriwa ndio anawasiliana na hao wanaotakiwa kuambiwa, likiwa la utekelezaji kutakuwa ni moja kwa moja sasa haiwezi kuwa la ushauri likawa la utekelezaji.

Mhe. Omar Ali Shehe: Sasa kama hivyo ndivyo Mhe. Mwenyekiti, ningelitaka kujua mahusiano sasa ni wapi katika sheria ilipozungumzwa kwa zile taasisi ambazo humu hazimo. Kwa sababu ukiangalia *composition* ya Baraza hili utakuta ni baadhi tu ya zile taasisi ambazo tulizitaja, lakini kuna nyengine ambazo ni muhimu na hapa hazikuainishwa. Sasa ni pahala gani ambapo waziri kama ndiye atakuwa yeye atajenga mahhusiano ya moja kwa moja na zile taasisi ambazo hapa hazipo. Kwa sababu kuna taasisi hapa zipo kama Manispaa ambayo tayari ufafanuzi wake kautoa lakini kuna nyengine hapa hazipo. Sasa Mhe. Waziri ama akubali kwamba hizo aziongeze

hapa katika *composition* ya Baraza hili au azitafutie namna ya kuweza kuwa na mahusiano nazo ya kisheria ya moja kwa moja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, niliyoiona muhimu ambayo haikutajwa hapa ni ile ya maji ambayo tunakubali iongezwe. Ninachoogopa kwamba kila mmoja anayeguswa itakuwa sasa ni serikali ndani ya serikali, litakuwa ni kubwa kiasi cha kwamba halitokuwa tena Baraza la Ushauri itakuwa ni taasisi ambayo ni kubwa mno. Sasa wengine itakuwa wanatekelezwa kupitia hizo idara zilizokuwa wana mahusiano nazo. Niliyoiona yenye kustahiki kuwepo hapa ambayo itakuwa ya saba ni ile ya maji sijui nyengine ipi ambayo tutakuwa tumeiacha kwa maana anayoisema yeye, lakini naogopa tusiweke ikawa sasa dudu kubwa ikawa badala ya kuwa Baraza la Ushauri ikawa kama vile ni wizara mpya nyengine.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, nirudie katika kifungu cha 39 zilitajwa hizi kwamba mawaziri wanaohusika na mifugo na uvuvi, kilimo, viwanda, mazingira, ardhi, makaazi, maji, nishati na serikali za mitaa ni sehemu ya zile ambazo nilizitaja, lakini hebu tuangalie kama hizi *NGOs* sijui zitakuwa na nafasi gani na katika nchi yetu kwa kweli tunahamasisha mashirikiano na *NGOs*. Sasa sijui hapa zitakuwa zina nafasi gani katika hili.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, kuna *NGOs* nyingi zinafika hata mia sasa kama kule kwenye *NGOs* kuna ile wanaita *apex board* ikiwa ile ipo basi mjumbe mmoja atoke huko kama mwakilishi wao, lakini hatuwezi kuweka kila *NGO* ikawa ni mjumbe wa hapa mana ni nyingi imno *infact* kuna *NGOs* nyengine zinafanya kazi *almost* kwa kuisaidia wizara ya afya. Kwa hivyo, kama iko taasisi *apex* ya *NGOs* tutakubali hapa kwamba Mwakilishi kutokana na hizi Kiswahili wanaitaje vile..

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa keshakufahamu huyo. *(Kicheko)*

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa waziri amekubali kuwa ikiwa *NGOs* hizo zinazohusiana na mambo ya jamii wana *umbrella* yao yeye yuko tayari kushirikiana nazo nadhani hilo limekaa vizuri. Ahsante.

Kifungu 129 pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 130 kanuni pamoja na marekebisho yake.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia Mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyooshe mikono. Waliokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mswada wa Sheria ya Afya ya Jamii na Mazingira ya Mwaka 2012

(Kusomwa kwa mara ya tatu)

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Afya ya Jamii na Mazingira ya mwaka 2012 usomwe kwa mara ya tatu.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa niwahoji waliokubaliana Mswada wa Mhe. Waziri wanyooshe mikono. Waliokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mswada wa Sheria ya Afya ya Jamii na Mazingira ya mwaka 2012 sasa umepitishwa rasmi na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe baada ya taarifa ya Katibu niwashukuru kwa ushirikiano mzuri wa tangu jana kuweza kuwasilisha mswada huu, tumeuchangia na sasa hivi tumeupitisha rasmi. Kwa hivyo, sasa tunaendelea na mswada mwengine.

Mswada wa Sheria ya Usajili wa Taasisi za Biashara Zanzibar ya 2012

(Kusomwa kwa mara ya pili)

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kusoma Mswada wa Sheria ya Usajili wa Taasisi za Biashara Zanzibar na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Naibu Spika, kabla sijaanza kusoma Mswada huu naomba nitoe masahihisho kidogo, katika miswada yote miwili ambayo nitaiwasilisha kwenye madhamuni na sababu za miswada hiyo naomba turekebishe kwa sababu zimechanganyishwa, ile madhumuni na sababu ya mswada mmoja wa Usajili wa Taasisi imewekwa katika madhumuni na sababu ya Mswada mwengine wa Mawakala. Kwa hivyo, naomba tufanye marekebisho hayo na baada ya hayo naomba kutoa hoja kwamba Mswada wa Usajili wa Taasisi za Biashara na Mambo yanayohusiana na hayo sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa tumo katika karne ya mashindani ya kibiashara ambapo mtu mmoja yeyote hutafuta njia fupi na sababu ndogo ili aweze kumtangulia mwenzake. Kwa maana hiyo, wafanyabiashara nao mara zote hutafuta njia fupi na zisizokuwa za gharama kubwa katika uendeshaji wa shughuli zao za kibiashara.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na haya, serikali ilikuwa ikipoteza fedha nyingi kutokana na kutokusajiliwa kwa makampuni mengi hapa Zanzibar kutokana na urasimu mkubwa na ada kubwa iliyowekwa na serikali kwa kusajili makampuni hayo ya binafsi. Kilichokuwa kikifanyika ni kwa watu hao au kampuni hizo au jumuiya hizo kuzisajili biashara zao nje ya Zanzibar na hapa kufungua matawi tu (*subsidiary companies*) za biashara zao.

Mhe. Naibu Spika, teknolojia yetu tuliyonayo hivi sasa pia inatulazimisha kufanya marekebisho makubwa katika sheria zetu ili tuweze kwenda na wakati. Wafanyabiashara siku hizi pamoja na kampuni wanatumia sana usajili wa biashara zao kwa kutumia mtandao. Mbali na hayo utumiaji wa mtandao pia unarahisisha upatikanaji wa taarifa na utoaji wa huduma bora katika kazi za usajili. Hii inarahisisha sana katika uanzishaji na usajili wa kampuni duniani.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na hayo basi, madhumuni ya mswada huu ni kupendekeza kutungwa kwa sheria mpya itakayoweka masharti ya usajili wa taasisi za biashara ambapo itawezesha kuanzisha na kurasimisha usajili wa biashara inayomilikiwa na mtu mmoja, ubia, kampuni, Jumuiya za kiraia na vyama vya ushirika na kutoa nafasi ya kutambulika rasmi kwa usajili wa wafanyabiashara wadogo wadogo katika biashara zao na hivyo kutupa nafasi na sisi Zanzibar kuingia katika mashindani ya shughuli hizi.

Pili kuanzisha mfumo wa usajili wa taasisi za biashara na mashirika utakaoendana na vigezo vya usajili vya kimataifa ikiwemo uwazi katika biashara.

Tatu kuweka taratibu za usajili kulingana na teknolojia ya kisasa inayotambulika kimataifa ikiwemo usajili kwa kutumia *internet* (*online registration*) kwa kurahisisha upatikani wa taarifa na utoaji wa huduma bora katika kazi za usajili.

Nne kupunguza gharama za usajili pamoja na kuondoa msururu mkubwa katika kufanya taratibu za usajili ambao umekuwa kikwazo kikubwa katika kuwarahisishia wananchi kusajili na kuendesha shughuli zao hapa Zanzibar. Kiujumla mswada huu umegawika katika sehemu nne na una jumla ya vifungu 25.

Sehemu ya kwanza ya mswada huu inaelezea utangulizi, jina fupi la sheria pamoja na tarehe ya kutumika kwa sheria hiyo. Sehemu ya pili Mhe. Naibu Spika, inahusu uanzishwaji wa masjala ya taasisi za biashara. Sehemu hii ina vifungu viwili yaani kifungu cha nne kinachohusu uanzishwaji wa masjala ya taasisi za biashara na kifungu cha tano kinachoelezea kazi za masjala jinsi zitakavyokuwa.

Mhe. Naibu Spika, sehemu ya tatu inahusu utaratibu wa kusajili na ina vifungu 12. Kifungu cha sita kinazungumzia namna gani maombi ya usajili yanatakiwa yawe na vifungu vya saba hadi 17 vinahusu wajibu wa taasisi ya biashara, wajibu wa kutoa vielelezo, usajili wa taasisi ya biashara na jina la biashara namna ya kuzuwia jina au kupiga marufuku katika baadhiya majina, kipaumbele katika kutumia jina, mapokezi ya maombi, taratibu za usajili, hati ya usajili, usajili wa marekebisho na uondoshaji wa jina kwenye daftari la usajili.

Sehemu ya nne Mhe. Naibu Spika, inahusu kuweka masharti mengineyo ambayo yatasaidia sana uendeshaji wa sheria hiyo. Sehemu hii ina vifungu nane, kifungu cha 18 hadi 25 vinahusu taarifa kwa umma, utoaji wa taarifa, mjumuiko wa makosa, adhabu ya jumla, makosa yanayohusu maofisa, msamaha wa makosa, uwekaji sawa taarifa na kumpa uwezo waziri anayehusika na shughuli hizo ili aweze kufanya kanuni kwa madhumuni ya kuhakikisha kuwa utekelezaji mzuri wa sheria hiyo unapatikana.

Mhe. Naibu Spika, mwisho naomba kutoa hoja na kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe waujadili mswada huu na hatimaye kuukubali ili uweze kuwa sheria kwa kusaidia utendaji mzuri kwa makampuni hayo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Wanu Hafidh Ameir (Kny. Mhe. Ali Abdala Ali, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Mhe. Naibu Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na afya njema kiasi kwamba tumemudu kukutana hapa leo ili kujadili mambo mbali mbali yenye manufaa kwetu binafsi na kwa wananchi wetu kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, pili napenda pia kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu ili niweze kutoa maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Mswada wa Sheria ya Usajili wa Taasisi za Biashara ya mwaka 2012 na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Naibu Spika, naomba pia nimpongeze kaimu waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, Mhe. Nassor Ahmed Mazrui na watendaji wote wa wizara hii kwa mashirikiano yao makubwa waliyotupa wakati wa kuupitia na kuuchambua mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, sitotenda haki ikiwa sitowapongeza Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi kwa kazi nzuri waliyoifanya na hatimaye leo hii nawasilisha maoni ya kamati hii mbele ya Baraza hili.

Mhe. Spika, naomba kuwataja Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

1.	Mhe. Ali Abdalla Ali	Mwenyekiti
2.	Mhe. Panya Ali Abdalla	Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Mjumbe
4.	Mhe. Mussa Ali Hassan	Mjumbe
5.	Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Mjumbe
6.	Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Mjumbe
7.	Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Mjumbe
8.	Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali	Mjumbe
9.	Ndg. Nassra Awadh Salmin	Katibu

10. Ndg. Abubakar Mahmoud Iddi Katibu

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kutoa maoni ya Kamati, naomba kwanza nilipongeze Baraza lako Tukufu kwa kufanya marekebisho ya Kanuni zake na kuingiza kanuni ya 83(2) ambayo inahusiana na Mswada kusomwa kwa mara tatu. Hatua hii imetoa nafasi zaidi kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili kupata muda wa kutosha wa kuipitia kwa umakini na kwa ufasaha Miswada ya Sheria, pamoja na kupata nafasi ya kuwashirikisha wananchi wa Jimbo husika kutoa ushauri wao katika Miswada hiyo.

Aidha, tunaishukuru Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa kutekeleza vyema kanuni ya 84(5) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, kwa kuipatia Kamati hii nafasi ya kuonana na wadau kwa lengo la kuisaidia Kamati katika uchambuzi wa Mswada husika. Kwa msingi huo, tunawashukuru wadau wote waliotoa maoni yao kwa Kamati hii.

Mhe. Naibu Spika, baada ya pongezi hizo napenda sasa niende moja kwa moja kwenye Mswada. Mhe. Spika, Mswada wa Sheria ya Usajili wa Taasisi za Biashara na mambo mengine yanayohusiana na hayo, umetungwa kwa lengo la kuhakikisha kwamba kazi zote za usajili zinaimarishwa kwa kuwekwa Sheria bora.
Mhe. Naibu Spika, Kamati yetu imefurahishwa sana kuona kuwa katika Mswada huu umeainisha mfumo wa usajili wa taasisi za biashara na mashirika utakaokwenda sambamba na vigezo vya kimataifa, ambapo pia utahamasisha utoaji wa huduma maalum kwa kampuni za nje na wawekezaji wa kigeni. Hii itapelekea kutanuka kwa wigo wa biashara za ndani na nje ya Zanzibar ambayo itapelekea kuzidisha kipato kwa wananchi na Taifa kwa ujumla.

Mhe. Nasibu Spika, ni kweli kwamba suala la usajili ni kitu ambacho kina urasimu mkubwa sana. Kwa kuwa kifungu cha 6 na 15 cha Mswada huu wa Sheria vimeweka taratibu za usajili kwa kutumia hata njia ya elektroniki, na kwa kuwa Afisi hii inatarajiwa kuhamia katika jengo lao jipya mnamo mwaka 2014, ni imani yetu kwamba huduma ya usajili kwa kutumia njia hii itapatikana bila ya wasiwasi wowote na hasa tukizingatia kuwa vile vifaa vyote ambavyo vilikuwa havijafungwa kwa kuwa Afisi hii haina jengo la kisasa, sasa vitafungwa na kutumika bila ya khofu yoyote.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na mambo mengine, Kamati yetu inaipongeza Serikali kwa kuweka ndani ya Mswada huu adhabu mbali mbali za kinidhamu zinazolingana na uzito wa makosa kwa wale wote ambao kwa makusudi wataenda kinyume na matakwa ya Mswada huu. Hatua hii inaonesha ni jinsi gani nchi yetu inavyofuata misingi ya Utawala Bora.

Mhe. Spika, baada ya kuupitia Mswada huo, Kamati yetu imependekeza marekebisho kadhaa yenye lengo la kusaidia kuimarisha Mswada huo. Kwa ruhusa yako Mhe. Spika, naomba niainishe baadhi ya marekebisho ambayo Kamati iliyapendekeza kama ifuatavyo;

Katika kifungu cha 3 na katika kifungu chochote kilichijotokeza neno ‘Rekodi’, Kamati imependekeza isomeke ‘Kumbukumbu’. Aidha, katika tafsiri ya neno ‘Daftari la Usajili’ neno ‘Rejista’ limependekezwa lisomeke ‘Daftari’. Hii ni kutokana na kuwa maneno haya yanapatikana pia kwa lugha ya kiswahili.

Mhe.Naibu Spika, Kwa kuwa kifungu cha 7 na cha 8 Maneno yake ya Pembeni yalikuwa yanafanana, Kamati ilipendekeza vifungu hivyo virekebishwe kwa kuzingatia tafsiri ya Mswada wa Kiingereza, ambapo kifungu cha 7 Maneno ya Pembeni yamependekezwa yasomeke ‘Jukumu la Taasisi ya Biashara’ badala ya ‘Wajibu wa Taasisi ya Biashara’ na kifungu cha 8 yamependekezwa yasomeke ‘Haki ya Taasisi ya Biashara’ badala ya ‘ Wajibu wa Taasisi ya Biashara’.

Mhe. Naibu Spika, sambamba na hilo, kwa kuzingatia nakala ya Mswada ya Kiingereza Kamati yetu imependekeza kuwa kifungu cha 10 kisomeke kuwa na vijifungu viwili vidogo, ambapo kijifungu cha (1) kitaishia kwenye neno ‘lililosajiliwa’ liliopo kwenye msatari wa pili wa kifungu hicho na kijifungu cha (2) kitaanzia kwenye neno ‘Jina’ hadi mwisho wa kifungu hiki.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yetu pia imependekeza kufutwa kwa baadhi ya vijifungu kwa kuwa maana zake zinajirudia. Baadhi ya vijifungu hivyo ni; kifungu cha 24(4) ambacho maelezo yake yanapatikana katika kijifungu cha (3) cha kifungu hiki. Aidha, tumependekeza kufutwa baadhi ya vijifungu ile kuleta mtiririko mzuri wa maneno, kwa mfano kifungu cha 20(3) kimependekezwa kisomeke kuwa ni ‘*proviso*’ ya kijifungu cha (2).

Mhe. Naibu Spika, tulifanya pia marekebisho ya uchapaji kama yanavyoonekena katika waraka wetu tuliouwasilisha kwako na nakala ya waraka huo kusambazwa kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili. Kwa msingi huo, na kwa kuokoa muda nawaomba Waheshimiwa Wajumbe waupitie waraka huo, ili kuona baadhi ya vifungu ambavyo sikuvitolea maelezo hapa.

Mhe. Naibu Spika, kwa muhtasari hayo ndio mapendekezo ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusiana na Mswada wa Sheria ya Usajili wa Taasisi za Biashara na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Sasa nawaomba Wajumbe wote wa Baraza hili nao wauchangie vizuri Mswada huu kwa madhumuni ya kuuimarisha zaidi, lakini hatimae kuukubali na kuupitisha bila ya pingamizi yoyote.

Mhe. Spika, natamka bayana kuwa mimi binafsi na kwa niaba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, naunga mkono Mswada huu kwa asilimia zote mia moja.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Wanu kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba Sheria na Utawala.

Waheshimiwa Wajumbe nadhani kwa kuwa mswada tumeusoma sasa hivi tuwape muda Wajumbe wakaupitie, tuje jioni kuanza kuchangia mswada wetu huu uliowasilishwa sasa. Hivyo ninamuomba Mwanasheria atoe hoja ya kuakhirisha kikao hiki hadi jioni kuanza kuchangia mswada wetu uliowasilishwa sasa hivi.

Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa muda uliopangwa kwa shughuli yetu asubuhi hii bado haujamalizika, lakini kwa kuwa ni busara Waheshimiwa Wajumbe wakapata fursa ya kuupitia vizuri zaidi Mswada huu muhimu kabla ya kuuchangia, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likubali kutenga kando kanuni ya muda na tuakhirishe kikao hiki asubuhi hii mapema kabla ya muda wake hadi leo jioni saa kumi na moja.

Naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Saa 6.07 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11.00 jioni).

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendela)

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii kusema mawili matatu ili niwape nafasi wenzangu wajitayarishe.

Mhe. Naibu Spika, nimeusoma Mswada huu kwa kadiri nilivyousoma nimegundua mambo matano ya jumla. Kwa sababu Mswada huu kama unavyosomeka kwenye jina la Mswada kua ni kuanzisha usajili wa taasisi za biashara. Mimi nilikuwa nafikiri huu usajili wa taasisi za biashara upo na taasisi zinasajiliwa, nikaanza kujiuliza kuna haja gani ya kuleta sheria hiyo wakati tayari hii kazi ambayo sheria hii imetaka ifanywe inaendelea kufanywa kwa miaka mingi hapa ndani ya nchi yetu. Nikagundua baada ya kusoma madhumuni na sababu ikanijia katika akili yangu labda mambo hayendi vizuri.

Mhe. Naibu Spika, nchi yetu inakushanya kodi na kodi nyingi zinapitia kwa wafanyabiashara, labda ufanisi wa ukushanyaji wa kodi hauwi mzuri na ndio maana ikaja sheria hii kama kutia nguvu ili wafanyabiashara kuanzia wakubwa mpaka wale wadogo wadogo wawe wanajulikana rasmi tena katika mfumo wa kisasa kabisa, pengine unaweza kurahisisha utaratibu wa ukusanyaji kodi.

Mhe. Naibu Spika, ni ukweli usiofichika kwamba wafanyabiashara wetu wengi hawakushanyi kodi na sio hawakushanyi bali hawazipeleki kodi kunakohusika. Maana mlipa kodi si mfanya biashara, mlipa kodi ni mlaji,

mwananchi wa kawaida ndio anayelipa kodi. Sasa tunapofika pahali kwamba mwananchi analipa kodi, mfanya biashara ni wakala tu wa kukushanya kodi, ikawa hakushanyi kodi au hazipeleki kunakohusika hilo nalo ni tatizo kubwa. Ni lazima kweli serikali itafute namna ya kuhakikisha kodi zinazolipwa na wananchi wetu walala hoi basi zinafika kule zinakohusika.

Nasema katika Mswada huu nimegundua mambo matano.

1) Kuepuka urasimu huu wa usajili, pengine njia zinazotumika sasa hivi urasimu unakuwa mwingi napengine watu wanakaa kwenye misururu mirefu ya kusubiri usajili na kupoteza muda. Moja ni hilo litawasaidia wafanya biashara kuepuka urasimu.

2) Pia kuepuka gharama, maana urasimu ukiwa mkubwa, gharama pia nazo zinaongezeka.

3) Kutumia teknojia ya kisasa. Imeelezwa humu kwamba usajili huu wa mara hii ambao tunautungia sheria tutakuwa tukitumia teknolojia ya kisasa (mtandao wa kompyuta).

4) Jengine ambalo pia litasaidia kwamba mpaka wafanya biashara wadogo wadogo sasa watakuwa wanatambuliwa rasmi na wao watapata kujingaza na biashara zao, japo ni ndogo lakini zitapata *publicity*.

5) Kuimarisha ukushanyaji wa kodi za wananchi. Haya ndio madhumuni.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa naomba sana tuwe na hadhari kidogo, kwa sababu usajili huu umeelezwa humu kwamba haufanywi bure unafanywa kwa malipo. Bila shaka ukishakusajiliwa ukawa unajulikana rasmi kutakuwa na mambo kama ya leseni na mapato na mambo mengine.

Nilikuwa naomba sana hata kama kuna wafanya biashara wadogo wadogo ambao pengine watapata kujulikana rasmi, lakini kwa maumbile ya nchi yetu au kwa mazingira tuliyonayo kuna wafanya biashara ukiwapeleka hapa kutokana na udhaifu wa biashara yao utakuwa umewaongezea mzigo na ugumu wa maisha. Naomba sana wakati wa kutunga Kanuni Mhe. Waziri aangalie kiwango cha mfanyabiashara gani au mfanyabiashara aliye na kiwango cha mtaji wa kiasi gani atapaswa kusajiliwa rasmi na kuingia katika mkondo huu. Tusijetukafika pahali mpaka muuza dagaa kwa tenga tukamsajili na kumtaka ajaze mafomu na mambo chungumzima, tutamfanya asichuuze tena lile dagaa. Nilikuwa naomba sana wakati wa Kanuni Mhe. Waziri hili alizingatie.

Wenzetu ndivyo wanavyofanya kuna viwango ikiwa mfanyabiashara hajafikia basi serikali inaendelea kumlea lea, inamuepusha nay ale magharama mengine ambayo yangemfilisi kabisa. Baada ya kuangalia madhumuni hayo nataka nianze kwenye ufafanuzi.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 3 cha Mswada huu ni ufafanuzi wa maneno mbali mbali yaliyotumika. Mimi binafsi nasikitika kidogo, kwa sababu ninavyojiona mimi si mwanasheria ni mtu nimetoka huko kazi yangu ilikua kuuza madafu, nikaja hapa Barazani kwa sababu wananchi wamenipa ridhaa zao lakini si mwana sheria. Kwa mantiki hiyo maana yake sijui lugha ya kisheria, sijui utaratibu wa kutunga sheria ukoje.

Mhe. Naibu Spika, huu Mswada mpaka ukifika hapa Barazani nafikiri unakuwa umepita katika vichwa vizito vizito, tunasikia mpaka wanasheria kwanza wakae wapange, waumize vichwa wapangue, waandike na wao hawaishii hapo, Mswada unapita kwenye Kamati ya Makatibu Wakuu, sijui unapita kwenye Baraza la Mapinduzi, hata ukifika huku wataalamu wote wamekwisha wa nchi hii. Sasa mimi huwa nasikitika kweli kweli kuwa Mswada mpaka unafika Barazani bado una makosa ya kiuandishi wa lugha, mpaka pia ije hapa na Kamati ya Baraza la Wawakilishi ikae kurekebisha lugha. Mimi nadhani na Mwanasheria Mkuu yumo humu anasikia angewambia wanasheria wake wakawa makini zaidi katika kutunga.

Nashukuru sana hii Kamati ya Katiba na Sheria mambo mengi ambayo nimekuwa nimeyamaki hapa na wao wameyaona. Lakini pale mwanzo Taasisi ya Biashara maana yake ni jambo. Inawezekana hili neno limeandikwa kimakosa, nafikiri ndivyo walivyoona watu wa Kamati ya Katiba wao wamesema ni chombo badala ya jambo.

Ukisema ni chombo inaleta maana nyengine, lakini taasisi ya biashara maana yake ni jambo la kibiashara inakuwa haileti sura nzuri.

Neno la pili biashara binafsi, maana yake ni chombo kisichojitegemea. Sijui Mhe. Waziri atwambie kweli hivi ndivyo ilivyokusudiwa au limeandikwa kwa makosa. Chombo kisichojitegemea au kinachojitegemea. Mimi nahisi sahihi zaidi ni kusema kinachojitegemea. Halafu na hili neno *record* za mapokezi hata mimi sikulipenda hili neno *record*. Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba lugha yetu ya Kiswahili ni masikini sana na imejaa maneno ya lugha nyengine. Kwa sababu ukenda mbali sana hata hili neno 'mrajisi' au 'tarjisi', haya si maneno ya Kiswahili tumeyatohoa kutoka kwenye lugha ya Kiarabu, 'buku' pia sio neno la Kiswahili tumelitohoa kutoka kwa Waingereza, pesa sio neno la Kiswahili. Hii lugha ya Kiswahili ni masikini sana lakini sasa inazidi, maana *record* neno hili ni Kiingereza moja kwa moja, sasa nalo tulizowea kwamba liwe la Kiswahili hili mbadala wake lipo ni kumbukumbu.

Naendelea kuishukuru sana Kamati ya Katiba ya Sheria wameliona hili. Lakini basi mpaka wanasheria wanatumia neno hili, inasikitisha kidogo. Au ukiangalia ukurasa wa 97 kuna daftari la usajili maana yake ni *register*, maana ndio unampoteza mtu zaidi, maana limetoka kwenye daftari sasa limekuwa *register*. Jamani hii tena, bora mambo kama haya madogo madogo wangeliyaangalia vizuri sana wanasheria, wasisubiri mpaka wauza madafu na wauza dagaa wakaja wakawakosoa wanasheria, si utaratibu mzuri kwa kweli. Naomba sana maneno kama yale yawe yanarekebishwa.

Mhe. Naibu Spika, labda niende kifungu cha 24. Maana huu Mswada umeandika vizuri na sisi tuliokuwa sio wanasheria hatuwezi kutoa makosa mengi sana ya kiufundi. Lakini kifungu cha 24 kidogo nimepata tatizo naomba nikisome hichi kifungu.

Kifungu cha 24 (1)

> "Kila taasisi ya biashara iliyosajiliwa kabla ya sheria hii kuanza itachukuliwa kuwa imesajiliwa chini ya sheria hii na ndani ya kipindi cha mwaka mmoja baada ya sheria hii kuanza kutumika, taasisi hizo zitatakiwa kujisajili upya"

Mhe. Naibu Spika, hii mimi naona kama *contradiction* kwa sababu taasisi zilizosajiliwa kabla ya sheria hii zitachukuliwa kwamba zimesajiliwa kwa mujibu wa sheria hii. Lakini wakati huo kifungu kinasema tena kwamba baada ya mwaka mmoja sasa waende wakafanye usajili upya. Maanayake huu usajili ambao tayari umeshaambiwa ni kwa mujibu wa sheria hii sasa haufai tena.

Nilikuwa nahisi hichi kifungu kidogo kina lugha mbili zisizolingana. Maana kama imesajiliwa yaani taasisi iliyosajiliwa kabla ya sheria hii itachukuliwa kama imesajiliwa kwa mujibu wa sheria hii, maana hapo ilikuwa iwe inatosha. Lakini ukirudi ukisema ije isajiliwe tena baada ya mwaka mmoja maana yake kwamba usajili ule una dosari. Nilikuwa nahisi hichi kifungu bora kingerekebishwa kidogo kikatumia msimamo mmoja, kama imesajiliwa kihalali basi iwe imesajili kihalali, kama maana yake baada ya mwaka mmoja ije isajiliwe tena maana yake haikusajiliwa kihalali.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema kwamba mimi binafsi kwa kadiri nilivyousoma Mswada huu basi sikuuona na matatizo mengi isipokuwa hizo sehemu chache ambazo nilizo zizungumza. Mimi binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa jimbo la Chonga naunga mkono Mswada huu kwa asilimia mia moja, pamoja na kumuomba Mhe. Waziri afanye marekebisho yale madogo madogo niliyoyasema. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na mimi kwa kuweza kunipatia nafasi ya kutoa mchango wangu japo kidogo.

Mswada huu kwa upande wangu miye hautokuwa na mchango mkubwa sana kwa sababu mimi ni mmoja kati ya Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria, labda nitasema kwa ufupi tu au kueleza hali gani ya huu Mswada wenyewe.

Pamoja na kuwa sisi tunataka tuangalie vipengele vya sheria, vipengele vya sheria tumeviangalia na tumevitoa kwa kila mtu amepata marekebisho ya Mswada huu kila mtu anao. Kwa hivyo itakuwa hatuna haja ya kurejea tena mule kwa mule. Tumejitahidi sana na nafikiri marekebisho yamekuwa ni mazuri kabisa.

Mhe. Naibu Spika, Wizara hii kwanza nimpongeze Waziri ambaye anayehusika na masuala haya kwa kutuletea Mswada huu wa Sheria ambao ni mzuri sana na ni pahala pake kuletwa wakati kama huu. Kwa sababu kumeonekana kabla kwamba kulikuwa na mapungufu mengi sana. Inaonekana kwamba watendaji wamejitahidi kuutengeneza Mswada huu ukawa mzuri na sisi haukutupa shida kubwa kuuangalia Mswada huu. Ila tuliona kuna marekebisho madogo madogo ya kawaida na tukaweka kwani ni kitu cha lazima marekebisho kwenye Mswada wowote ule.

Mhe. Naibu Spika, suala zima linalozungumzwa hapa ni suala la biashara ya aina yoyote, zinahitaji kusajiliwa. Zamani ilikuwa watu kila mmoja anafanya anavyotaka, hakukuwa na utaratibu maalum au utaratibu mzuri wa kusajiliwa hawa wafanyabiashara. Kwa hivyo wizara imeona wakati umefika sasa hivi biashara zote ziweze kusajiliwa. Ndio maana Mswada huu wa Sheria ya Usajili wa Taasisi za Biashara ukapewa jina hilo. Sasa katika suala la biashara hapa tunasema kwamba tuna biashara namna kwa namna. Kuna mtu anaweza akafanya biashara ya binafsi yaani mtu binafsi ni mtu mmoja au anaweza kufanya biashara akawa na mwenzake hizo zote ni biashara tunaona. Watu kushirikiana mahala pamoja wakafungua biashara zao, lakini kati ya hao ikiwa ni mtu mmoja au ni watu wawili walioshirikiana ni lazima watu hao kwa pamoja wende wakasajiliwe kwa utaratibu wa sasa.

Mhe. Naibu Spika, ruhusa hiyo imetolewa kwa kila mtu mmoja mmoja au ubia wa watu wawili ambao wataungana pahala pamoja na wakakubali kutoa mali zao, wakakubali kutoa ujuzi wao, wakakubali kwamba faida watakayoipata watu wawili wale waweze kugawana au hasara yoyote watakayoipata watu wawili waweze kugawana. Hiyo ndiyo biashara maana unapofanya biashara inaweza kuwa biashara ile ikatia faida au ikatia hasara. Kwa hivyo lolote mtakalolipata katika ubia basi mkubaliane ama faida au hasara.

Sisi tunataka watu hawa, kwa sababu wamo ndani ya nchi wanafanya biashara na wao wanapata mapato basi na sisi tunasema angalau na wao wakajisajili baada ya kujisajili na wizara itakuwa inapata chochote, inapata mapato ndani yake. Kwa hivyo hapa mapato yatakuwa hayayumbi tena.

Vile vile tunaweza tukasajili makampuni, tunajua makampuni yapo, yanaingia Zanzibar siku hadi siku, kwa hivyo tuna wajibu makampuni haya kuyasajili, maana watu wanaweza wakajisajili huko huko kwao wanakotoka wameshajisajili, wanakuja hapa kama ni wafanyabiashara. Lakini sasa hivi kama itakuwa ni makampuni basi yajisajili hapa hapa Zanzibar na yale makhuli yaingie hapa hapa Zanzibar, kama si haya makampuni vile vile tunakuwa tunazo jumuia nazo vile vile zinahitaji kusajiliwa. Kwa hivyo jumuia zetu zote kwa hivi sasa wajue kwamba kila jumuia pahala ilipo wanahitaji kusajili biashara zao.

Mhe. Naibu Spika, zamani kulikuwa kuna Jumuia za Vyama vya Ushirika hivi navyo vile vile vinahitaji kusajiliwa na taasisi nyengine yoyote ambayokuwa inataka kusajili inaweza kujisajili. Pia tunaweza kusajili biashara ambazo zinafanyika katika viwanda au katika aina yoyote ya mashirika. Katika kusajili ni lazima uwepo na utaalamu ndani yake, wapatikane wataalamu wa kuendesha shughuli zao, kama ni viwanda wajisajili, mashirika na kadhalika.

Mhe. Naibu Spika, katika suala la biashara kuna mambo ambayo ni muhimu hapa tunasema kwamba tunakuwa na Mrajisi ambaye huyu atakuwa ni Mkurugenzi ambaye ndiye Mtendaji Mkuu, yeye ndiye atakayeshughulikia mambo haya yote. Huyu ndiye yeye atakayekuwa dhamana ya mali yote ya Zanzibar. Itakuwa kama kuna mashirika ataangalia aina ya mashirika yenyewe na aina ya usajili wa mashirika hayo. Kama kutakuwa na marekebisho ya hizi sheria zetu tunaweza pia tukazisajili. Tunayo haki ya kuzisajili sheria zetu wakati zikishakufanyiwa marekebisho kama hivi sasa inakuwa wakati tunaingia ndani humu tunakaa, tunapiga kelele, tunaamua sheria zetu ziwe hivi, hivi, basi zile sheria ambazo tunazifanyia marekebisho ni wajibu wetu kuzisajili, sheria ambazo ni mpya baada ya zile kongwe za zamani.

Mhe. Naibu Spika, kuna mtu ambaye tunamwita Wakala wa usajili wa biashara huyu pia atakuwepo na kutakuwa na kitu masjala ya taasisi za biashara. Masjala kila mtu anafahamu, sote tunafanya kazi mawizarani hata katika mawizara ya serikali masjala zipo, nani aliyekuwa hafahamu nini masjala. Kwa hivyo katika masuala haya ya biashara masjala itakuwepo na taasisi zote zitasajiliwa, patakuwa na masjala maalum ya kuweka kama ni kumbukumbu. Pia wakala wa usajili wa biashara atakuwepo na kuweka kumbukumbu zote.

Jambo la mwanzo ambalo ni la msingi katika masuala haya ya biashara katika kusajili ni lazima watu hawa tuwapokee na tuweze kuwawakea kumbukumbu zao. Kumbukumbu za mapokezi, unapo pokewa lazima uwekewe kumbukumbu zako. Huwezi kumpokea mtu katika biashara bila ya kumuwekea kumbukumbu zake. Mtu yeyote anayekuja na maombi yake, akishakupeleka maombi yake ni lazima awekewe kumbukumbu.

Vile vile kutakuwa na daftari la mapokezi, hili litakuwa ni daftari la kuweza kusajiliwa, kila mtu atasajiliwa katika daftari hilo. Kwa sababu wanataka wajulikane wafanyabiashara wote watakao kuja pale ni lazima daftari lile liwepo kila mtu liwe linaonekana kwamba huyu amekwisha kujisajili na kutakuwa na orodha ya usajili.

Mhe. Naibu Spika, kazi iliyopo kwa wananchi wetu wajue tu kwamba Mswada huu wa Sheria upo na tunawataka wafanya biashara wote baada ya Mswada huu kuwa tayari waende wakajisajili na watapokewa vizuri na watapeleka maombi ya kutaka kusajiliwa biashara zao, pamoja na majiya ya biashara zao. Hili ni jambo la msingi la kawaida wenyewe wafanyabiashara wanajua, sisi si wafanyabiashara lakini wao wanajua zile taratibu ni lazima ukitaka kuisajili biashara utoe na jina la biashara yako. Kwa hivyo kila mfanyabiashara ataweza kusajili vizuri. Jina lake litawekwa katika daftari la usajili na orodha zitakuwepo kikamilifu.

Katika kazi za masjala kuzisajili hizi taasisi zote na katika masjala hii mtu atahitaji kupewa nambari ya utambulisho. Mfano fulani bini fulani kaja, jina lake limeshaorodheshwa, limeshasajiliwa, atapewa nambari yake. Hili ni jambo la msingi kwamba kila mtu atapewa nambari ya utambulisho. Hizi zitawekwa katika kumbukumbu ni mambo ya kila siku haya. Maombi yao atakapopeleka *application* yake ya kutaka asajiliwe basi tabaan itabidi apewe na fomu za usajili ambazo hizo atakuwa nazo. Haya ni mambo muhimu ambayo yanahitaji kuzingatiwa vizuri. Tunawaarifu wananchi wote mtu mmoja mmoja, watu wanaotaka kushirikiana, Makampuni, Majumuia, NGOs, watu hawa wote wanatakiwa wasione tabu. Mambo haya tunataka tuyaweke mahali pamoja ili Wizara ijue wafanyabiashara wake na mapato yaweze kupatikana kwa wafanyabiashara wote, sio kama zamani ambayo mapato yalikuwa yanapotea potea.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa natoa mchango wangu kidogo tu kwa sababu huu Mswada tumeupitia na ilikuwa kubwa sisi ni kutoa baadhi ya mambo ambayo tuliyaona katika Mswada huu na kila mtu hapa anao, kwa hivyo sina haja ya kuendelea sana katika Mswada huu. Tunawakaribisha wale wengine ambao hawajapata nafasi ya kuchangia wauchangie.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru, ahsante.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, nataka nikushukuru na mimi kunipa nafasi hii nikazungumza machache kabisa ili niweze kupata uelewa mzuri na ufafanuzi katika Mswada huu wa Sheria hii ambao tunaamini serikali umeuleta kwa madhumuni makubwa hasa ya kuweza kuwafanya wafanyabiashara wetu wafanye kazi zao kisheria zaidi na ili kuondoa manung'uniko pale ambapo inapotokezea.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa naomba sana Wajumbe wa Kamati hii washereheshe kidogo mswada huu ili na Wajumbe wengine ambao hawakupata nafasi kwenye kamati na wao kupata nguvu ya kuweza kutoa yale maeneo ambayo yanahitaji ufafanuzi zaidi. Kwa sababu kama tunavyojua Mhe. Naibu Spika, tunatakiwa Wajumbe wa Kamati tumsaidie sana Mhe. Waziri katika kutoa maelezo ya ziada ili wakati wa kupitisha vifungu buti zisiwe nyingi au zisiwepo kabisa.

Kwa hivyo ninaamini Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hii wananisikia na ninaamini kuanzia hivi sasa watajiandaa kutoa mchango mkubwa sana ambao utaweza kusaidia wananchi wetu. Mhe. Naibu Spika, kwa nini nikasema hivyo. Nimeamua kusema hivyo kwa sababu kama nilivyoeleza nilivyochangia kama sikosei jana kwamba hivi sasa wananchi wetu wanahitaji kupata uelewa mkubwa sana wa hizi sheria ambazo tunazozipitisha, na kwa bahati nzuri hivi sasa tunashukuru kwamba redio, televisheni huwa zinarusha matangazo yetu moja kwa moja kutoka Baraza la Wawakilishi.

Sasa mara nyingi tunapopitisha vifungu sisi hii miswada na sheria tumezipitia tumepata kuona nini kilichomo, lakini wananchi wetu wapo kwa bahati mbaya wengi sana huwa hawapati nafasi ya kuipitia na kuisoma miswada hii wakajua ile sheria nzima hasa kifungu kwa kifungu kilikuwa kinasemaje, kina madhumuni gani na kwa nini sheria ile ikapitishwa. Kwa sababu sheria tunazozipitisha zaidi zinawalenga wananchi wa kawaida kwa ajili ya matumizi.

Sasa nilikuwa naomba Waheshimiwa tujitahidi sana hizi sheria tuzisome kifungu kwa kifungu ili wananchi wetu waweze kupata ufafanuzi kwa sababu, wakati mwengine wananchi wanavunja sheria bila ya kujijua na kwa sababu wanavunja sheria ile sheria yenyewe hawaijui. Kwa hivyo matokeo yake vyombo vya serikali vinawachukulia hatua pahala ambapo mwananchi ile sheria wala haijui. Kwa hivyo mimi nadhani ufafanuzi wetu utaweza kuwasaidia wananchi kuweza kupata kujua hizi sheria zikoje.

Sasa Mhe. Naibu Spika, baada ya dibaji hiyo, sasa hivi naomba moja kwa moja niende katika kuchangia huu Mswada wa Sheria ya Usajili ya Taasisi za Biashara na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Naibu Spika, mimi ninavyojua kipo kitengo pale Afisi ya Mrajisi kama sikosei ambacho kitengo kile kinasajili biashara, makampuni yanapoanzishwa, biashara nyengine mbali mbali zinapoanzishwa. Kitengo hiki naamini kinataka kuboreshwa zaidi, nadhani ni kitu kama hicho.

Sasa Mhe. Waziri nafikiri akija hapa atazidi kuja kunielimisha na atakaponielimisha mimi atakuwa amewaelimisha wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura lakini na Wazanzibari wote ambao sheria hii wao ndio wanaotakiwa kwenda kuitekeleza.

Mhe. Naibu Spika, hapa katika huu mswada nitaomba tu nikisome hiki kifungu cha kwanza na cha pili. Kifungu cha kwanza kinasema jina fupi. Sasa hili jina ndio linalotoa tafsiri ya mswada huu au sheria hii tunapoipitisha hapa.

Kifungu cha kwanza kinasema sheria hii itajulikana kama ni sheria ya usajili wa taasisi za biashara Zanzibar na itaanza kutumika tarehe ambayo Waziri ataitangaza katika gazeti rasmi la serikali. Sasa nilikuwa hapa nataka niulize jee, hii taasisi ndio ile ile inaboreshwa au kuna taasisi nyengine ambayo itayobeba kazi ya taasisi hii.

Lakini kifungu cha pili kinasema sheria hii itatumika sambamba na sheria zinazosimamia usajili wa uendeshaji wa taasisi zifuatazo, biashara binafsi ama biashara ya mtu mmoja mmoja au ubia, kampuni, Jumuiya, vyama vya ushirika na taasisi yoyote iliyoorodheshwa kwenye kanuni zilizotungwa chini ya sheria hii.

Sasa hapa nitataka nieleze kimoja baada ya kimoja katika hii (a), (b), (c), (d) na (e). Mhe. Naibu Spika, tunaposema biashara binafsi ama biashara ya mtu mmoja mmoja na huku chini kwa sababu imetolewa ufafanuzi kutakuwa na vile kuweka kumbukumbu za biashara na vitu vyengine. Sasa hapa mimi nilikuwa ninataka niulize kwa sababu hata sheria hii vile vile huku chini imeeleza kwamba wafanyabiashara watatakiwa wasajili katika hii taasisi husika, lakini sikuona ni muda gani ambao uliowekwa, maana yake leo tumepitisha sheria hapa, sio leo samahani kuna sheria itakuja lakini imeweka muda.

Maana yake unapotunga hii sheria kwamba biashara zinatakiwa zisajiliwe, kwa hivyo lazima patakuwa pana muda maalum na vile vile kwa mfano kama kuna kampuni au wafanyabiashara mmoja mmoja, yaani mfanyabiashara binafsi kama ilivyoelezwa katika kifungu hiki cha pili hii (a), jee kwa wale ambao watakaokuwa hawakwenda kusajili biashara zao, jee watakuwa ni wakosa na kama watakuwa ni wakosa hatua gani zitachukuliwa dhidi yao.

Kwa sababu hapa kama itakuwa kuwa anayetaka tu aende akajisajili basi tunajua taratibu za watu wetu huwa wakati mwengine wanaona usumbufu, na kwa sababu huku itatakiwa aweke kumbukumbu za mahesabu, pengine atatakiwa asijulikane kwamba biashara yake ameuza vipi na kumbukumbu zipo vipi.

Sasa hapa Mhe. Waziri aje atueleze jee, kutakuwa kuna ulazimu kwamba biashara yoyote, maana yake hapa imeelezwa hapa mpaka ya mtu binafsi pengine wauzwa vioski na kuna vioski sio vioski vidogo vidogo, kuna vioski vikubwa tu ambavyo vinafanya biashara kubwa pengine hata maduka mengine ambayo yana leseni kubwa ambazo wamepewa na serikali. Sasa hapa pia nilikuwa ninataka nije nipate ufafanuzi.

Lakini (b) Mhe. Naibu Spika, makampuni tunajua kampuni hapa tunajua kawaida kampuni inapoanzishwa lazima inakuwa inasajiliwa na inaposajiliwa inakuwa na *memorandum of standing*, lakini vile vile na pengine kuna sheria nyengine, lakini vile vile kuna wale wamiliki wa kampuni aidha kama mtu peke yake au na familia yake au na wengine.

Sasa hapa mimi kwanza nataka nipongeze kwa sababu sheria hii itaweza sasa kubana yale makampuni ambayo ni hewa. Kwa nini nikasema makampuni hewa. Kuna baadhi ya kampuni tumezishuhudia kwamba wamefika mpaka

kupewa baadhi ya kazi, lakini ukija ukiangalia makampuni yale hayakuanzishwa katika utaratibu uliokuwa mzuri au utaratibu wa kisheria. Unaweza ukakuta kampuni imesajili jina tu lakini huoni chengine chochote na wakati mwengine wanaweza wakapewa kazi pengine na taasisi za umma, kitu ambacho wakati mwengine kinakuwa ni kinyume na sheria.

Mfano Mhe. Naibu Spika, kuna baadhi sitaki kusema Zanzibar lakini kuna baadhi ya nchi hizi za Afrika ya Mashariki, kuna baadhi ya makampuni binafsi yameweza kupewa mpaka kazi za serikali. Hii ninatoa mfano wamepewa mpaka kazi za umma na kazi zile wakazifanya lakini kwa bahati mbaya kati kati ya kazi ile ikaja ikaharibika, aidha kuharibika kwenyewe haikumalizika kabisa au ule mradi umekamilika lakini matokezeo yake ukawa hauna kiwango kinachokubalika.

Sasa matokezeo yake mfano kama kampuni ya ujenzi, kama itakuwa wamepewa kazi na ikifika pahala kazi ile wamefanya haikumalizika na ujenzi ule ukawa umeharibika kabisa. Sasa kwa mfano kwa Zanzibar inatakiwa kampuni yoyote ya ujenzi lazima isajiliwe katika bodi ya Wakandarasi.

Sasa kuna baadhi ya makampuni, mfano kama haikusajiliwa kwenye Bodi za Wakandarasi, lakini ukakuta kampuni ile imeweza kupewa mpaka kazi ikafanya lakini kazi ile ikaharibika. Matokezeo yake unapokwenda kumpeleka Mahakamani kampuni kama ile, ina pale pesa za umma zinakuwa zimeshapotea.

Kwa sababu yule katika taratibu za kupewa kazi lazima athibitishwe kwamba amesajiliwa na Msajili wa Wakandarasi, lakini inapofika pahala kama hakusajiliwa katika Bodi ya Wakandarasi akipewa kazi huyu na akiiharibu basi huna jinsi ya kuweza kumshitaki.

Sasa nilikuwa ninajaribu kuuliza jee, msajili huyu kwa sababu kama ilivyosema kwamba sheria hii itatumika pamoja na sheria nyengine, jee mfano kama hawa Wakandarasi wao wameshasajiliwa na Bodi ya Wakandarasi, jee hii mamlaka ya huu wakala ambao atakayekuwa tunaitungia sheria hii na wale vile vile watatakiwa waje wasajili tena katika hii sheria mpya ambayo tumeitunga au katika zile Bodi au zile taasisi zilizosajili biashara zile itakuwa imetosha au vipi, hapa kidogo nilikuwa nataka maelezo, kwa sababu hofu yangu moja isiwe ikawa kwamba kama wafanyabiashara wetu wa Zanzibar wanavyolalamika kwamba leo anakwenda Manispaa anataka kodi, kesho anakwenda ZRB anataka kodi, keshokutwa anakwenda TRA anataka kodi.

Sasa wenyewe wanasema zile kodi kwa nini zisikunywe eneo moja ili mfanyabiashara anapokwenda kulipa kodi anajua akishalipa kodi inakuwa kodi zote amemaliza kuliko leo anakwenda huyu na kesho anakwenda. Sasa isije kuwa baadhi ya makampuni yamesajiliwa na vile vyombo ambavyo tayari tumevitungia sheria, halafu leo inapokuja hii anatakiwa na kule aende akasajiliwe tena, ikaja ikaonekana kama labda tunatunga sheria ambazo zinagongana.

Sasa hii ninadhani Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri akija akitutolea ufafanuzi atapata kututoa hofu na akinitoa hofu mimi kama nilivyosema atakuwa amewatoa hofu na wale wengine ambao wakisikia tunatunga hii sheria.

Lakini vile vile kwenye kifungu cha (c) cha pili kinasema jumuiya. Jumuiya tunachukuliwa mfano kama vikundi, kama hivi sasa tuna vikundi vingi vya akinamama, vyama vya ushirika na jumuiya nyengine mbali mbali ambazo zinajikusanya, hata hizi *NGO's* ambazo kuna baadhi ya nyengine kwamba wanafanya kazi ambazo zinaingiza na tija.

Sasa jee, hapa katika hawa waliojisajili kwa sababu unajua vikundi vya ushirika wao huwa wanasajiliwa na Idara ya Vyama vya Ushirika na pale kunakuwa kuna kumbukumbu zao nyingi na huwa wanatoa mafunzo. Sasa jee hizi kutakuwa na mahusiano gani au na mashirikiano gani na hizi taasisi nyengine. Hapa niliposema jumuiya kumbe na hapa chini kuna na vyama vya ushirika vile vile, sasa nadhani Mhe. Waziri akija akitusaidia ufafanuzi ataweza kuweka sawa na mambo mengine.

Lakini kifungu hiki cha pili kinasema bila ya kuathiri masharti ya kifungu cha kwanza cha kifungu hiki, sheria hii pia itatumika kwa mashirika ya serikali. Sasa mfano kama tuna mashirika yetu ya serikali, mfano *ZSTC*, Shirika la Bandari, sasa hawa jee mashirika ya serikali watatakiwa wajisajili upya kwa hii taasisi ambayo tunaiundia hii sheria hivi sasa. Kwa hivyo vile vile hapa nitakuja kuhitaji kupata maelezo.

Mhe. Naibu Spika, hapa kifungu cha tatu nilikuwa najaribu kuangalia katika maeneo yaliyoandikwa ufafanuzi, kuna taasisi za biashara imetolewa ufafanuzi wake, biashara binafsi imetolewa ufafanuzi wake lakini hapa katika rekodi za mapokezi, hapa inasema rekodi za mapokezi maana yake ni kumbukumbu za kila siku za mambo ya daftari la usajili.

Sasa hapa kidogo nilikuwa nataka ufafanuzi na ndio maana nikasema kuna biashara nyengine au kuna kampuni nyengine au kuna taasisi nyengine au kuna jumuiya nyengine, wanapofanya biashara zao huwa wanaweka kumbukumbu za mahesabu. Sasa kama ikiwa kwamba tukishapitisha sheria hii kwamba biashara zote zinatakiwa lazima zisajiliwe. Jee, kutakuwa kuna usimamizi wa kuhakikisha kwamba hawa wengine wanafunga mahesabu yao au vipi.

kwa sababu ndio pale niliposema kama itakuwa wengine wanaangaliwa rekodi za ma- *ledger* yao ya kumbukumbu za biashara na kama wengine watakuwa hawaangaliwi, sasa sijui kutakuwa kuna ulazimu gani kwa wale wengine kushajishika ili kwenda kusajili biashara zao.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea katika mswada huu hapa katika kifungu cha 6 (1), kinasema kila taasisi ya biashara inayotakiwa kuwasajiliwa chini ya sheria hii italazimika kuwasilisha maombi ya usajili kwa Mrajis ambaye ataingiza katika rekodi ya mapokezi, halafu kifungu (2) kinasema maombi ya usajili yataambatanishwa na fomu ya usajili zilizojazwa na kusainiwa vitambulisho kama vinavyoainishwa kwenye sheria husika zinasimamia taasisi zilitajwa kwenye kifungu cha pili cha sheria hii na (c) malipo ya ada zilizoainishwa katika mswada huu.

Sasa hii inajirejea kama ile ya mwanzo niliyoizungumza kwamba tayari hapa kuna biashara nyingi ambazo hazipo rasmi ambazo yaani hazijasajiliwa. Sasa jee hizi kwa muda gani ambao watalazimishwa na wao lazima wasajili ili kuhakikisha kwamba haya yaliyotajwa hapa yanaweza kutekelezeka kivitendo.

Lakini vile vile Mhe. Naibu Spika, kwamba kuna baadhi ya kampuni ambazo zilikuja kufanyakazi hapa Zanzibar na nitaomba nitoe mifano hiyo. Kuna baadhi ya makampuni ambayo yamepewa kazi ya kujenga minara hii ya simu na wao makampuni haya usajili ukiangalia au kampuni hizi hazipo hapa Zanzibar pengine zipo Tanzania Bara, kwa hivyo mtu akishapewa tenda ya kujenga minara ya yeye anapewa ramani tu kwamba minara hii itakuwa maeneo fulani, tuseme Morogoro, Tanga, Zanzibar na unaposema Zanzibar inakuwa Unguja au Pemba na sehemu nyengine.

Sasa matokezeo yake unawakuta mafundi wanakuja, yaani fundi kwa mara ya mwanzo ndio anaingia Zanzibar hata lile eneo anakuwa halijui lakini moja kwa moja anakwenda site kwenda kuanza kazi. Mambo haya kwa kweli yalituletea matatizo makubwa sana kipindi cha kati kati.

Kwa sababu wakati mwengine unaweza ukakuta eneo halijafanyiwa tathmini za sheria na taasisi zinazohusika, mfano Halmashauri au Mabaraza ya Miji au taasisi nyengine zinazohusika na maeneo. Unaweza ukakuta kwamba kuna baadhi ya maeneo kuna nyumba za watu, unajua kutokana na ukwasi wakati mwengine mtu nyumba yake anaikodisha nusu au anaiuza nusu kwa sababu ukishajenga mnara huwezi kusema labda umekodisha kwa sababu mnara ule utakuwa ni *forever*.

Kwa hivyo utakuta mtu mbele nyumba anakaa lakini nyuma kakodisha pengine kampuni kwa ajili ya mnara. Sasa matokezea yake unapokuja kufuatilia unamuuliza jee vibali vipo wapi, yeye hata vibali havijui vinapatikana wapi. Kwa hivyo matokezeo yake unakuta kwamba kuna minara imejengwa kiholela ukiangalia hakuna kibali pengine cha Halmashauri, inawezekana Shehe, kwa kuwa ngoma ipo katika eneo lake anaweza akachangamka barua ya Sheha ikawepo lakini hakuna vielelezo vyengine vyovyote vilivyokuwepo katika Halmashauri au katika Manispaa.

Matokezeo yake ujenzi ule unakuwa unaendelea kiholela. Sasa yule anayehuka unapomwambia kufuatilia vibali haijui taasisi hata taasisi moja. Sasa hili kwanza ni tatizo kwa sababu kwanza kwa utaratibu wetu kampuni yoyote itakayokuja kufanya kazi Zanzibar na sio Zanzibar peke yake na hata Tanzania Bara, kampuni yoyote ya kigeni itakapokwenda kufanya kazi ni lazima kwanza iwe *registered*, samahani juzi nimeona kipindi cha Baraza la Wawakilishi tukatakiwa tusitohowe maneno ya watu, kwa hivyo tunasema kampuni yoyote ambayo inayokwenda kufanya kazi katika nchi yoyote lazima isajiliwe kwanza pale iwe na kazi yake ya muda na halafu ndio iweze kufanya kazi ili taasisi za serikali zilizokuwepo pale na hata wananchi watakapokuwa na tatizo lolote na kampuni ile, basi lazima wajue wapi pa kwenda kuweza kufuatilia masuala haya.

Sasa hii ndio maana nikasema nijaribu kulitolea ufafanuzi kwa sababu ilileta sitofahamu katika baadhi ya mitaa kwa sababu kuna baadhi ya minara imejengwa chini ya uwa za watu za nyumba inakuwa inaleta tafrani wakati mwengine na wananchi wakati mwengine walijenga hofu labda kutokana na miozi ile ya minara. Kwa sababu kulikuwa hakuna ile taaluma iliyotolewa kwa wananchi.

Sasa mimi ninadhani kupitia sheria hii, hawa tutakaowapa mamlaka ya usajili hizi biashara na makampuni basi wahakikishe kwamba wanafuatilia mpaka na zile kampuni ambazo zinazokuja kufanya kazi kuhakikisha na wao wanasajili ili kupata taratibu za kisheria.

Lakini jengine Mhe. Naibu Spika, nimejaribu kuangalia kifungu cha 7 cha mswada kinasema wajibu wa taasisi ya biashara. Kifungu cha 7(1) kinasemaje, "Muombaji atawajibika kutoa taarifa kamili na sahihi katika fomu za usajili wa viambatanisho atakavyoviwasilisha na atalazimika kuthibitisha ukweli wa taarifa hizi.

Kifungu cha 7 (2) kinasema, "Taasisi itawajibika kusajili marekebisho au mabadiliko ya taarifa au taasisi za biashara iliyosajiliwa", na (a) inasema kwamba "Iwapo wakati wowote mabadiliko yatakapotokea au yatakapofanywa katika taarifa za taasisi za biashara iliyosajiliwa ndani ya siku 28 au muda usiozidi siku hizo, taasisi italazimika kumuarifu Mrajis kwa maandishi juu ya mabadiliko hayo kwa kutumia fomu maalum zitakazoeleza aina ya tarehe ya mabadiliko ikilazimu ithibitishwe katika namna kama itakavyotakiwa wakati wa usajili.

Sasa hapa kifungu kihi Mhe. Naibu Spika, nilikuwa ninataka kuzungumzia zaidi katika maeneo ya uwekezaji. Mhe. Naibu Spika, ndio nikasema kwamba sheria hii tunayoipitisha imekuwa kama ile sheria tuliyoipitisha wakati wa asubuhi, Sheria ya Afya na Uhifadhi wa Mazingira kwa sababu ndani ya sheria ile katika utekelezaji wake kuna taasisi nyengine ambazo tayari kuna baadhi ya sheria zipo zinasimamiwa na taasisi nyengine.

Ukiangalia kifungu kile cha 7 ufafanuzi wake kwa nilivyofahamu, mfano kama maeneo ya uwekezaji hasa mahoteli hapa Zanzibar kumekuwa na utamaduni, wawekezaji wengi katika sekta ya utalii hasa mahoteli, hatujui kwamba labda ndio mbinu za kibiashara au ni sehemu ya uendeshaji wa biashara au wakati mwengine hofu inayotutaza ni hofu ya kukwepa kodi katika suala zima la kulipa kodi serikalini.

Kumekuwa kuna baadhi ya mahoteli, mwanzo utakuta katika maombi ya ujenzi wa taasisi hizi unaweza ukakuta jina jengine, lakini baada ya miaka miwili au mitatu management inabadilika na *management* inapobadilika, sio kwamba ya hoteli ile ile lakini mpaka jina la hoteli linakuwa linabadilika.

Ukiangalia historia ya mahoteli mengi hapa Zanzibar, mengi hasa yale majina ambayo mwanzo yaliomba ule ujenzi basi unaweza ukakuta yameshabadilishwa majina zaidi ya mara mbili, mara tatu wakati mwengine mpaka mara nne. Lakini haya tunajua ni miongoni mwa mbinu za wafanyabiashara pengine labda katokea mtu ambaye anataka kuinunua ile biashara au anataka kuiendeleza zaidi katika ufanisi au wakati mwengine hata kuingia ubia. Sasa hapa matokezeo yake utakuta kampuni inakuwa inabadilisha jina mara kwa mara.

Sasa jee, katika haya maeneo ya uwekezaji na hii taasisi ambayo tunaiundia hii sheria na kwa sababu katika maeneo ya uwekezaji tunajua kule kuna vibali vya *ZIPA* ambao wao ndio wanatoa vibali kwa ajili ya uwekezaji lakini vile vile kuna na taasisi nyengine, ukiangalia hata Wizara ya Hahari huwa inatoa baadhi ruhusa kwa ajili ya haya mahoteli mengine.

Sasa nilikuwa ninataka niulize jee, katika haya mfano mahoteli yanayobadilisha majina au kubadilisha uongozi kila baada ya muda, jee hii sheria tunayoitunga itaweza ku-*apply* katika kuingilia katika mamlaka zile. Sasa hili vile vile nitataka kupata ufafanuzi.

Ikiwa sheria hii itakuwa inahusika mpaka na yale mahoteli kama ninayosema yanayobadilisha uongozi mara kwa mara basi itaweza kutusaidia kuweza kupunguza ule utamaduni au lile wimbi linapofika pahala kwamba anatakiwa pengine *tax holiday* kwenye mahoteli ina miaka mitano, ikishaona miaka mitano inakaribia kumaliza anaweza akabadilisha jina au akamuulizia mtu mwengine, kwa hivyo yule mtu mwengine anapokuja kuanzisha ile biashara kwa kuwa yeye anakuwa ni mpya na yeye ana-*enjoy tax holiday* wakati hapo serikali inakuwa inakosa mapato yake.

Lakini vile vile Mhe. Naibu Spika, katika eneo hili pia tuligundua kuna baadhi ya matatizo ambayo yaliwahi kutokezea kwa baadhi ya wawekezaji ambao walishirikiana na wazalendo. Mhe. Naibu Spika, tuna kumbukumbu

kwamba kuna baadhi ya kesi ziliwahi kwenda mpaka Mahakamani miaka mingi tu, kwenye miaka ya tisini, tisini na tano mpaka kwenye miaka ya elfu mbili, hatujui kesi zile zimemalizia vipi.

Kuna wengine unaweza ukamkuta mtu amekuja mwekezaji au amekuja pengine mgeni akaowa au akaolewa na mzalendo, katika makubaliano mema wakaendesha biashara na wameendesha biashara ile pengine kwa ubia na pengine katika lile eneo walilofanyia biashara walichukuliana ile kimazoea zoea, pengine hatimiliki ya eneo ya yule mume lakini mjenzi aliyekuja kuendeleza ule ujenzi pengine ni mke ambaye pengine ni raia wa kigeni, matokezeo yake wanakwenda inapofika pahala wanapokuja kufarikiana matokezeo yake mmoja anakimbilia Mahakamani na anapokwenda Mahakamani kunakuwa kunazuka mgogoro mkubwa, na hii inatokana na nini.

Sasa kwamba lile eneo lilikuwa la mmiliki fulani lakini akaingia na *partner* wake akishirikiana lakini waliamua wao wenyewe wenyewe tu bila ya kwenda kubadilisha pengine ule umiliki au uendeshaji, lakini vile vile hata kumbukumbu za mapato ambayo wanayoyapata na vile vile mgawanyo wake ukawa haujulikani.

Sasa mpaka mambo yanapoharibika ndio wanakimbilia Mahakamani lakini sasa ukija, na wanapokwenda Mahakamani chombo hiki ambacho kinachosajili na ndio hiki tunachotungia sheria kukipa mamlaka, watakuja kufika pahala watakuwa mara nyingi wanakwenda kukaa ushahidi Mahakamani. Kwa sababu mfano biashara ilianzishwa pengine na watu wawili na wakaingia ubia, kwa sababu siku hizi kuna utaratibu wa kuuza hisa, wanaweza wakauza hisa kwa taasisi nyengine, ina maana ile sheria ikawa na mabadiliko mpaka mgawanyo wa mapato na faida ukabadilika, mpaka na umiliki wa mali ukawa umebadilika. Kwa hivyo, kama wanakuwa wamefanya wenyewe kienyeji hawakupitia katika taasisi hii wakaelezea kila mabadiliko yanapotokezea. Matokezeo yake siku ambayo inapofika anaamua mwengine haridhiki pengine na mwenendo wa biashara na akijakwenda mahakamani, matokeo yake taasisi yetu hii itakuja kuwa shahidi mkubwa wa kwenda mahakamani kuweza kutoa uthibitisho.

Kwa hivyo, taasisi hii ikiwa itasimamia kazi zake vizuri kwa mujibu wa hii sheria ilivyoandikwa, basi hata katika zile mahakama ambazo pia tumeunda mahakama zile za biashara kwa kesi kama hizi za bishara, mara nyingi zinakwenda katika ile *arbitration.* Kuna sheria tulitunga hapa, wanakwenda kule wanajadiliana na kukubaliana. Kwa hivyo, nafikiri taasisi hii ikifanya kazi zake vizuri hata ile mahakama ya *arbitration* itakuwa haina kazi kubwa sana ya kuweza kuhukumu kesi za migogoro ya biashara ambayo inaweza kutokezea.

Sasa nadhani Mhe. Waziri ukija kunitolea ufafanuzi kwa baadhi ya hizi hoja zangu ambazo nimejaribu kuzielezea, nadhani nitaweza kuridhika. Kimsingi sijaona umuhimu wowote wa kutaka kuzuia labda sheria hii, kwa sababu hii sheria tunaamini kuwa imetungwa kwa ajili ya kuja kuweka mambo mengi ambayo yalikuwa hayaendi vizuri. Vile vile na wananchi wetu wataweza kujua hasa hii sheria ilikusudia kitu gani.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache, nimejitahidi sana kuchangia ili kuweza kupata ufafanuzi. Naomba niunge mkono hoja, ninaamini jawabu za Mhe. Waziri zitaweza kutusaidia kuweka sheria hii vizuri. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja kwa asilimia mia juu ya mia. Ahsante. *(Makofi).*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Naibu Spika, awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu *Azza Wajalla*, kwa kutujaalia kuwa hai na wazima na kuendelea na shughuli za Baraza hili tukufu la wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, nikushukuru na wewe kwa kunipa fursa na mimi kusema machache sana kuhusiana na mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, katika mambo ambayo yana kumbukumbu katika utungaji wa sheria kwenye Jamhuri ya Muungano, moja wapo ni katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977, ilipitishwa masaa mawili tu baada ya kujadiliwa katika bunge, katiba ya nchi nzima. Sasa Mhe. Naibu Spika, ikiwa katiba ya nchi nzima ilichukua masaa mawili tu na leo tuko hapa usishangae kwamba mswada huu leo hauna wachangiaji.

Mhe. Naibu Spika, kuna wakati mmoja nilipokwenda kutembea Pemba nilipewa hadithi moja, nikaambiwa ilipokuja MV. Mapinduzi wakati wa awamu ya pili ya Sheikh Aboud Jumbe, alitoka mshairi mmoja akaenda kuikagua ile kuanzia juu mpaka chini. Alipomaliza kuzunguka akatoka akaja na shairi, akasema MV Mapinduzi sijui niseme nini, kwa ule uzuri aliouona.

Sasa Mhe. Naibu Spika, ndio mswada huu leo wa Waziri wa Katiba na Sheria, Sayyidna Abubakar Khamis, na leo wale Masheikh siwaoni kule juu tukasema labda kuwepo kwao ndio kumetufanya hatuna la kusema. Lakini Mhe. Naibu Spika, kusudio langu ni kwamba mswada huu umeandikika vizuri na zaidi ni mswada wa kitaalamu.

Mhe. Naibu Spika, nasema haya kwa sababu mara nyengine tujifunze kwamba hakuna ulazima katika kutunga sheria, kuwa ni lazima kijadiliwe kitu ambacho hakiko cha kukijadili. Ni utaratibu sio kuwa tutakuwa tunafanya kihoja. Hata katika mabunge yaliyoendelea kabisa duniani Mhe. Naibu Spika. Kuna sheria zinakwenda baada ya nusu saa zinapitishwa kwa sababu zinakuwa zimekamilika na mambo yake yamekaa vizuri. Ndivyo ulivyo mswada huu Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, naamini hata ule mswada mwengine ulioambatana na huu wa Wakala sasa wa usajili, ukija yatakuwa ni haya haya kwa sababu kwa jumla mambo yake yamekaa vizuri.

Mhe. Naibu Spika, mimi binafsi nataka kusema sina lolote kwa maana ya vifungu vilivyomo katika mswada huu, labda katika kusaidia kupata uelewa mpana zaidi kama alivyoomba Mhe. Mwakilishi makini na mahiri wa wananchi wa Jimbo la Kwamtipura, Mhe. Hamza Hassan Juma, mwenye msimamo usioyumba, Mzanzibari mwana kindakindaki. Alisema Wajumbe wa Kamati tusaidie ili watu wapate uelewa mpana.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa naomba Mhe. Waziri akija atusaidie mambo machache nje ya mswada. Kwanza nilichokiona mimi katika madhumuni na sababu ambayo inapatikana kwenye ule mswada wa pili. Moja katika sababu za kuletwa kwa mswada huu ni kwa sasabu huku kukua kwa teknolojia katika dunia yetu. Kwa hivyo, ni utaratibu wa kawaida kabisa duniani katika kupunguza usumbufu na urasimu kwamba unaweza pia kufanya usajili kwa njia za *electronic* kama ninavyosema. Sasa mswada huu umelenga hivyo. Nilikuwa namuomba tu Mhe. Waziri akija atusaidie, kwamba mbali ya kuleta mswada huu na Baraza hili kufanya kazi hii, sijui ni kiasi gani wizara kwa kupitia nadhani atakuwa ni Mrajisi Mkuu wa Serikali wamejipanga kiasi gani katika kuhakikisha kwamba watu wameandaliwa na vifaa vimeandaliwa na utaalamu wake wenyewe wa kufanya kazi hii.

Vile vile na watumiaji wenyewe wa hizo huduma zetu Mhe. Naibu Spika, kwa sababu Mji Mkongwe ni kitovu cha biashara, rafiki zetu wengi kule wanajishughulisha na shughuli hizi. Lakini mimi mara nyingi huwa ninawaambia kwamba moja katika tatizo letu kubwa sana la wafanyabiashara tuliokuwa nao, ni kwamba namna wanavyofanya biashara imekuwa ni miaka nenda miaka rudi ni ile ile, yaani ni watu wa kwenda kununua na kuuza. Ni wachache sana kati ya wafanyabiashara wetu walioamua kuingia katika biashara kwa upana zaidi na kutoka pale ambapo wamekuwepo pa kwenda kuchukua mali na kuleta.

Kwa hivyo, katika njia moja ya kusaidia kuingia katika bahari nyengine, kwa maana ya kufanya biashara nyengine kuingia katika masuala ya kimataifa na kampuni nyengine ni pamoja na kwamba uwe na huduma kama vile mswada huu umezilenga. Yaani kwamba kuna daftari ambalo lina kumbukumbu za biashara zinaweza kupatikana kwa njia hizi za *electronic*, na inakuwa ni rahisi kwa mtu yeyote anayetaka kuingia katika biashara na kampuni nyengine basi aweze kwa huko huko aliko duniani kwa kutumia mtandao, aweze kupata taarifa hizi ili kuthibitisha usahihi wake, uhalisia wake na uhalali wake uweze kupatikana.

Sasa sijui wizara imejipanga kwa kiasi gani katika kuwasaidia wafanyabiashara wetu ambao ndio waliolengwa zaidi katika suala hili kuweza kujibadilisha kutoka katika zile biashara walizokuwa wakizifanya mwanzo hadi kuja katika mfumo mpya wa kufanya biashara.

Pili, nipongeze Mhe. Naibu Spika, kwamba katika mswada huu, nadhani kama sikosei katika kifungu cha 5. Katika masuala yanayozungumzwa vile vile kwamba moja katika kazi yake itakuwa ni 5(b) kutoa nambari za utambulisho wa kipekee wa taasisi za biashara. Ukiisoma katika Kiingereza ile inataja kuwepo kwa kodi maalum Mhe. Naibu Spika, ambayo kila biashara itapewa. Sasa nilikuwa naomba suala hili Mhe. Waziri akija atusaidie kwamba ni kwa kiasi gani litasaidia kurahisisha biashara kwa wewe mwenye biashara katika kupewa kodi ya namna hii. Tunajua kwa mfano unapopewa kodi kwa maana ya ulipaji kodi. Kwa mfano *tin number* inasaidia kwamba unapokwenda kulipa kodi unapunguza urasimu, mtu akitaka kumbukumbu zako pale pale zinapatikana. Je katika ile biashara mbali ya ile kwamba kumbukumbu zako ziko pale zinapatikana katika ile masjala, lakini katika kurahisisha ufanyaji wa biashara ni kiasi gani hili litasaidia, kwa sababu ni kitu kipya ambacho tunakianzisha hapa kwetu. Nilikuwa naomba hilo nisaidiwe.

Jengine Mhe. Naibu Spika, nilikuwa naomba vile vile ufafanuzi kwa suali kama ambalo kaliuliza Mhe. Hamza Hassan Juma, liko katika kifungu cha 24(1). Katika kifungu hiki Mhe. Naibu Spika, kinasema kwamba;

Kifungu cha 24(1)

> "Kila taasisi ya biashara iliyosajiliwa kabla ya sheria hii kuanza itachukuliwa kuwa imesajiliwa chini ya sheria hii na ndani ya kipindi cha mwaka mmoja baada ya sheria kutumika, basi taasisi hizo zitatakiwa kusajiliwa upya kwa mujibu wa masharti ya sheria hii".

Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa naomba hapa kusaidiwa kwamba moja ni imani yangu kwamba mswada huu utayaweka masuala yote ya usajili chini ya wakala mmoja, kwa hivyo kupunguza ule urasimu ambao uko sasa hivi. Swali langu ni kwamba je, katika huku kuchukuliwa kuwa limesajiliwa chini ya sheria hii, hawatatakiwa tena kulipa ada nyengine za usajili.

Lakini mimi nilikuwa nataka kuuliza Mhe. Naibu Spika, kwamba kwa kuletwa mswada huu, hatuwaongezei wafanyabiashara wetu, kwa sababu moja katika malalamiko makubwa kwa wafanyabiashara wetu ni kwamba kumekuwa na utitiri wa malipo ya ada na leseni za aina nyingi.

Mhe. Naibu Spika, hata katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, tulikuwa tumepewa mwaka huu, moja katika sehemu za utangulizi pale lilikuwa limetajwa suala hili, kwamba moja katika mazingira yanayopelekea ugumu wa kufanyika biashara kwetu ni kuwa na utitiri wa malipo ya leseni na ada mbali mbali ambazo wafanyabiashara wanatakiwa kulipa. Sasa nilikuwa nauliza je, mbali ya ku-*synchronize* kwa maana ya kwamba unaondosha ule utitiri wa wasajili. Je, itapunguza vile vile huu utitiri wa leseni, tozo na ada mbali mbali wanazotakiwa wafanyabiashara wetu kuzilipa na hasa katika kipindi hichi ambacho kifungu cha 24 kinakusudia kusema kwamba wale ambao wameshasajiliwa wanachukuliwa kwamba watakuwa wamesajiliwa chini ya sheria hii. Lakini na hapo tutakapoingia baada ya mwaka mmoja, je itasaidia kuondosha hilo ama tunaongeza aina nyengine tena ya leseni, tozo au ada kwa wafanyabiashara wetu ambao tayari tunawakamua sana. Hilo nilikuwa naomba akija Mhe. Waziri anisaidie.

La mwisho kabisa Mhe. Naibu Spika. Ninazungumza mara nyingi humu ndani ya Baraza kwamba nchi yetu ilijumuishwa katika jumla ya nchi ambazo zinafanyiwa utafiti kupitia benki ya dunia. Bila shaka ikishirikiana na serikali yetu juu ya urahisi ama ugumu wa kufanya biashara katika nchi husika. Kuna ripoti Mhe. Naibu Spika, huwa zinaitwa *doing business in the world.* Sasa kuanzia mwaka 2010 kumeanzishwa *doing business in Zanzibar, report* imetoka 2010.

Mhe. Naibu Spika, katika *report* ile niliwahi kusema humu ndani kwamba serikali ilibeba kigezo kimoja tu ikaja ikajisifia humu ndani kwamba mazingira ya wafanyabiashara wa Zanzibar ni mazuri. Lakini kuna vipengele vyengine tisa au zaidi ambavyo ukivitizama Zanzibar tuliokuwa tuna alama au maksi za chini kabisa na ilikuwa inapelekea kwamba *report* ile inaposomwa na mtu ambaye anataka kuja kuwekeza Zanzibar, basi hashawishiki kuna ugumu wa kuja kufanya biashara Zanzibar, ukiondoa kipengele kimoja ambacho kilitajwa. Moja wapo iliyotajwa mule ni suala zima la urasimu uliokuwa unahusishwa katika usajili wa biashara Zanzibar, kwamba moja katika kigezo Mhe. Naibu Spika, katika nchi za wenzetu cha kuvutia mwekezaji kuja katika nchi. Kila nchi Mhe. Naibu Spika, huwa inafanya bidii kuvutia wenye fedha zao kuleta mitaji katika nchi husika ili kuja kufungua biashara, kuongeza mapato serikalini, na kutoa nafasi za ajira kwa wananchi wa nchi husika.

Mhe. Naibu Spika, moja katika kigezo kinachotumika ni kwamba muda gani unatumika katika kusajili biashara yako. Kuna nchi unaweza ndani ya masaa 24 ukamaliza utaratibu mzima wa kuisajili biashara yako, kwa maana ya kupata leseni na kila kitu. Kuna nchi nyengine ni kwa siku tatu na kuna nchi nyengine ni kwa siku saba. Kuna nchi Mhe. Naibu Spika, ndio kama hii yetu sisi ule utaratibu wa kupandishwa ngazi ukishuka unaingia katika kumbukumbu kwamba unaweza ukafika pengine wewe siku 60 bado hujapata leseni na katika ile *report* ya *doing business in Zanzibar 2010* yametajwa Mhe. Naibu Spika.

Kwa hivyo, nampongeza sana Mhe. Abubakar Khamis Bakary kwa sababu hii ni sheria ya pili na inayokuja ya Wakala itakuwa ni ya tatu ambazo zinajitahidi kuweka mazingira mazuri ya kufanya biashara. Kwanza alituletea sheria mwaka jana kama sikosei, iliyokuwa inaruhusu mali zinazohamishika kutumika kuwekea kama msingi wa usalama katika kupata mikopo, ilikuwa ni sheria nzuri na mara hii zinakuja hizi mbili. Kwa hivyo, ndio nasema

mbali ya hizi, ni kiasi gani wizara yake ina mradi wa BEST unaotegemewa pia kusaidia Zanzibar ni kiasi gani inaweza ikaweka mazingira mazuri zaidi ya kufanya biashara.

Mhe. Naibu Spika, sijui ni kwa kiasi gani wizara katika hili imejipanga kuona kwamba yale maeneo mengine ambayo yamelalamikiwa katika *report* ya *doing business in Zanzibar, report* ya 2010 yanafanyiwa kazi nayo ili Zanzibar, kwa sababu uchumi wake tumesema mara nyingi sio uchumi unaotegemea rasilimali, ni uchumi wa kisiwa unaotegemea utoaji wa huduma. Ni *service oriented economy,* sio *resource based economy.* Ni kwa kiasi gani tunajenga mazingira mazuri zaidi ya kufanyika biashara kuvutia wawekezaji ili hatimaye tuweze kuwavuta wawekezaji kwa wingi kuja katika nchi yetu Mhe. Naibu Spika, kuongeza mapato katika nchi yetu kwa kupitia kodi, lakini vile vile kutoa ajira kwa wananchi wetu.

Nilikuwa naomba maelezo hayo Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kama nilivyosema mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria na Utawala. Kwa hivyo, mswada huu katika hotuba iliyosomwa kwa niaba ya Kamati tulishauunga mkono, lakini nasema tena kwa na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mji Mkongwe walionichangua kihalali bila vurugu au fujo kuingia katika Baraza hili, basi naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia mswada huu wa sheria kuhusu biashara. Kwa kweli sehemu zote zinatakiwa kusajili shughuli zao za siku zinapoanza kufanyika kuanzia asubuhi, hadi muda wote wa kazi jioni, ili kuhakikisha kwamba kwa siku sehemu zile zinasajili watu wangapi na wangapi ambao wana uwezo wa kufanya shughuli kwa kutwa nzima, ama kujua ni wangapi wamefika katika sehemu zao za kazi kwa wakati, ama kujua shughuli zao zinakwenda vipi kwa siku na mapato yanaingia kwa kiasi gani au yanamalizika kwa kiasi gani. Kama ni kupasi au ni kufeli.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli hii inasaidia sana sehemu zetu kuwa na usajili wa uhakika, hasa kwenye mawizara yetu ambayo ndio tunayotegemea kujua kwa siku kunaingizwa nini, ama kwa siku kunapungua nini. Hii inasaidia sana kwa wafanyabiashara hata wale wadogo wadogo na watu binafsi. Biashara yoyote ni lazima kusajili hata kama unauza samaki ni lazima ujihakikishe kwamba kwa siku unauza samaki wangapi ama umeshirikiana na wenzako ambao mmeweka umoja wenu wa kuweza kujisajili mujue watu wangapi ambao siku ile mmeuza samaki na kipato chenu kinahakikisha kwamba kinatosholeza kumiliki hali ya maisha ya ushirika ule ambao mmeusajili.

Mhe. Naibu Spika, kusajili kunasaidia sana hasa kwa ndugu zetu ambao ni madereva hasa wa daladala, kujua kwa siku tuna gari ngapi ambazo zinatembea katika mji wetu, ambazo zinatembea kwa uhakika na ambapo gari zile ni nzima zimesajiliwa na zina hakika kwamba zinatembea bila ya matatizo. Hiyo inasaidia sana kwa upande wa umiliki wa hali ya usalama wa wananchi wetu, pamoja na madereva wetu kuwa na uhakika wa kufanya kazi zao na wanajulikana kwamba leo ni madereva wangapi wameweza kufanyakazi katika nchi yetu na ambao wamesaidia kusafirisha wananchi kwa usalama na kufika katika shughuli zao za kazi kwa wakati.

Mhe. Naibu Spika, kusajili ni kitu muhimu sana hasa katika usafiri wa aina zote kusajiliwa na hasa kwenye meli zetu zinapokwenda safari hasa za Pemba na Dar es Salaam. Hizo zinasaidia sana kujua kwa siku Zanzibar zimeweza kutembea meli ngapi na kufika katika sehemu ya bandari ya Dar es Salaam. Je, zimefika salama ama vipi. Kwa vile tumeshapata kuumwa na nyoka hilo ni suala zuri sana la kuhakikisha katika meli zile zinaingia abiria wangapi, sio kwamba meli zinakwenda tu bila ya kujua ni watu wangapi hasa wapo katika meli wakati wa safari. Hii inasaidia sana kuhakikisha sheria yetu imepitisha vizuri kwamba chombo kinachoondoka katika bandari kuelekea katika bandari nyengine, kuhakikisha watu wote waliomo mule ndani ya meli wamesajiliwa vizuri. Kusajili ni kitu cha maana kwamba wewe mwenyewe ukiona kwamba umeingia katika meli au umerukia au umepata rafiki amekuingiza mule kwamba umeshindwa kulipia, sio ufundi mzuri kwa sababu hukujisajili, utakosa haki yako inapotokea tukio lolote.

Mhe. Naibu Spika, hii inatusaidia sana kukumbusha ingawa ni kidonda kwamba chombo kinapopata ajali au meli kuna haki fulani wewe mwananchi ambaye umejisajili unayoipata. Tumeona katika matukio ya mara hii, watu wote ambao wamesajiliwa katika vyombo ni wale ambao wamelipwa haki zao, ingawa wamefariki lakini familia zao wamepata haki zao kwa vile wamesajiliwa. Kwa wale wote ambao hawakusajiliwa mule naona haki zao zimepotea ndio utaona mizozo mpaka sasa hivi serikali inapata majukumu mengi sana, kwamba watu wanakwenda kudai kuwa mtu wangu au jamaa yangu kasafiri, lakini katika orodha ya kujisajili hatukumuona. Kwa hivyo, sio rahisi mtu yule kukubaliwa kupata haki yake.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, hii kusajili inasaidia kwa hata mtu mmoja mmoja, sio kwenye kampuni tu au katika shirika au serikali kuwa inaorodhesha watu wake kila siku ambao katika shirika hili lina watu wangapi. Lakini hata mtu binafsi ni vizuri sana unapojisajili utakuwa unapata haki zako tena zinafika kwa wakati.

Kuhusu matengenezo mengine ambayo yanatengenezwa katika mambo ya usajili, ni yale ambayo yanaambatana na mambo ya biashara ndogo ndogo. Biashara zetu ndogo ndogo za kuuza hata *fruit* ni wazi kwamba tuzisajili, kwa sababu yanapotokea maradhi kama umeuza *fruit* za mapapai ya kuponda katika gilasi, basi tunaweza kujua ni watu wangapi ambao wamesababisha kutoa maradhi, ambapo watu wale ipo nafasi nzuri ya kuweza kuwatafuta na kujua kwamba leo maeneo ya Darajani palikuwa na watu 10 walikuwa wanafanya biashara ya kuuza *fruit* ya mapapai, au kujua ni watu wangapi walikuwa wanauza maziwa ya kuganda na watu wamekunywa kisha wakapata matatizo ya matumbo, basi kama wamejisajili ni rahisi kwenda kuwachukua watu wale na kwenda kuwapimisha hospitali kwamba je, wale wahusika walikuwa na uwezo wa kuuza yale maziwa, ni vizuri sana tutawafikisha katika sehemu, sio kuwalazimisha kuwa tunawashtaki, lakini ni kwa uhakika kwamba watu wale wanahitaji kupewa nyenzo kwamba walikuwa wamejisajili. Lakini kwa mtu ambaye hakujisajili ni vigumu sana kwenda kumpeleka kunakohusika kuweza kupata matibabu ili biashara yake iendelee na atakosa haki zake, kumbe vile alikuwa na uwezo wa kupata haki ya kuweza kufanyiwa matibabu ya kushajihishwa kwamba anafaa kufanya biashara pale sokoni.

Mhe. Naibu Spika, hiyo kwa kweli inasaidia sana kwamba watu wetu sasa wahakikishe kuwa usajili wa jambo lolote ni muhimu. Hata wale wapanda baiskeli wa hapa mjini. Asubuhi akiamka tu kama akitaka utaratibu mzuri, siku hizi watu wanagongwa sana na magari. Kwa hivyo, ipo haja ya kufika katika kituo cha polisi kujisajili kwamba mimi leo naandika nitapanda baiskeli yangu kwa muda mrefu. Kwa hivyo, nitakwenda Makunduchi, nikitoka Makunduchi nitapitia Bwejuu, Jambiani na kurudi mjini. Kwa hivyo, ni vizuri kujua kwamba polisi leo bwana ndugu yetu Ismail Jussa amepanda baiskeli kutoka Makunduchi na yuko njiani, hivyo itasaidia sana kuweka usalama wake mwenyewe kwamba amejisajili. Kama mpaka saa mbili usiku hajaenda tena katika kituo cha polisi kuripoti kuwa nimesharudi safari yangu, inawezekana polisi pale ikatia mashaka na ikaanza kumtafuta katika maeneo ambayo alisema atapita kwa baiskeli yake. Hilo Mhe. Naibu Spika, nafikiri ni utaratibu mzuri ambao umekuja na hoja hapa kwamba ni vizuri kusajili jambo lolote na mtu asidharau jinsi ya kujisajili.

Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, mchango wangu huu nafikiri unatosha kwa nilivyochangia. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia, mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Koani, kuanzia sasa tunahakikisha kwamba tunajisajili kwa mambo yetu yote, hasa kwa vile tuko katika maeneo muhimu sana na nyeti katika maeneo yetu ya mashamba. Kwa hivyo, sina zaidi Mhe. Naibu Spika, naunga mkono kwa asilimia mia. Ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Abdalla Mohamed Ali: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi Magharibi haya kunipatia fursa ya kuzungumza machache katika mswada huu ambao wengi wanauona ni wa ufundi na ni kweli mswada huu ni wa ufundi, kwani naona wengi unatuchachafya hatujui tuanzie wapi wala tutokee wapi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kupata miswada mara hii, nimepata mawazo kwamba zile ziara zetu ambazo tunazifanya Wajumbe za kwenda China na kwengineko, basi zimeanza kutoa matunda, kwani mengi ambayo nimeyaona katika mswada tulioupitisha asubuhi, nafikiri ni matokeo ya ziara na sasa tunataka kuyaleta katika nchi yetu.

Pia mswada huu tulionao pia unanipa funzo hilo hilo, kwamba sasa tunataka kuondoka pale tulipo na tunataka kuingia sehemu nyengine. Lakini wasi wasi wangu ni kwamba wale tunaowaiga, wao tayari wanaanza kushuka ngazi na sisi tunaoiga tunapanda ngazi. Sasa waswahili wanasema mpanda ngazi na mshuka ngazi mara nyingi huwa hawakamatani mikono. Nachelea kwamba wale tunaowaiga wao tayari wanaanza kushuka ngazi na sisi tunaoiga tunapanda ngazi. Sasa Waswahili wanasema mpanda ngazi na mshuka ngazi mara nyingi huwa hawakamatani mikono.
Kwa hivyo, nachelea kwamba yale tunayoyaiga kwetu sisi yakawa ni mazito, kwamba hatuwezi kuyatekeleza au ni mazito katika utekelezaji wake basi itakuwa tunawanyonya wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, katika kuangalia mswada huu nimepata mawazo kwamba hili si jambo jipya, isipokuwa ni jambo kongwe na lipo. Lakini labda tumeona tunatafuta njia nyengine ya uhakika zaidi ya kutafuta mapato. Kwa maana hiyo, katika nchi yetu bado mapato ni mzigo kwa wananchi.

Sasa mimi mawazo yangu ni kwamba japo kuwa tunakuja na mswada au sheria nyengine, lakini kanuni na taratibu zitumike zile zile ambazo tulikuwa tunazitumia huko nyuma, kwani kuja na taratibu nyengine itakuwa ni kama kuwaongezea wananchi wetu mzigo, ambao kwao itakuwa ni tatizo.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwanza ningetaka ufafanuzi kuhusu masuala tofauti kwenye sheria hii. Kwanza ningetaka kujua ile taasisi ambayo itasajiliwa, je ikishasajiliwa shughuli zake itakazozifanya itakuwa ni zile tu ambazo imezisajili na imeziombea usajili au itaruhusika kufanya shughuli tofauti na zile ambazo imeziombea, ikiona kwamba kuna haja labda ya kufanya vile kwa wakati ule.

Kwa hivyo, nachelea kwamba au nikisema hilo ikiwa jawabu itakuwa ndio pengine je ni kwa ile kampuni ambayo itakuwa imekwenda kinyume ikajiingiza katika biashara au shughuli ambayo haikujisajili rasmi. Je kutakuwa na adhabu yoyote kwa kampuni ile imewekewa na itabidi pengine iingie katika makosa kufanya vile au haitokuwa na kosa lolote.

Kwa maana hiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho akanielekeza, kwa sababu sifa yetu sisi ni kuiga. Mhe. Naibu Spika, inawezekana pengine ikawa umesajili leo kwamba ni *contractor* wa ujenzi, lakini kesho ukaona mwenzako anafanya shughuli fulani ambayo ina faida zaidi na wewe ukajiingiza, sasa je, katika hayo ni vipi.

Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho akaniwekea wazi suala hilo.

Jengine labda ni vigezo gani vitatumika katika kuwatoza ada ya usajili ni upana wa ile kampuni yenyewe au ni mtaji, ambao pengine kampuni ile itakuwa inao, ndio kitakachotumika katika kumwambia wewe utawajibika ada yako iwe ni hii na wewe ada yako iwe ni hii.

Mhe. Naibu Spika, inawezekana pengine taasisi ikawa imekufa kufanya shughuli zake na yeye ikawa analo jina analitumia, hivi labda jina lile linaweza kutumika au kampuni nyengine kwa vile kampuni ile imekufa. Kwa hivyo, ni muda gani ambao utatolewa, ili kuiruhusu kampuni nyengine kutumia jina lile.

Mhe. Naibu Spika, nilipokuwa nikipitia mswada huu nilikuwa nikiwaza kwamba sisi tunaelekea katika usajili, yaani *registration*. Sasa hapa katika kueleza ufafanuzi wa maneno kuna neno mrajis, neno hili limepewa maana ya kuwa ni Mkurugenzi mtendaji. Kwa hivyo, lengo nini ni kupata Mkurugenzi mtendaji au ni kupata Mrajis ambaye atakuwa anaorodhesha hizo kampuni.

Kwa kweli mimi napata mawazo kwamba kwa sababu nafasi ya urajis pengine itakuwa ina mafao kidogo ukilinganisha na nafasi ya mkurugenzi mtendaji. Sasa labda hii nafasi tumeiunda kwa ajili ya kumuundia mtu mazingira tu ya kuwa yeye awe ni mtendaji, lakini sababu ya kusema kuwe na mkurugenzi mtendaji siioni.

Namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho anifafanulie na kwa nini tusitumie neno mrajis wakati tunakwenda kwenye *registration* na mrajis kwa kiswahili ni mtu ambaye anasajili mambo, kwa nini twende katika kutumia lugha hii ya mkurugenzi mtendaji na asibakie kuwa yeye ni mrajis.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, wakati atakapokuja hapa anipe ufafanuzi kwa nini turuke huko na tusibakie hapa kwenye urajis.

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba nizungumzie kuhusu kipengele kinachosema kwamba ikiwa kampuni mbili au watu wawili wanataka kusajili na wao wamekuja na jina moja, basi yule aliyekuja mwanzo ndiye atakayekuwa na fursa ya kusajiliwa ikilinganishwa aidha tarehe au saa aliyofikisha maombi yake, jambo hili sio baya.

Lakini Mhe. Naibu Spika, mara nyingi tunaposajili tunakwenda na uhalisia, kwa hiyo na hii ningependa nayo ikawa ni kigezo cha kumruhusu mtu kutumia jina lile. Mhe. Naibu Spika, kwa nini nasema hivyo, kwa sababu kuna aidha

kutafuta kwamba wewe unataka urahisi wa kujulikana au unataka kutafuta umaarufu wa ile nembo yako, ili wateja wavutike zaidi.

Kwa kweli haitokuwa rahisi kwamba kampuni labda iko Nungwi ikajiita kwa mfano Mji Mkongwe *Construction Limited* lakini ikawa iko Nungwi. Nadhani ni vyema tungekwenda tukaangalia kwamba huyu kwa vile yupo Mji Mkongwe na anataka kutumia hili jina la Mji Mkongwe, basi huyu apewe uwezekano zaidi, kwa sababu *location* yake ni Mji Mkongwe na sio Nungwi.

Sasa hili nalo nafikiria lingezingatiwa ule uhalisia wa kampuni yenyewe inataka kufanya nini, isijekuwa pengine kampuni hii inataka kuzalisha mwani lakini jina lake halilingani na ile kampuni ya mwani, isipokuwa itakuwa ni jina tu. Mhe. Naibu Spika, mambo haya nadhani wakati wa kuangalia ni jina gani iwepo kampuni moja na isiwe jengine basi tungeangalia zaidi.

Mhe. Naibu Spika, kama tulivyoona kwamba mswada huu kidogo unanichanganya, basi mimi nafikiri kwa leo ningemalizia hapa na kwa ujumla naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Marina Joel Thomas: Mhe. Naibu Spika, kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia siku hii ya leo nikiwa katika hali ya uzima na afya njema. Pili nakushukuru wewe Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi kuweza kuchangia mswada huu.

Tatu napenda kumpongeza Mhe. Hussein Ibrahim Makungu Mwakilishi wa Jimbo la Bububu kwa ushindi wa kishindo ambao ameupata. *(Makofi)*

Nne napenda kumpongeza Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria kwa kazi nzuri aliyoifanya ya kuandaa Mswada huu wa Sheria ya Usajili na Taasisi za Kibiashara.

Mhe. Naibu Spika, mimi naomba kuchangia kwenye ukurasa wa 99 kifungu cha 9(2), Mhe. Naibu Spika naomba kunukuu.

Kifungu cha 9(2) cha mswada kinaeleza hivi:-

> "Iwapo Mrajis atakataa kusajili jina lililopendekezwa atapaswa kutoa sababu kwa maandishi".

Mhe. Naibu Spika, katika hili naomba kutoa ushauri kwamba iundwe bodi, ambayo itapitia majina haya ambapo mrajis atatakiwa atie saini yake kuyapendekeza, lakini ikikaa bodi na kupitia majina basi hata yule mrajis kama atakuwa pengine labda jina la biashara hajalipenda kwa *interest* zake. Lakini ikipitia bodi ina maana bodi itachanganua yale majina na yatapatikana maamuzi ya pamoja, ili kumrahisishia mrajis kutoa maamuzi yaliyo sahihi.

Jambo jengine ili mswada au sheria hii itekelezeke vizuri, basi namuomba Mhe. Waziri kupitia kwao Mhe. Naibu Spika, aharakishe kuzitunga zile kanuni ambazo zitaweza kusaidia mswada au sheria hii iweze kutekelezeka ipasavyo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo naomba kuunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwanza nakushukuru kwa kunipa fursa hii angalau na mimi niseme machache kuhusu mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, mswada huu ni mfupi, lakini kusema kweli *context* yake ni nzito kufahamika. Vile vile ni kwa sababu mswada huu hatukupata semina, maana yake tungepata semina japo kidogo basi tungeweza kuchangia vizuri.

Mhe. Naibu Spika, kwani tunajua bila ya elimu ni tatizo ni sawa na kuwa kizani huoni isipokuwa kupapasa mpaka ubahatike kupata kile ulichokikusudia ni sawa na kuwa na ulemavu wa macho.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, kuanzishwa kwa sheria hii kutaleta ufanisi kwa kujua wafanyabiashara wangapi wanafanya biashara ya aina gani na hata kama ni mikopo, basi ni rahisi wafanyabiashara hawa kuwasaidia.

Mhe. Naibu Spika, matumaini yangu ni kwamba sasa baada ya kupitisha mswada huu wa sheria hii, basi hatua itakayofuata ni kuwasaidia kwa kuwapa mikopo, ili sasa biashara hizo ziweze kukua na kulisaidia taifa katika pato lake la taifa.

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba niingie kwenye vifungu vya mswada huu, ambapo kifungu cha 11 naomba kunukuu kidogo Mhe. Naibu Spika.

Kifungu cha 11 cha mswada kinaeleza hivi:-

> "Mrajis, iwapo atapokea maombi kwa maandishi anaweza kuzuia jina la taasisi kwa muda kabla ya kusajiliwa au mabadiliko ya jina la taasisi. Jina la taasisi litazuiwa kwa kipindi cha siku 30 au kipindi kisichozidi siku 60, iwapo Mrajis ataruhusu kwa sababu maalum na katika kipindi hicho hakuna taasisi itakayosajiliwa kwa jina hilo".

Mhe. Naibu Spika, hapa tungeona kwamba kwa sababu nafikiri kuna zile namba ambazo zitatumika kwenye usajili, basi zile zingekuwa ni muhimu zaidi kuzitizama zile namba za usajili na kuliko kusema tunatizama majina. Kwa mfano, mimi jina langu ni Fatma kwa hivyo nikaanza biashara yangu na kusema *Fatma and Sons* na akatokea mwengine akasema biashara ile ile pengine yupo Fatma mwengine na yeye akaita jina lile na likafanana. Lakini kutakuwa na namba ambazo ni za utambulisho na ndizo zitakazotusaidia kutambua ni Fatma gani mwenye *Enterprise*.

Sehemu ya nne kifungu cha 18(2) ambayo ina masharti mengineyo Mhe. Naibu Spika naomba kunukuu kidogo.

Kifungu cha 18(2) cha mswada kinaeleza hivi:-

> "Mtu yeyote anaweza kukagua kumbukumbu zinazohifadhiwa na Mrajis kwa kufuata vigezo na masharti kama ilivyoelezwa katika kanuni za Sheria hii".

Mhe. Naibu Spika, ni mtu yeyote tu kwa kweli hapa kidogo inanipa mashaka kwamba mtu yeyote anaweza kukagua kumbukumbu zinazohifadhiwa na mrajis kwa kufuata vigezo. Kwa hivyo, nafikiri kungekuwa na watu maalum ambao watakuwa na uwezo wa kukagua daftari la usajili.

Vile vile kwenye kifungu cha 20(1) ya sehemu hiyo ya nne Mhe. Naibu Spika naomba kunukuu kidogo.

Kifungu cha 20(1) cha mswada kinaeleza hivi:-

> "Mrajis anaweza kuunganisha makosa yatakayofanywa na mtu chini ya sheria hii au Kanuni za Sheria hii kwa kutamka mtu huyo kulipa faini iliyoelezwa kwa makosa hayo iwapo mhusika:-
>
> (a) Atakiri kwa maandishi kuwa ametenda kosa na hatorudia tena;

Mhe. Naibu Spika, mimi naona ni vizuri zaidi sheria hii kama alivyosema Mhe. Hamza Hassan Juma, kwamba wananchi wetu sheria hizi hawazitambui, kwa hiyo tusiwaadhibu watu bila ya kuwaelimisha na watu wanasema kwamba kutenda kosa si kosa kurejea kosa ndio kosa. Kwa hivyo, ni lazima kupitia vyombo vya habari pamoja na njia nyengine mbali mbali basi kuwajuilisha wananchi sheria hii ambayo ni muhimu kwetu.

Kifungu cha 22 cha mswada Mhe. Naibu Spika naomba kunukuu.

Kifungu cha 22(a) cha mswada kinaeleza hivi:-

> 22. "Mtu yeyote ambaye:-
>
> (a) Ni Mrajis atakataa au bila ya sababu zinazokubalika ataacha kuisajili taasisi au mambo yanayohusu taarifa za taasisi zilizowasilishwa kwake na muombaji na ambapo Mrajis

anatakiwa azisajili kwa mujibu wa sheria hii; ambayo iko katika Makosa yanayohusu Maofisa".

Mhe. Naibu Spika, kama kosa la afisa basi sioni sababu labda aadhibiwe mtu ambaye anafanya biashara au taasisi ya biashara ama ni shirika au *partnership*, lakini hili naliona kwamba kutosajiliwa au sijui sijafahamu. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika wakati atakapokuja kufanya majumuihso anifahamishe.

Madhumuni ya mswada huu kwa kweli ni mazuri na mswada huu wa sheria itakayoanzishwa wakala wa usajili wa biashara na mali, sasa hapa sijui hizi mali ni za aina gani. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika wakati atakapokuja kufanya majumuisho anifahamishe kuhusu masuala haya ya biashara na mali, je ni mali zote au ni za aina gani ama hata pengine ni baiskeli.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea hapo katika madhumuni na sababu kuhusu kuimarisha uwajibikaji ndani ya ofisi na miongoni mwa ofisi za taasisi nyengine kwa shughuli za usajili. Kwa kweli haya ni mambo muhimu na bila ya uwajibikaji basi dhana yote ile inakuwa mafanikio yake ni madogo. Kwa hivyo, ni lazima tuwe na uwajibikaji na huu ni msingi mkubwa ambao tunautegemea katika kufanikisha mambo yetu.

Vile vile kwenye madhumuni na sababu ni kuhakikisha kuwa kazi za wakala zinafanywa na wafanyakazi wenye sifa pamoja na ujuzi watakaowajibika kwa kuzingatia sheria, taaluma, uadilifu na maadili ya kazi.
Mhe. Naibu Spika, hili pia ni miongoni mwa mambo ya msingi sana, kwa sababu bila ya kuwa na sifa kwa kweli tutakuwa ni wababaishaji, kwani bila ya kuwa na ujuzi hatuwezi kufanya kitu na mazingatio ya sheria hii taaluma na uadilifu. Kwa hivyo, naunga mkono kwa kulitilia mkazo suala hili la uwajibikaji.

Baada ya hayo machache Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Asaa Othman Hamad: Mhe. Naibu Spika, awali ya yote nami nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa rehema zake na uwezo wake mkubwa ametujaalia jioni hii kurudi tena kwenye chombo chako hichi Baraza la Wawakilishi la Wananchi, kuwatendea yale ambayo wametutuma wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, na mimi niungane na wenzangu kumpongeza sana Mhe. Waziri mwenye dhamana ya wizara hii. Vile vile nimpongeze pia kwamba mswada umeandikwa lugha ni ya sheria, lakini kuna hekima na busara nyingi zimetumika.

Kwa kweli nikiri kwamba si rahisi sana kuona kilichomo. Kwa mfano, utasoma maandiko lakini kiini cha mambo ndio maana unatuona tumepita kwa wenzetu kutaka kujiridhisha na vile ambavyo tunaona ndivyo.

Mhe. Naibu Spika, mswada huu umeletwa si kwamba hapa tulipo au tunakotoka hakuna taasisi za kibiashara ama zile zinazokusanya kodi. Lakini alichokifanya Mhe. Waziri ni kwamba Zanzibar hatuna budi tuende sambamba na wenzetu dunia. Mhe. Naibu Spika, huwa nasema na leo narudia kusema kwamba Zanzibar ni visiwa, lakini hayo ni maumbile na wala hatutabaki kuwa kisiwa katika ile mtiririko wa mabadiliko ya kidunia. Mhe. Rais wa Zanzibar mara kwa mara anarudia neno tubadilike. Mhe. Naibu Spika, tubadilike kutoka huko tunakotoka, ili tufanane na wenzetu tuwe sambamba.

Mhe. Naibu Spika, mswada huu umeingia pia kwenye wimbi la mitandao kwa ajili ya kurahisisha mawasiliano pamoja na utekelezaji wa dhana iliyokusudiwa. Lakini bado mitandao hii na vyombo hivyo vya teknolojia vinatumiwa na sisi binadamu, havitofanya kazi kama sisi wenyewe hatujaamua kufanya kazi. Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba hili si lake peke yake isipokuwa ni letu sote. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, Zanzibar tunao wataalamu wakubwa tena wa fani tofauti wasomi, lakini tunalo tatizo moja hata wasomi wetu kuandika inakuwa ni tatizo na tuliobaki kusoma kwa maana ya kudurusu ni tatizo jengine. Sasa na ulimwengu huu tuliokuwa nao sasa ni hayo, maandiko kwa maana ya kwamba wasomi wanaandika sana hichi na kile kwa maana ya kubadilishana. Kwa hivyo, nadhani ni vyema tubadilike tuliobaki tusome hayo hayo yanayoandikwa. Mhe. Naibu Spika, kwa kufanya hivyo basi tutaweza kwenda sambamba na dhana iliyokusudiwa kwenye mswada huu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, wasi wasi wangu ni kwamba bado jinamizi la rushwa Zanzibar ni tatizo. Kwa kweli jinamizi hili mnasaba wake ni wapi mimi sijui. Lakini nashukuru Mhe. Waziri sijui kama anajua hilo ama ni katika zile busara na hekima ametaja adhabu pia hata kwa yule msajili kuna adhabu amezitaja ambazo zitatolewa.

Vile vile kuna sehemu moja inataja kwamba kutakuwa na fomu kule kwenye masuala ya kanuni. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika wakati atakapokuja kufanya majumuisho atueleze utaratibu wa fomu hizi zitapitia kwa wale wenzetu masheha, maana kwa uzoefu wangu kile kiini cha tatizo ndipo kinapoanza.

Sasa kama hivyo ndivyo basi taaluma kwamba itangulie tena kwa kasi kubwa kwa wao wenzetu waheshimiwa masheha pamoja na wananchi wetu wapate taaluma kubwa, ili wafahamu kwamba hii ni haki yao na pia ni wajibu kwao, hii ni nchi yao, kodi si jambo la utumwa isiwe ikaonekana ni udhia. Tufike mahali tuone kwamba ahisi udhia kama hajailipa ile kodi.

Mhe. Naibu Spika, madhumuni ni kupendekeza kutungwa kwa sheria mpya. Hii ni mpya kama hii ni mpya kongwe ipo, sasa kuna sababu zipi mpaka tukafikia mahali kutaka mpya. Kama tumefikia hapa tunatunga sheria mpya ni kujifunza kwa yale yote ya sheria kongwe yaliyotangulia yakatufikisha kwamba lazima tupate sheria mpya.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri katika madhumuni anasema kupunguza gharama za usajili pamoja na kuondoa msururu mkubwa katika kufanya taratibu za usajili. Hapa kakusidia urasimu, suala la urasimu linatajwa Zanzibar ni moja ambalo linatupotezea hata wale wanaonia ya kuwekeza. Mtu anazungushwa mwezi mmoja, miezi mitatu, sita mpaka mwaka, watu wenye fedha zao hawatoweza kazi hiyo.

Tulikaa tukakubaliana kwamba jamani katika suala hili la uwekezaji hebu tujaribuni kuwa na hii *One Stop Center*, lakini *One Stop Center* ile wanaofika pale si watu wenye maamuzi, mwenye maamuzi yupo ofisi kwake kwengine, afuatwe kwa wakati wake. Mfano wa hao sasa nasema kwamba ni miongoni mwa yanayokataliwa na sheria hii. Sasa ni vipi tumejipanga ili hayo yasitokee.

Mhe. Naibu Spika, nasisitiza sana na namuomba sana Mhe. Waziri itabidi amege muda. Pamoja na zile taasisi ambazo zitahusika na mambo haya kutoa taaluma kwa wananchi, umma wa Zanzibar. Narejea kusema kwamba hatuna uzoefu wa kujisomea, sasa jambo hili linataka angalau kusikilika mara kwa mara kwenye vyombo vyetu vya habari. Angalau hizi TV watu kwa kusikiliza taarifa za habari na matukio mbali mbali basi inapotokea hivi vipindi itasaidia sana na wao kujua kipi kinaendelea.

Naomba sana Mheshimiwa pamoja na kwamba sheria ni mpya inayopendekezwa. Lakini kuna adhabu ambazo zitakuja kuwakumba watu pengine kwa kutokuelewa tu. kama mtu ameelewa mapema asingesubiri hilo. Mhe. Waziri nakuomba sana utumie muda huo, ninavyokufahamu kwa busara zako na hekma ulizonazo bahati nzuri sana mwenyewe ni mwanasheria uliyeiva, mzawa wa nchi hii, hupendi wala hutopendeleapo kumuona Mzanzibari ananyanyasika ndani ya ardhi aliyozaliwa kwa jambo ambalo litakuwa na maslahi kwake mwenyewe naamini sana hilo. Niushauri tu katika mchango wangu kwamba huko nako ukutizame kwa namna stahiki.

Mhe. Spika, katika sheria pia kuna eneo pale Mhe. Waziri ndio nasema mwenzetu katika Sheria hii tumpongeze sana kwa busara na hekma aliyoitumia, pale anaposema kwamba wake waliotangulia kusajili kabla ya sheria hii ya sasa watahesabika na wao kwamba wameingia kwenye mkumbo huu. Lakini mbele kidogo baada ya mwaka wanaambiwa watatakiwa na wao wajisajili upya na ada zao, Kutokufanya hivyo itakuwa wametenda kosa na adhabu zitawakuta.

Nashukuru Mhe. Waziri ameikimbia sheria moja ambayo tumeletewa hapa ya leseni mpya, ikawa kidogo kuna stofahamu, wananchi walikuwa wakilalamika sana juu ya jambo lile. Kweli lilikuwa likikera, mtu amekata leseni mwezi uliopita anaambiwa leo akakate leseni mpya kwa gharama mpya. Hili nashukuru sana Mhe. Waziri amelikwepa sana kwa jitihada kubwa, haidhuru nia na malengo yaliyopo ni kutaka suala zima la makusanyo ya weze kwenda kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Naibu Spika, ushauri wangu waheshimiwa wajumbe wa Baraza lako tukufu katika shughuli zetu za kila siku kwa wananchi wetu pia tutumie nafasi hii ya kuwaelimisha wananchi wajibu lakini pia na madhumuni ya sheria hii. Tatizo letu kubwa hivi sasa ambalo lazima serikali itafute namna sio tu kulipunguza lakini pia kuliondoa kabisa.

Mhe. Naibu Spika, Zanzibar ni nchi ambayo sifa zake nzuri na nyingi zimeenea duniani. Lakini sasa kadiri siku zinavyokwenda tunapata uoza wa kupoteza sifa hizo nzuri. Suala hili la rushwa Mhe. Spika, hebu tutafuteni namna hasa ya kulidhibiti. Hapa pamoja na vyombo hivi vya *registration*, haoni ulazima mtu wa kuyatumia hayo ili hizo kumbukumbu zionekane zikae. Kamanda Mussa hapa alisema umuhimu mkubwa wa usajili hata madereva wetu wawemo kwenye kumbukumbu hizo, akataja mambo mengi muhimu na ni kweli, Lakini yanaingizwa na binaadamu kwenye hiyo mashine. Sasa kama binaadamu hakuyafanya hayo mashine itabaki haina kazi. Umuhimu mkubwa hapa ni uzalendo, tubadilikeni, tuacheni yale ambayo yaliyotutangulia huko nyuma.

Mhe. Naibu Spika, Mswada huu wenyewe hasa ni wataalamu wa sheria na sisi ambao tumo ndani ya chombo hiki hatuna budi tuweze na sisi kusema lolote kuwasaidia na wao ili umma ulioko huko nje wanaotusikiliza watusikilize waweze kuelewa na Ishallah kwa sababu mwenye dhamana ya wizara hii sifa nyingi anazo ni *Alhajji* kwa hiyo Baraka humu Mwenyezi ungu *In shaa Allah* atazimimina, usajili uwende na ufanisi mkubwa kama mambo yalivyokusudiwa.

Mhe. Naibu Spika, baada ya haya machache sana nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na nawashukuru sana Waheshimiwa wajumbe kwa utulivu wao wa kunisikiliza. Naunga mkono Mswada huu kwa asilimia mia moja na nawaomba Waheshimiwa wajumbe wauchangie na baadae waukubali kwa asilimia mia moja na ziada. Ahsante sana.

Mhe. Abdi Mosi Kombo: Ahante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii ya kuweza na mimi kuchangia kidogo Mswada wetu huu wa Sheria ya Usajili wa Taasisi za Biashara.

Mhe. Naibu Spika, hapa tunavifungu vitatu ambavyo vimetajwa mpaka vine, biashara binafsi, makampuni, na jumuia.Sheria hii tunazo za kusajiliwa, lakini tatizo kubwa ni ufanisi na utekelezaji wake. Wananchi wetu wanahitaji elimu ya kuelimishwa juu ya usajili na wafanyakazi wetu wanahitaji kuwa na imani ya wananchi wao juu ya kuwasajili. Wafanyabiashara tuliokuwa nao kuna makampuni na kuna wafanya biashara wadogo wadogo.

Mhe. Naibu Spika, wafanyabiashara wadogo wadogo wakati wanapotaka usajili huwa wanapata tabu sana ya kupata usajili wenyewe. Kwa hivyo naiomba Wizara wakati tutakapopitisha sheria hii basi ijitahidi sana kuwaelimisha wananchi na wizara ijitahidi sana wafanyakazi wake, maofisa wake wawasajili wananchi kwa uhakika.

Mhe. Asaa kama alivyosema kwamba nchi yetu imetawaliwa na rushwa, kwa hivyo upatikane ufanisi mkubwa sana kwa hivyo wizara ihakikishe kwamba wananchi wanasajiliwa kama inavyopitishwa sheria.

Mhe. Naibu Spika, mimi mchango wangu mfupi isipokuwa naishauri wizara iwaelimishe wananchi na ihakikishe inawasajili kiukweli. Mimi pamoja na wananchi wangu wa matemwe naunga mkono Mswada huu na hoja hii ya usajili. Ahante.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, awali ya yote napenda nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehma kwa kutujaalia kufika siku ya leo kuwa hai na hatimaye kutupa nguvu na uwezo wa kutoka katika maeneo yetu mpaka humu Barazani tena kwa miguu yetu bila kushikwa mkono.

Mhe. Naibu Spika, hii ni hazina kubwa aliyotujaalia *Allah* na kwa vyovyote hatuna budi kumshukuru. Pia nichakuwa mchache wa shukurani kama sikutumia fursa hii kukushukuru wewe kwa kuweza kunipatia fursa angalau na mimi kutia tia nyalio katika Mswada huu uliopo mbele yetu.

Mhe. Naibu Spika, siku za nyuma zilizopita nilisema kama kuna Mabunge ya *Common Wealth* yaliyotahatika kupata uongozi makini kwa maana ya Spika, na Naibu Spika, basi ni hili Baraza letu la Wawakilishi. Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, nimependezwa sana na jinsi wewe na Spika wetu mnavyoliendesha hili Baraza. Kwa hivyo kwa niaba ya wapiga kura wa jimbo la Wawi nasema asanteni sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nadhani sasa nichukue fursa hii kuipongeza serikali yetu ya GNU kwa kuweza kutuletea Mswada huu kwa kweli ni Mswada makini mno na kuna mambo sio tu kwamba umetayarishwa kiufundi lakini mpaka Mhe. Waziri wa Sheria wakati anautayarisha hata aliyekuwa hasikii basi alikuwa akisikia na kuona. Kwa hivyo napenda nimpongeze Mhe. Waziri wa Sheria na Ofisi yake kwa kazi nzuri waliyoifanya.

Mhe. Naibu Spika, kwa mnasaba huo nadhani sina sababu yoyote ya kuupinga Mswada huu. Kwa sababu kuna mambo ambayo yanahitaji kukwaruzwa na kuna mengine hayahitaji kukwaruzwa, Mswada huu hauhitaji kukwaruzwa hata kidogo katika Baraza hili. Kwa hivyo nawaomba wenzangu wasiukwaruze na waupitishe tu. Baada ya dibaji hiyo Mhe. Naibu Spika, nadhani sasa niende moja kwa moja katika Mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, jina fupi la Mswada huu linasema kwamba Sheria hii inajulikana kana Sheria ya Usajili wa Taasisi za Biashara Zanzibara ya Mwaka 2012. Mimi nilikuwa na hofu kidogo pamoja na kukamilika kwake Mswada huu vizuri lakini nimekuwa na hofu kidogo. Nadhani Mhe. Waziri wa Sheria, atakuja kunitoa hofu baadae katika vipengele hivi ninavyovitaja.

Kwanza usajili wa taasisi ya biashara, kuna biashara katika biashara hizi napata wasi wasi kwa sababu ni biashara ambazo zinahitaji msingi moja kwa moja, nakuna biashara za kitaaluma ambazo msingi wake ni ile taaluma ya taasisi au mtu aliyenayo. Hapa sasa nadhani Mhe. Naibu Spika, sijui Mhe. Waziri atanieleza nini. Kwa sababu kuna makundi ya watu na kuwa mmoja mmoja wanafanya biashara lakini hawana hata senti tano ya kuanzia. Kwa mfano kule kwa Mhe. Hija Hassan Hija kuna wataalamu katika matibabu ya kienyeji.

Mimi nadhani Mhe. Naibu Spika, utakapofika mwaka wa 2015, kama utakaa maeneo ya Mhe. Hija Hassan Hija pale nyumbani kwake basi sura nyingi hizi utaona zinaelekea kule kwa wataalamu, kabisa kabisa, wengine wanatoka Maskati, wengine Madina, wengine wapi wanaelekea Mwambe. Sasa hawa itakuwaje, hatutowatendea haki ikiwa hatukuwasajili, eti kwa sababu hawana msingi. Nadhani katika hili tusije tukafanya utaratibu wa kutowasajili wale wachoraji wa majengo. Lakini na hawa wataalamu wanaotoka kwa Mhe. Hija Hassan Hija kule Mwambe, sehemu za Nanguji, sehemu za Kiwani ambao wengi wanatumiwa na watu wengi humu, basi nadhani na wao katika hili tuwaangalie na tuwape usajili.

Mhe. Naibu Spika, nina wasi wasi wa hizi mali, mali zinapopatikana siku hizi zina matata. Mali nyingi zinazopatikana katika kipindi hichi hususan katika hizi nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara unawakutia vijana wadogo wadogo wameibuka na mamali hayo hujui hata wameyapatia wapi. Sasa ni kipimo gani Mhe. Waziri wa Sheria na Katiba hapa atwambie ni kipimo gani kinatumika katika kuziangalia mali na hatimaye kuzisajili. Mali nyengine zina matata Mheshimiwa. Unakutia wajukuu zetu tumewazaa juzi wanakupitia na mkoba wa ukili wanakwenda zao wapi huko hata wakirudi wana makontena ya pesa, biashara gani hii wanayoifanya.

Biashara inachukuliwa katika mkoba wa ukili anapita *Air Port* pale unamuona hasa ana kibrifkesi kadogo lakini akirudi pesa zake ni kontena zima. Usajili wa mali ya sampuli hii ndio nadhani Mhe. Waziri atueleze kwamba taasisi hizi zitakapokuja zitakuwa na kipimo cha kuangalia mali, isijekuwa tunasajili mali za sampuli hiyo na nyengine tunaambiwa zinatoka mali wapi huko zinakuja. Je, kutakuwa na kipimo?

Mhe. Naibu Spika, wakati naangalia katika madhumuni ya Mswada huu kifungu cha 1(3) kinasema “kuhakikisha kuwa kazi za wakala zinafanywa na wafanyakazi wenye sifa na ujuzi, watakaowajibika kwa kuzingatia sheria, taaluma, uwadilifu na maadili ya kazi”. Hili neno taaluma, wakati tunazungumza sasa hivi kuna vijana wengi wamewekeza maisha yao katika mambo haya ya *Forwarding and Clearing Agents,* elimu yake ni ya darasa la 6, lakini kazi anaifanya *efficiently,* kwa kweli wana uwezo mzuri hawa vijana. Sasa ukija ukisema kwamba humpi usajili kwa sababu taaluma yake ni ndogo mimi nadhani itakuwa hatuwatendea haki. Miaka yote kabla ya kuja hii sheria wapo pale na wanafanya kazi zao vizuri, wanatutolea gari zetu na kututunzia vizuri mali zetu. Leo tukisema hatuwasajili kwa sababu hawana taaluma, hapo itakuwa hatukuwatendea haki.

Mhe. Waziri utakapokuja hapa ututoe wasi wasi na mashaka, haya makampuni ambayo tayari yamewekeza katika mambo hayo lakini wamiliki wake hawana taaluma je, mtawasajili au hamtowasajili. Mimi naomba muwasajili kwa sababu wamefanya vizuri katika kipindi kirefu.

Mhe. Naibu Spika, Mswada huu kama tulivyosema hautiliki mkono, kuja kukosoa ni sawa sawa na mfinyanzi kufinyanga chungu chake ukaja ukasema unakirekebisha badala ya kukipikia tu, utakivunja. Kwa mnasaba huo, mimi ni Mwakilishi wa Jimbo la Wawi kwa niaba ya wapiga kura wangu naunga mkono Mswada huu kwa asilia mia moja. Lakini utakapokuja hapa unitowe wasi wasi kuhusu wale wataalamu wa Muwambe na hawa vijana wetu ambao tayari wana kampuni zao lakini taaluma yao ni ndogo, ili uniweke sawa. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Naona Waheshimiwa wachangiaji wamemalizika kwa tunavyokwenda. Kuna tangazo kabla sijaahirisha kikao.

Naomba kuwatangazia kwamba siku ya Jumapili ya tarehe 14 saa 3:00 za asubuhi itakuja Tume ya kukusanya maoni ya Katiba na tutakutana katika ukumbi wa juu hapo asubuhi na mapema saa 3:00. Kwa hivyo kila mmoja ataitwa atatoa maoni yake, wale watakaoshindwa kutoa kwa maelezo wataruhusiwa kuandika. Tunachoomba kwenu kwamba tumeshauriwa je, itangazwe moja kwa moja au wachukue wenyewe *record* zao tu.

Baada ya hayo kwa muda uliobakia dakika 25, naona Mhe. Waziri hatoweza kufanya majumuisho, kwa hivyo tunampa muda aende akakae na wataalamu wake kesho baada ya maswali na majibu tutamwita ili aweze kufanya majumuisho na kupitisha vifungu. Naakhirisha kikao chetu hichi hadi kesho siku ya Ijumaa tarehe 12 saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 1:20 usiku Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 12/10/2012 saa 3:00 za asubuhi)